# AGANO LA KALE.

Biblia imegawanyika katika sehemu kuu mbili nazo Ni:-

i. Kitabu cha Mwanzo hadi Malaki (Agano la Kale)
ii. Kitabu cha Mathayo hadi Ufunuo (Agano Jipya)

## KITABU CHA MWANZO HADI MALAKI (AGANO LA KALE)

Agano la kale limegawanyika katika sehemu kuu 5 yaani

i. Vitabu vya Musa (Mwanzo, Kutoka, Lawi, Hesabu na Kumbukumbu la torati) hivi utambulika kama vitabu vya Musa au vitabu vya sheria.
ii. Manabii wakubwa (Isaya, Yeremia, Daniel, Ezekiel na Maombolezo)
iii. Manabii wadogo (Amos, Yoel, Obadia, Yona, Mika,Nahumu, Habakuki, Sefania ,Zekali , Hagai na Malaki)
   Hivi vitabu vyote ujulikana Kama avitabu vya manabii.
iv. Vitabu vya historia (Yoshua, Waamuzi, Wafalme, Mambo ya Nyakati N.k)
v. Vitabu vya mashairi/nyimbo (Zaburi Ayubu, Wimbo Ulio Bora, Methali na Muhubili)

**NB:** Katika biblia agano la kale linatajwa kama maandiko matakatifu, ahadi na wakati

Mwingine walinukuu kama mwanzo unapokutana na neno akaanza kutoka Musa au

Vitabu vya sheria au Torati wanamaanisha vitabu vya Musa na inapoandikwa na pamoja na vitabu vya historian a akisema zaburi alimaanisha vitabu vyote vya mashairi. **Hivyo katika biblia agano la kale linafahamika kama vitabu vya Musa manabii na zaburi au maandiko matakatifu.**

## SABABU ZA KUSOMA AGANO LA KALE.

i. Yesu mwenyewe alilikubali agano la kale kama utimilifu wa neno la Mungu Mathayo 5.7

ii. Yesu na wanafunzi wake walifundisha habari za wokovu na kufa na kufuka kwa Yesu Kristo kupitia Agano la kale pia kuna habibu rejea au nukuu au mistari Zaidi ya 600 iliyonukuliwa kwenye agano jipya kutoka kwenye agano la kale kikiongozwa na kitabu cha mathayo chenye nukuu 120 kutoka katika agano la kale.

iii. Katika agano la kale tunapata mianzo ya habari za wokovu, ondoleo la dhambi, mwanzo wa Imani na mwanzo wa dhambi pia ni kitabu kinachokubaliwa na dini nyingi kama vile waislam, wakristo na wayahudi n.k

iv. Agano la kale linawakilisha agano jipya lililofichwa likieleza habari za wokovu wa Yesu kristo kwa kutumia mafumbo, lugha ya picha na mifano kadha wa kadha kueleza habari za wokovu na linaonyesha ahadi tangu mwanzo Mungu alivyompenda mwanadamu na kutaka kumuokoa katika ulimwengu huu wa dhambi kwa njia ya kumwamini Yesu Kristo kama ahadi ya Mungu na masihi ajaye ambao utimilifu wa mambo haya ni katika agano jipya.

**YESU NA WANAFUNZI WAKE WALILIKUBALI AGANO LA KALE.**

| | |
|---|---|
| Yesu alidai maandiko ya agano la kale yapo kwa ajili ya kuelekeza watu kuja kwake ili wamwamini wapate uzima wa milele | Yohana 5:39-40 |
| Filipo alithibitisha Yesu Kristo aliandikiwa habari zake katika | Yohana 1:45 |
| Yesu alisema watu wanapaswa kumuamini kama maandiko yasemavyo (yaani maandiko ya agano la kale) | Yohana 7:38-39 |
| Mtume Paulo alitumia zaburi kufundisha kufa na kufufuka kwa yesu Kristo alitumia zaburi ya 16:8-9 pamoja na zaburi ya pili kuthibitisha ufufuo wa Yesu Kristo | Matendo ya mitume 13:15-34 kwa kifupi na haraka Zaidi Matendo ya mitume 13:33-39 |
| Yesu alikiri kuwa iliandikwa katika agano la kale lote pamoja na zaburi habari zake za kufa na kufufuka kwake pia aliwafundisha wanafunzi wake habari za wokovu kuanzia musa, manabii na zaburi akimaanisha agano la kale lote lilikuwa noi kivuli cha mambo yatakayomkuta Yesu Kristo | Luka 24:26-27<br>Luka 24:44-47 |

| | |
|---|---|
| Hata mtume petro mwanafunzi wa Yesu akuishia tu kumuona yesu na miujiza yake bali alimuamini kwa sababu aliyoyafanya yote yalikuwa yameandikwa katika maandiko matakatifu (yaani agano la kale) | Matendo ya mitume 3:18-26<br>Anaposema kitabu cha Samwel soma waebrania 11:23<br>Matendo ya mitume 2:14-36 hapa tunaona petro akinukuu katika kitabu cha Yoel pamoja na zaburi ya 16 habari za kujazwa roho mtakatifu, kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo na wokovu utakaowafikila watu wote watakao mwamini Yesu Kristo |
| Yesu alisema habari zake za kufa na kufufuka ili kila amwaminie hapate kuhesabiwa haki bure mbele za Mungu habari hizi zilaindikwa na Musa mtu asipoamini maneno ya Musa awezi kuamini habari za Yesu Kristo | Yohana 5:45-47 |

Agano la kale linatusaidia vema agano jipya na kuelewa historia ya wokovu, Imani, ahadi ya Mungu ya kumleta Yesu Kristo aliye bwana na mwokozi.

Kwanini tunasoma agano la kale*!!

**UMUHIMU WA AGANO LA KALE KWA MSOMAJI BIBLIA***

- Tunaposema agano la kale Kwa mktadha wa biblia kama vitabu 66, tuna maanisha vitabu 39, kuanzia mwanzo Hadi Malaki.
- Mwanzo mpka Malaki ndio Kwa jina lingine yanaitwa maandiko matakatifu, ninaposema maandiko matakatifu ni kwamba mara nyingi tunakutana na sentensi nyingi katika vitabu 29 vya agano jipya vinavyosema *kuwa kama ilivyoandikwa* au *kama inavyosemwa* *kama tusomapo* , katika *maandiko matakatifu*

Kwahiyo kumbe kama kwenye agano jipya tunaona sentence za kama ilivyoandikwa kwenye maandiko matakatifu Ina maana kwamba agano jipya sio maandiko matakatifu Bali ni fafanuzi za maandiko matakatifu,

Agano la kale limebeba ujumbe umoja ambao ndio huohuo upo kwenye agano jipya

Agano la kale yaani mwanzo mpaka Malaki sio story nyingi kama wengi wanavyoona kama zilivyo Bali ni ujumbe wa wokovu KUPITIA kazi ya msalaba

yaani kufa na kufufuka Kwa yesu kristo.. Kwahiyo agano la kale ni maandiko yanayotabiri habari za yesu tu... ila ni kwa mifano na misemo na kivuli cha vitu.

***Yohana 5:39-41, 45-47***

Kumbe kwenye maandiko ameandikwa yesu ..

Hakuna ujumbe mwingine isipokuwa wokovu wa yesu kristo pekee

*1 Petro 1:8-12*

Yesu mwenyewe anathibitisha haya kwenye vitabu vya injili baada ya kufufuka kwake kwamba maandiko yaote yaani mwanzo mpka Malaki ni habari zake yeye sio mapichapicha wanayoyaona watu

*Luk 24:25-27, 44-47*

✡ Luka anaonesha kuwa yesu hakuishia kuwaambia kwamba yeye ndiye aliyeandikwa, Bali aliwafundisha namna nzuri ya kusoma agano la kale na kuona ujumbe sahihi wa kristo katika wokovu wake kwenye hivyo vivuli,,. *Yaani aliwafunulia akili zao wapate kuelewa maandiko*

Tunaona baada ya wanafunzi kusubiri yerusalem hata wajaze uwezo kutoka juu, ili wawe mashahidi wa huo wokovu, wanaanza kufundisha na kumfunua kristo katika maandiko hayo yaani mwanzo mpka Malaki,

✡ Iko hivi kipindi wanafunzi au mitume wa yesu wanahubiri injili, hapakuwepo vitabu vya agano jipya, ila wao walihubiri habari za kristo na wokovu wake yaani kufa na kufufuka kwake wakionesha ushahidi kupitia mwanzo mpka Malaki,

Matendo ya mitume 2: 14-32

Petro anafafanua Joel 2:28-30. Zaburi 16

Matendo ya mitume 3:11-20, 22-24,

Hapa pia ni mafafanuzi ya agano la kale

Matendo 13:32-27

Ufafanuzi wa agano la kale..

Nimalizie Kwa kusema hivi Kuna ushahidi mwingi unaonesha agano la kale ni habari za yesu na wokovu wake sio story zile tuzionazo Bali asomaje Kwa uangalifu na kufuata kanuni za usomaji anamuona kristo tu, amen

*We are not trust in your imagination or your preach but we trust in Bible.*
*2 Petro 1:19-20*

**SABABU TANO ZINAZO TUFANYA TUAMINI MUNGU YUPO**
**(The 5 reasons to believe entrance of God)**
Mungu muumba mbingu na nchi kwa mapenzi yake amejifunua kwa watu wake na kutujulisha uwepo wake kwa njia kuu mbili

1) **SPECIAL REVELATION**
2) **NATURE REVELATION**

**SPECIAL REVELATION**

- Huu ni ufunuo wa kipekee kwa sababu ujumbe huu haukuja kwa njia ya asili bali ulikuwa ni ufunuo maalumu kutoka kwa MUNGU na haukutokana na njia za kibinadamu au utashi wa mtu au mazingira bali ulitoka kwa mungu mwenyewe pasipo mchango wa mwanadamu au mazingira watu walipokea tu ushuhuda yaani wa neno la mungu yani vitabu vyake (bibilia ), malaika zake, manabii wake , mitume wake,
  kwa ushahidi wa ishara ,maajabu na mazihilisho ya nguvu ,upendo,na jina lake .

- kama ilivo andikwa **( waibrania 2 :3-4)** mimi nauliuza sisi tutapataje kupona tukiuzalau ukweli huu namna hii ambao ulinenwa na mungu mwenyewe kisha ukaletwa kwetu kupitia wajumbe wake malaika , manabii,mitume etc na kuzibitishwa neno lake kwa ishala na maajabu na kwa nguvu na upendo namna hii.

**NATURAL REVERATION**

Hii ni njia ya kawaida ya asili kwa kutumia akili na sayansi za mazingila yanakili uwepo wa Mungu.

Hata Mimi **mtumishi kidigitali (ANIL BLASTER)** nathubutu kusema ni mpumbavu pekee na kafili ambaye akili zake zimekufa anaweza kusema hakuna Mungu.

Kama ilivyo andikwa kwenye maandiko matakatifu **( zaburi 14:1)** mpumbavu kasema hakuna Mungu pia **( yuda 1:4)** makafili ndio wanao badili neema ya Mungu kuwa ufisadi na kumkana Mungu mmoja na wa pekee.

**ZIFATAZO NI SABABU 5 KUWA MUNGU YUPO SABABU ZA NATURAL REVELATION NA NIKIZIBITISHA KWA KUTUMIA SPECIAL REVELATION**

Natural Revelation

1. **Cosmological argument kila kitu unacho kiona ulimwenguni kimesababishwa.**

Ever thing that exists has cause ni makubaliano ya kisayansi na falsafa na ndio ukweli kila unacho kiona ulimwenguni kuna kisababishi chake au kuna mtu amekifanya kiwepo.

kwa sababu hii ya cosmological factor tunaamini hata ulimwenguni yupo aliye umba Sayansi inasema ni super natural power waki likwepa kwa makusudi neno la Mungu ukweli hakuna super nature power nyuma ya kuumbwa ulimwengu bali yupo Mungu **THE MIGHT AND POWER FULL LIVING GOD.**

**UDHIBITISHO WA SPECIAL REVELATION (BIBLE SCRIPTURE)**

Neno la Mungu lina dhibitisha kua Mungu ndiye muumbaji

**(Mwanzo 1:1, isaya 45:18 isaya 42:5)** inadhibitisha kuwa Mungu ndiye aliye ziumba mbingu na nchi.

**Je, yesu ni muhusika wa uumbaji wa mbingu na nchi?**

Ndio muhusika (**wakolosai 1:12-18 yohana 1:1-14 yohana 14:9 yohana 1:8)** maandiko haya yana dhibitisha kua Yesu ndiye muumbaji

2. **TEOLOGICAL ARGRUMENT/ UNIVERSAL DESIGN**
   The low of design inasema kila design ina design wake hivyo mpangilio mzuri wa ulimwengu haupo kibahati mbaya yupo aliye design ambapo. Wana sayansi wanasema super natural power ukweli nikwamba hakuna super natural power bali ni Mungu ndiye aliye design.

**UDHIBITISHO WA SPECIAL REVELATION (BIBLE SCRIPTURE)**

Neno la Mungu (**mwanzo 2:1 kutoka 31:17 zaburi 8:3 zaburi 102:25)**

**Swali: je, Yesu anahusika katika ku design ulimwengu?**

Ndio (**wafilipi 2:4-12 yohana 5:15-19 yohana 1:1-4 waibrania 2:8-15)** maandiko haya machache katika mengi yana dhibitisha kuwa Yesu ni muumbaji.

3. **POWER ENCOUNTER/EYES WITNESS ENCOUNTER (USHAHIDI WA MACHO)**

   Huu ni udhibisho wa ushahidi wa moja kwa moja wa matukio ambayo Mungu amefanya katikati ya maisha ya mwanadamu na ushuhuda huu wa nguvu za Mungu umedhibitika kwa watu tumeshuhudia mungu akiponya, akiokoa, akiuwisha pia pepo akitolewa kwa nguvu za Mungu pamoja na matukio mbalimbali yanayo onyesha msaada wa nguvu za Mungu.

**UDHIBITISHO WA SPECIAL REVELATION (BIBLE SCRIPTURE)**

Mungu mwenyewe hupenda kuonyesha nguvu zake, upendo wake ili ajulikane na watu. kwa sababu watu wote waliumbwa na wana samehewa na Mungu, kuhudumiwa kwa upendo wa kimungu ili wazitangaze sifa za Mungu ulimwenguni **(1petro 2:9 zaburi 66:2 isaya 43:21)**

Ndivyo ilivyo Mungu hupenda kujulikana ulimwenguni amebariki, anaokoa, anaponya, anafanikisha, anasamehe ili ulimwengu wote umjuwe.

**(Mwanzo 12:1-3, wagalatia 3:6-11)** Mungu ali mbariki Ibrahimu ili kupitia Ibrahimu Baraka zake zijulikane ulimwenguni kote na watu wabarikiwe.

**Walawi 22:23** Mungu alileta sabato ili tujuwe yeye ndiye mwenye kututakasa na amesha kwisha kutakasa kwa kumleta **BWANA WA SABATO YESU KRISTO** atutakasae kwa damu yake na kutupa pumziko la milele.

**Swali je, kupitia Yesu kristo nguvu za Mungu zinaonekana?**

Ndio kwa kupitia imani katika jina la Yesu kristo nguvu za Mungu zina dhihirika **yohana 14:12-14.**

kwa kushika amri ya Yesu yaani imani na upendo nguvu za Mungu hudhihilika kwetu yani upendo, msamaha wa dhambi, uzima wa milele na kazi na ishara za Mungu hutendeka kwetu na tunapata kibali cha kumwendea Mungu (**wagalatia**

**2:16, waefeso 2:13, waibrania 12:24, yohana 14:15, petro 1:1-2, 1yohana 1:7)** hivyo nguvu ya Mungu inajulikana kupitia Yesu kristo.

1. Ukweli Mungu alimuumba mwanadamu ili amuabudu hivyo kila **ontological argument every culture have idea of God in their meaning.**

Mwanadamu ana wazo na uwaminiu ndani ya nafsi yake kuwa kuna Mungu na hii ina dhibitika tamaduni zote ulimwenguni huwa zina tabia ya kuabudu na kuamini kuwa Mungu yupo.

The idea of invisible support super natural power ina shuhudiwa ndani ya kila aliye hai huu ni udhibitisho kuwa Mungu yupo hivyo tuna ushahidi wa dhamiri zetu zina shuhudia kuwa Mungu yupo na jamii zote za kibinadamu zina Idea of worship.

## UDHIBITISHO WA SPECIAL REVELATION (BIBLE SCRIPTURE)

Maandiko matakatifu yana dhibitisha Mungu yupo anaye stahili kuabudiwa na wanadamu **(kutoka 20:2-4, kutoka 34:14, kumbukumbu la torati 6:14, zaburi 81:19)** huu ni ushuhuda kuwa Mungu ndiye aliye weka kiu ya wandamu kuabudu na yeye ndiye anae paswa kuabudiwa.

**Swali, Yesu ni nani hata ahusike kwenye kuabudu Mungu?**

kupitia Yesu tumemjua Mungu wa kweli hivyo Yesu ni njia **yohana 14:6,** tunapata msamaha wa dhambi kwa njia ya kuamini kazi ya msalaba wa Yesu **wakolosai 1:14,** tuna hesabiwa haki na Mungu kwa njia ya kumuamini Yesu pia tuna muomba Mungu kwa jina la Yesu **yohana 14:13-17**. Hivyo tukitaka kumuabudu Mungu wa kweli lazima tumuamini Yesu kristo.

## MORAL ARGUMENT, WE BORN WITH IT

Hizi ni tabia ambazo wanadamu tumezaliwa nazo na zipo katika jamii zote hatujafundishwa na mtu nazo zinadhibitisha kuwa Mungu yupo anae zisimamia pasingekuwa na Mungu hizi tabia zisinge jidhihilisha mfano upendo, vipaji nk. mfano hakuna jamii ya kibinadamu inayo ruhusu mtu kulala na mama yake, mauwaji nk.

## UDHIBITISHO WA SPECIAL REVELATION (BIBLE SCRIPTURE)

**Waefeso 2:10** inatufundisha kua tumeumbwa na Mungu na ndiye aliye weka upendo, huruma, vipawa ndani ya wanadamu inasema maana tu kazi yake tuliumbwa katika kristo Yesu tutende matendo mema ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tutende katika hayo.

**Swali, je, inasaidia nini kumwamini Yesu kwa habari ya mwenendo wa tabia zetu?**

**Yohana 3:16,tito 2:11-12** inatufundisha Yesu alikuja ulimwenguni ili kuleta ukombozi kwa mwanadamu aliyepote na kuacha tabia ya Mungu na kwa kifo chake amelipia makosa ya wanadamu wote na kwa kufufuka kwake watu wote wapate haki isiyo tokana na mwenendo wala tabia zao.

**Tito 2:14** inasema alijitoa nafsi yake kwaajili yetu ili atukomboe na maasi yote na kusafisha watu wawe miriki yake mwenyewe wale walio najuhudi katika kutenda mema hivyo wanao mwamini Yesu wanapokea msamaha wa dhambi na uzima wa milele, ana wajibu wa kutenda mema maana asili ya imani hii ni upendo na yesu ndiye atupatiae nguvu ya kutenda ili tumwakilishe katika jamii (**waefeso 2:10,1timotheo 5:10, tito 3:8, tito 3:14.**)

**Hivyo ukiamini upendo wa Mungu kupitia kufa na kufufuka kwa Yesu kristo tutapata kupokea upendo wa Mungu, msamaha, uzima wa milele, na swawabu ya roho mtakatifu atupae nguvu ya kutenda mema**

## VIPINDI 7 VYA KANISA SAWA SAWA NA UNABII WA MAKANISA SABA YA KITABU CHA UFUNUO WA YOHANA.

Kwa sababu Ukiristu siyo Falsafa, Sera, Imagination wala sio mawazo ya Kifilosophia bali ni Imani na nguvu ya Mungu iletayo wokovu kwa kila mtu ahaminiye **(War. 1:16).** Hivyo kanisa limepitia nyakati mbalimbali ngumu lakini limeshinda **(War. 8:35-39)** kwa sababu hakuna kitakachowatenga wakristo (waamini) na upendo wa Mungu **(War.8:31-39)** ndio maana kanisa (waumini) wapo mpaka leo ulimwenguni sawasawa na neno alilosema Yesu katika **(Math.16:18)** ya kwamba nitalijenga kanisa wala malango ya kuzimu alitalishinda, ndio sababu dunia na serikali na shetani wameshindwa kabisa kulifuta kanisa (waumini) wakristo duniani. **(Mdo. 5:38-39)**

Kwa sababu kanisa sio kampuni, mradi, shirika na halipo kwa sababu kumnenepesha mtu bali ni ushirika kamili wa Mungu na mwanadamu katika roho. **(Kor. 1:6-19-20)** ndio maana hadi leo lipokanisa duniani

Kanisa au waumini au Mkristo imempasa kutoshangaa au kukata tamaa pale yeye mwenyewe au huduma yake inapopingwa, kukataliwa, kupuuzwa, kuzushiwa na kususiwa bali imempasa aamini atashinda **(War. 8:37), (Wafl. 1:14), (1 Yoh. 5:1-5)**

Waamini (wakristo) imempasa kukumbuka na kutambua ukweli wa historia kuwa Ukristo umekuwa ukipingwa tangu mwanzo lakini umekuwa ukishinda na Ukristo upo mpaka leo Duniani. **(Zab. 129:2)**

- ***Wayahudi,*** walipinga Ukristo kwa kutumia pesa, vitisho wakiuona kuwa ni uhadui wa mafundisho ya Musa, lakini kanisa lilishinda Injili ikatoka Yerusalemu, Samalia na Yudea Hatimaye ikafika Rumi. (Mdo 5:17-20).

- ***Warumi,*** walipinga Ukristo kwa sababu Ukristo uliwaweka watu wote katika usawa wakati huo warumi walipendelea raia wa Rumi kuwa bora kuliko wengine. Hivyo waliona kuwa Ukristo kuwa ni tishio kwa siasa na Dola la Rumi na kanisa likashinda mateso makali kutoka kwa warumi hatimaye likafika Yunani.(Mdo. 22:28)

- ***Wayunani,*** waliupinga Ukristo wakio kuwa ni ujing na upuuzi, lakini kanisa lilishinda na hatimaye likaufikia ulimwengu wote. (1 Kor.1:23 )

- ***Waislamu,*** waliotokea karne ya 6 sawa na miaka 500 tangu kufa na kufufuka kwa Yesu na kupaa. Ajabu na inasikitisha japo waliukuta Ukristo umekwisha enea sana Ulimwenguni waliupinga na kukataa Uungu wa Yesu utatu Mtakatifu, roho mtakatifu, uweza wa jina la Yesu n.k wakapambana kuufuta Ukristo lakini kanisa limeshinda hata leo watu wanaokoka, jina la Yesu linaubiliwa na watu wanabatizwa na wananena kwa lugha.

**Vifuatavyo Vipindi 7 vya Kanisa Sawa Sawa na Unabii wa Makanisa Saba ya Kitabu cha Ufunuo wa Yohana.**

Makanisa 7 yalikua Asia ndogo (Uturuki ya leo) na yalikua karibu karibu kiasi kwamba unaweza kutembea kwa miguu kwenda moja hata jingine.

Japokua nabii za Yesu zilihusu makanisa lakini pia ujumbe ulilenga kwa mtu mmoja mmoja, na Yesu Kristo alijifunua kwa Yohana kama Mwokozi, Mfalme na Hakimu.

Mazingira yalikua yakiathiri makanisa. Kwa mfano;

- Efeso iliathiriwa na mazingira ya uchumi na siasa wakaacha upendo
- Smirna iliathiriwa na mazingira ya upinzani (mateso) mkali kutoka nje ili kuipinga Imani
- Pergamo iliathiriwa na mazingira ya kuteseka ndani ya kanisa kupitia mafundisho potofu
- Thiatira iliathiriwa na mzingira ya kusaka uchumi na kuacha Imani
- Sardi iliathiriwa na mazingira ya maisha rahisi kwa uchumi mzuri
- Filadelfia iliathiriwa na mazingira ya kijiografia

- Laodikia iliathiriwa na mazingira ya kiroho cha Uongo (vuguvugu na kujisikia)

Shetani amekua akitumia mazingira kutuhamisha kutoka kwenye hali ya ushirika/uhusiano na Mungu, bado ni mpango wa Mungu kutumia kila aina ya mazingira kutupa ushindi wa Kiroho.

1. **KIPINDI CHA MITUME (33BK HADI 100BK)** Kinawakilishwa na kanisa la Efeso **(Ufu. 2:1-7)**.

   Kipindi hiki kinaanzia pale siku ya Pentekoste 33BK hadi 100BK mitume wote walipokua wamekufa, kwa historia Zaidi soma kitabu cha Matendo ya Mitume jinsi kanisa lilivyoanza na kuenea ulimwenguni. Ukweli kwamba wakristo wakati huu walipitia changamoto nyingi ikiwemo baraza la wazee, serikali ya Rumi walishinda lakini wengi walipunguza upendo wa kwanza lakini Yesu anawaonya waukumbuke upendo wa kwanza **(2 Tim. 2:4-10).**

   ***Ujumbe binafsi, japokua tunapitia changamoto nyingi katika maisha ya Kiroho imetupasa kutokuacha upendo wa kwanza katika maisha ya Kiroho, wito wa Yesu ni mtu kukumbuka wapi alipoanguka na kutubu. (Ufu. 2:4-5)***

2. **KIPINDI CHA MATESO YA KANISA (100BK HADI 312BK)** kinawakilishwa na kanisa la Smirna.

   Kipindi hiki Dola ya Rumi ikiongozwa na Kaizali Nelo kwa kuwauwa mitume wote na kuwatesa wakristo kama Yesu alivyotabili watakua katika dhiki kwa awamu kumi, kuna unabii ulimaanisha nyakati 10 na awamu kumi za wafalme kumi wa Dola la Rumi walitesa kanisa. Hivyo Yesu aliwataka waamini kuwa waaminifu hadi kufa.

   ***Ujumbe binafsi, kweli kuu ya kitabu hiki ni uhaminifu hadi kifoni na jinsi ya kubaki muaminifu katika mateso na majaribu. Yesu ana ahidi taji ya uzima.***

3. **KIPINDI CHA UPAGANI WA KANISA (312BK HADI 590BK) kina wakilishwa na** kanisa la pergamo.

   Kipindi hiki kilianza baada ya mtawala Constantino kuamini na kuanzisha sheria ya milani iliyopendelea Ukristo kwa kujenga makanisa, kuwalipa posho watumishi wa Mungu, akakomesha mateso na wakristo walipata nafasi ya ajira kiurahisi na kupata vyeo serikalini. Hivyo ikasababisha watu wengi waliookoka wakati huo walifuata maslahi japo walikua wanaitwa wakristo lakini awakuwa waaminifu ikapelekea kanisa kuwa la kipagani.

*Ujumbe binafsi, japokua Yesu aliwapongeza wakristo walioshika jina lake kwa uhaminifu nakua na msimamo juu ya upinzani uliokuwepo wa kuabudu miungu na Kaizali, lakini aliwaonya wale ambao hawakushika Imani sawasawa na kufuata mafundisho potofu. (Kuabudu) miungu Yesu aliwaonya akasema tubu na kuishika Imani ya Yesu.*

4. **KIPINDI CHA MAOVU YA KANISA (590BK HADI 1517BK)** kina wakilishwa na kanisa la Thiatia.**(Ufu. 2:18-29)**

   Baada ya kanisa kuingia katika upagani ulioletwa na Muunganiko wa serikali na kanisa, walianzisha ibada za kitapeli kama vilekuombea wafu, kuuza na kununua cheti cha msamaha, ibada za wafu, kubatiza kwa maji machache, ibada za bikira maria. n.k.

   *Ujumbe binfsi, ni msisistizo wa kutunza matendo matakatifu hadi mwisho.*

5. **KIPINDI CHA MATENGENEZO YA KANISA (1500BK HADI 1700BK)** kina wakilishwa na kanisa la sardi. **(Ufu. 3:6)**

   Pamoja na kipindi hiki kanisa lilikua limekufa lilikua na jina tu ila kanisa lilikua limekufa lakini walikuwepo waamini wachache tu lakini Yesu anawajua walianza mapendo kutoka katika  kanisa la Roma na kujenga upya Imani ya Ukristo. Mfano; Ruta King, John Kelvin n.k.

   *Ujumbe binafsi, siku zote Mungu ana mashahidi wake waaminifu katika hali yoyote, hivyo ni jukumu letu wote kuwa waaminifu.*

6. **KIPINDI CHA UMISHENI WA KANISA (1700BK HADI 1900BK)** kina wakilishwa na kanisa la Filadelfia.

   Kipindi hiki kilikua na uamsho ulipokuja na kujenga makanisa mbalimbali ulimwenguni ndio maana Yesu aliwasihi wakeshe wakisali na kuomba katika kipindi hiki makanisa yamekua yakienea sehemu tofauti tofauti ulimwenguni. Kipindi hiki ndicho makanisa mengi yalianzishwa na kuenea ulimwenguni Mf. KKKT, Anglikana, Morovian, Pentekoste Movement n.k

   *Ujumbe binafsi, Yesu ametoa mlango uliofungwa ili kuziendea rasilimali zisizo na mwisho yaani uzima wa milele pia mlango wa kuwaendea watu wengine.*

7. **KIPINDI CHA UVUGUVUGU WA KANISA (1900BK HADI hadi Yesu atakaporudi)** kina wakilishwa na kanisa la Loadikia.

   Kipindi hiki ndicho tulichonacho sasa kutokana na mazingira mazuri ya kiuchumi na ueneaji wa Injili ya kweli na mafundisho mengi ya uongo na kuongezaka kwa Imani tofauti tofauti na hali ya utajiri wa kimwili yaani majengo mazuri, miziki mikubwa na hii ni utajiri wa kimwili lakini kiroho tumeshuka sana na ni maskini wa kiroho kwa kupungukiwa na karama za kiroho Mf. Upendo, utu wema, uvumilivu, subira/staha n.k tunajiona ni matajiri kwa sababu ya vitu vya kidunia lakini Yesu analiao kanisa ni maskini na mambo ya kimungu analiita lilejee kwake ili lipate utajiri udumuo milele.

   Yesu aliyatabili haya na kutupa ushauri watu wa sasa tumrejee yeye ili tupate dhahabu safi na tuwe majiri safi wa kiroho kutokana na uvuguvugu imepelekea mashindano na kupotea kwa uhalisia wa nguvu za Mungu na kuligeuza kanisa kuwa sehemu ya burudani na kujipatia kipato.

   Pamoja na uvuguvugu wa kanisa lakini bado wapo waamini safi na wa kweli wanaompenda na kumwabudu mungu kwa roho na kweli, bado kanisa linashinda hali ya uvuguvugu na mafundisho ya uongo,tamaa, majivuno na Yesu bado anawapenda watu wake ili watubu ili washinde na kufika uzima wa milele. **(Ufu. 3:19-20)**

   ***Ujumbe binafsi, japokua tu vuguvugu na midhaa mingi lakini bado Mungu anaonyesha neema yake ya kutuita na kutubu ili tupate utajiri wa kweli udumuo (uzima wa milele) (Ufu.3:18-19).***

**N: B** tuwe macho na hiki kipindi cha mwisho tukeshe, kusali, kuomba na kusoma neno la Mungu ili tuweze kuufikia uzima wa milele/ufalme wa Mungu.

Pamoja na makanisa haya yaliwakilisha unabii wa vipindi vitakavyopitia kanisa lakini pia yanawakilisha hali ya kiroho ya kila mmoja wetu ndio maana msisitizo mkubwa Yesu anasema anayajua matendo yako hivyo tunaposoma makanisa haya saba jilinganishe na hali uliyonayo ya kiroho ya kwako binafsi na kukumbuka ya kuwa yesu anayajua matendo yako.hivyo chukua hatua kulingana Yesu alivyo shauri kulingana na hali uliyonayo.

- Kama upendo wako umepungua kama wa Efeso, ukumbuke ulipoanguka na kutubu na kurudia upendo wako wa kwanza
- Kama huko katika dhiki kwa sababu ya mambo ya Mungu kama smirna, Yesu anakuomba kuwa mwaminifu katika mateso hata kufa.

- Kama huko umejichanganya umekua mpagani umachanganya Imani na mambo ya mtaani kama pergamo basi tubu mrudie Mungu wako siku zimebakia chache sana.
- Kama umepotea kama thiatia umrudie Mungu wako maana atafanya vita na wewe kwa sababu ya matendo yako ya machafu ya giza.
- Na kama ulikua umekufa na unahitaji kuwa hai kiroho basi uwe mwenye kukesha ukayaimalishe mambo yaliyosalia na yanayolegalega na kutubu maana siku zimebaki chache kama alivyoambiwa sardi.
- Kama mlango wako wa mafanikio ya kiroho na huko wazi kama Filadelfia jitahidi kutunza Imani na matendo mema ili kuufikia uzima wa milele na kuwafikia wengine ili wamjue Mungu aliyekuwezesha (fanya kazi ya Injili na kutenda matendo mema na kudumu katika Imani ili mlango wako uendelee kuwa wazi ufanikiwe kiroho na kimwili)
- Kama vuguvugu kama loadikia tubu na uwe na msimamo maana utatapikwa, maana Yesu bado anakupenda **(Ufu. 3:19-21)**

# KITABU CHA KUTOKA

## PENTATUKI

- Tangu mwanzoni mwa Ukristo, na labda hata kabla ya wakati huo, vitabu vitano vya kwanza vya agano la kale vilijulikana kuwa pentatuki. Jina hili linatokana na maneno mawili ya kiyunani (kigiriki), yaani penta maana yake "tano" na teuchos maana yake “kitabu”. Waebrania walitaja pentatuki yote wakisema “sheria” au “torati”
  **(2Nya 17:9; Neh 8:14; Mt 5:17; 11:13; 12:5; Lk 24:44).** Mwazoni pentatuki ilikuwa kitabu kimoja, lakini kitabu kile kiligawanywa kiwe vitabu vitano kwa sababu ilikuwa rahisi kuvishika na kuvisoma. Majina ya vitabu vile katika tafsiri ya kale ya kiyunani ya Septuaginta yalikuwa Genesis kwa kitabu cha mwanzo, Exodus kwa kitabu cha kutoka, Leviticus kwa kitabu cha Walawi, Numeri kwa kitabu cha Hesabu na Deuteronomium kwa kitabu cha kumbukumbu la Torati.

## KITABU CHA KUTOKA KILIANDIKWA MWAKA.

## 1450 – 1410 K.K

- Kama ilivyokitabu cha mwanzo hata kitabu cha kutoka kilipewa jina lake la EXODOS la kiyunani lenye maana KUTOKA.

- Tukio la kutoka kwa wana Israeli katika utumwa wa Misri kwa kawaida linajulikana kuwa "kutoka" (au kilatini=Exodus). Matukio yale yalikuwa mwaka wa 1280K.K hivi, na maelezo ya historia yake yanapatikana katika kitabu cha kutoka ambacho ni kitabu cha pili katika Biblia.

## MWANDISHI

Mapokeo ya kiebrania ya kule pamoja na yale ya Kikristo yalimtambua Musa kuwa ndiye mwandishi wa Pentatuki, ingawa Pentatuki yenyewe haimtaji mwandishi wake **(2 Nya 35:12; Neh 13:1; Mk 12:26; Yn 5:46).** Sehemu mbalimbali Biblia inataja kazi ya uandishi wa Musa. Aliandika sheria ambayo Waisraeli waliipokea kutoka kwa Mungu **(Kut 17:14; Hes 33:2)** naye alitunga nyimbo na mashairi **(Ku 15:1; Kum 31:22-30).**

Musa ndiye mwandhishi wa kitabu hiki **(kutoka 17:14; 24:4; 34:28; hesabu 33:2; kumbu 3:9)** Musa aliyezaliwa misri yaani Afrika na kulelewa katika nyumba ya kifalme na baadae alikuwa kiongozi wa Taifa la Israeli.

Mnamo mwaka 1280K.K Musa alianza kuwaongoza wana wa Israeli akiwa na umri wa miaka 80 **(Kutoka 12:41; Matendo 7:23).**

## NIA NA MAKUSUDI.

Licha ya thamani yake ya kutoa ripoti za matukio ya historia ambayo maisha ya Israeli ya kidini naya kitaifa yalijengwa juu yake, kitabu cha kutoka kina thamani pia katika kudhihirisha sehemu kubwa ya tabia ya Mungu jinsi alivyo Mungu wa kuokoa, Mungu anayesikiliza ya wanadamu na Mungu mwenye kutimiza maagano.

Hivyo mtu asomapo kitabu cha mwanzo atagundua kuwa kuna Mungu aliye mwokozi awaokoaye wanadamu, aliye mwaminifu kwa ahadi zake pia ni mshika maagano.

Mungu alifanya kazi yake, akiwahifadhi watu wake kwa kadri ya ahadi yake ya agano **(Kutoka 15-22)**

1. Jina Waebrania lina asili mbili
   i. Katika mwanzo 10:21 sheu anatajwa kuwa baba wa wana wote wa Eberi aliyekuwa katika orodha ya wazazi wa Ibrahimu ambaye alikuwa mtu wa kwanza katika Biblia aliyeitwa mwebrania **(Mwa 14:13; Mwa 11;10-26; 1 Nya 1:24-27).**

   ii. Maana ya pili ya tafsiri ya neno hili ni "mgeni" au mtu wa ng'ambo. Ibrahimu alikuwa mgeni wa nga'ambo ya mto wa Frati **(Yosh 24:2-3).** Yusufu na ndugu zake huko Misri waliitwa Waebrania (**Mwa 39:15).** Baadaye waebrania walikuwa waisraeli safi tu, waliotofautishwa na makabila waisraeli sahihi tu, waliotofautishwa na makabila mengine **(Kut 1:15, 16, 19, 3:18; 5:3).**

## MGAWANYIKO WA KITABU CHA KUTOKA

Kitabu hiki cha kutoka kimegawanyika sehemu kuu mbili

i. Sehemu ya kwanza inaonyesha Mungu ni mwokozi **(Kutoka 1hadi sura ya 18)**

Katika sehemu hii Mungu anajionyesha kuwa yeye ni mwokozi mwenye kusikia kilio cha watu wake na akionyesha upendo mwingi kwa kuwaokoa watu wake na kumshinda adui kwa njia mapigo mbalimbali huku akitoa njia ya kuepuka adhabu yake kwa njia ya damu ya mwanakondoo ambalo ni tukio la kiimani nacho ni kipawa kitokacho kwa Mungu kama ilivyo sasa tunaokolewa kwa njia ya Imani kwa kumwamini mwanakondoo Yesu kristo.

ii. Kuundwa kwa Taifa la Israeli na kufunga agano rasmi (Ahadi za Agano la Mungu) (**kutoka (19 hadi sura 40).**

Na hii ni sehemu muhimu sana katika biblia inaonyesha jinsi Mungu alivyomwaminifu na mshika maagano na huu ni mwendelezo wa Agano alilomuahidi Ibrahimu na kupitia agano hilo mataifa yote yatabarikiwa **(Mwanzo 12:15-17)** na hapa Mungu anaahidi endapo Israeli itatii sheria na mafundisho yake watakuwa makuani wake na Taifa lililobarikiwa Duniani, lakini Israeli inashindwa kutii hivyo tunapata sababu kuu za Yesu kuja ili watu wote wahesabiwe makuhani kwa njia ya Yesu Kristo kwa maana Mungu yeye ndiye mwenye rehema si mwepesi wa hasira mwenye kusamehe uovu lakini hatomwesabia haki mtu mwovu **(Kutoka 34:6-7).**

***NB: WAKATI MUNGU ANAWACHAGUA ISRAELI KUWA TAIFA LAKE TEULE, MATAIFA MENGINE YALIONEKANA KUTENGWA NA MUNGU NA KUWA CHINI YA LAANA LAKINI ISRAELI NAO AWAKUZITUNZA SHERIA NA***

***AGANO NAO WAKAINGIA CHINI YA LAANA KWAIYO WOTE TUKAWA CHINI YA LAANA KWAIYO SIO ISRAELI SIO MATAIFA WOTE TUMETENDA DHAMBI NA TUMEPUNGUKIWA NA UTUKUFU WA MUNGU NA WOTE TUNAHITAJI REHEMA ZA MUNGU KUPITIA KUMWAMINI YESU KRISTO ILI TUPOKEE MSAHAMA WA DHAMBI (RUMI 3:23-26).***

PASAKA – KUTOKA 12:1-51

1. **Pasaka**
    - ❖ Dhabihu ilitakiwa iwe mwanakondoo
    - ❖ Ukombozi – Kristo mwanakondoo wa Mungu **(1 Korintho 5:7)**
2. **Pasaka**
    - ❖ Mwanakondoo asiwe na doa wala wa mstari wa 5 Ukombozi
    - ❖ Kristo bila doa wala mawaa **(1petro 1:8-19)**
3. **Pasaka**
    - ❖ Anapotelewa awe katika kilele cha maisha yake
    - ❖ Ukombozi – Kristo alipotolewa alikuwa katika kilele cha maisha yake
4. **Pasaka**
    - ❖ Damu ya wanakondoo ilimwagwa ili awe na uzima
    - Ukombozi – damu ya Yesu ili wote wawe na uzima **(Yuda 3:16, 1Petro 2:24)**
5. **Pasaka**
    - ❖ Haikutosha damu kumwagika tu bali kuiweka kwenye milango akitumia tawi la mhisopu au mti
    - ❖ Ukombozi – Haikutosha damu ya Yesu imwagike tu bali lazima kila mmoja atakayeamini aipake ndani ya moyo wake. **(Rumi 3:25, 10:9-10)**
6. **Pasaka**
    - ❖ Damu ilikuwa nje ya mlango ili kila mtu aione na ajue ni nani anayetegemea damu hiyo mstari wa 7
    - ❖ Ukombozi – ni lazima Kristo ashuhudiwe wazi kwa watu na hao wanaomwamini. **(Mathayo 10:32-33)**
7. **Pasaka**
    - ❖ Hakuna usalama isipokuwa nyuma ya hiyo milango yenye damu mstari wa 22
    - ❖ Hakuna usalama isipokuwa nyuma ya damu ya Yesu **(Marko 16:16)**
8. **Pasaka**
    - ❖ Kutengwa kutoka chachu (ambayo ni mfano wa dhambi) mstari 8
    - ❖ Ukombozi – ni lazima tutengane na dhambi zote hata zile ndogo **(Yohana 3:19-10)**

9. **Pasaka**
    - Ni lazima kuwa katika hali ya usafiri viuno vilikuwa vimefungwa, viatu miguuni, fimbo mkononi. Mstari 11
    - Ukombozi katika hali ya usafiri hapa duniani **(1Petro 2:11, Ebrania 11:13)**

# ZABURI

## (SIFA KUPITIA MAOMBI)

Kitabu cha zaburi

Zaburi ni kitabu kipana na kirefu kilichobeba sala, maombi na sifa kupitia uimbaji na kinachogusa hisia na roho za watu wengi hasa waaminio. Na chenye utabiri mwingi kuhusu masihi Yesu Kristo.

Zaburi ni kitabu cha mashairi yaliyotungwa kwa uvuvio wa roho mtakatifu pia ni kitabu chenye sura nyingi kuliko vitabu vyote vya bibilia yani kurasa 150.

Sura ndefu kuliko zote inapatikana kwenye zaburi yaani zaburi 119 yenye mistari 176 pia sura fupi katika bibilia inapatikana katika zaburi yaani zaburi 117 yenye mistari 2.

Zaburi ni kitabu kilicho andikwa na waandishi wengi Kuliko vitabu vingine vyote hii inawaandishi Zaidi ya 6 na wengine hawajulikani ikumbukwe kuwa kila zaburi inajitegemea haina uhusiano na nyingine na kila zaburi iliandikwa kwa muda tofauti na nyingine. Hivyo kitabu cha Zaburi hakina sura 150 bali kina zaburi 150, haziitwi sura kwa sababu kila zaburi inajitegemea yenye yaani haina mwendelezo pia ikumbukwe mfalme Daudi ndiye aliyezikusanya na kuzitunza baadaye Ezra.

Pia ni kitabu kinachoaminiwa na watu wengi Wakristo, waislamu na Wayaudi mara nyingi kimetumika kufariji, kuonya na kufundisha. **(Kolosai 3:16), (Efeso 5:18-20)** na pia ni kitabu cha nyimbo za ushairi.

Katika lugha ya kiebrania kitabu cha Zaburi kunajulikana kama kitabu cha sifa na Zaburi 145 inathibisha hili Zaburi ni mashairi yaliyoimbwa kwa kutumia vyombo vya muziki. Neno Zaburi linatokana na kiebrania lenye maana ya piga chombo chenye nyuzi kwa ajili ya kuimba.

### MWANDISHI WA KITABU CHA ZABURI.

Watu wengi uzani kuwa zaburi hizi ziliandikwa na Daudi pekee ukweli ni kwamba kuna waandishi wengi wa Zaburi

| **Mwandishi wa zaburi** | **Idadi ya zaburi alizoandika** | **Baadhi ya sura za vitabu hivyo** |
|---|---|---|
| Daudi | 73 | Kitabu cha 1.2.18. kitabu cha 3. Kitabu cha 4,2; kitabu cha 5,15 |
| Asaph | 12 | Zaburi 50,73-83 |
| Korahites | 12 | 42-49,84,6,87,88 |
| Solomon | 2 | Zaburi 72,127 |
| Musa | 1 | Zaburi 90 |
| Ethan | 1 | Zaburi 89 |
| Waandishi Wasio Julikana Kwa Majina Yao | 50 | |

Zaburi zingine zina maneno ya vichwa yanayotoa majina ya watunzi au majina ya watu ambao kutoka mkusanyika wao zaburi fulani imetolewa (k.mf. zab 41 na 42. Kwa baati mbaya katika tafsiri ya kiswahili majina yale na vichwa havikuandikwa).

Daudi ametajwa kuwa mtunzi wa zaburi 73, yaani karibu nusu ya mkusanyiko wote. Alikuwa na kipawa cha muziki na utunzi **(1 Samwel 16:23; 2 Samwel 23:1),** naye aliweka vikundi mbalimbali vya waimbaji na wacheza muziki kwa ajili ya ibada za hekaluni **(1 Nyakati 15:16-28; 16:7, 37-42).**

Daudi alipanga waimbaji na wachezaji vyombo katika makundi matatu chini ya uongozi wa watu watatu waliotoka katika koo tatu za kabila la Lawi, yaani Asafu, Hemani na Ethani (au Yeduthuni) **(1 Nya 6:31-48; 15:17-19),** nao pia walitunga baadhi ya Zaburi zilizoingizwa katika kitabu cha Zaburi **(k.mf. Zab 50, 73-78, 88-89).** Kitabu pia kina Zaburi mbili za Suleimani **(Zab 72 na 127)** na moja ya Musa **(Zab 90).**

**MUDA WA KUANDIKWA.**

Kwa kuangalia Zaburi ya 90 kinaweza kuwa cha kwanza kilichoandikwa na Musa kati ya 1405 K.K Zaburi za Daudi zinaweza kuwa zimeandikwa kati ya 1020 na 975 K.K na zile Zaburi za Asaph nazo zaweza kuwa kwenye kipindi hicho.

Zaburi imekuwepo tangu kipindi cha utawala wa Suleimani kati ya 950 K.K. ni vigumu kujua ukoo wa Koran na hata wale wawili akina Ezra waliotajwa labda walikuwepo kabla ya uhamishoni lakini Zaburi haijawaeleza. Labda wamekuwepo lakini kati ya miaka 500 K.K.

MGAWANYIKO WA ZABURI.

Zaburi ni vitabu vitano katika kitabu kimoja. Kila kitabu kina sifa za Mungu na ile Zaburi ya 150 ina sifa za Mungu na ina hitimisha Zaburi zote.

Wasomi walisema, "waebrania waligawa zaburi katika sehemu tano ili iwe ***Pentateuch (vitabu vitano alivyoandika Musa yaani Mwanzo,Kutoka,Lawi,Torati na Hesabu)*** nyingine zaburi 1:1 inasema Musa akawapatia Waisraeli vitabu vitano vya Sheria na kwa kuangalia hapa Daudi naye akawapatia kitabu chenye vitano vitano".

ORODHA YA MAANDIKO HAYA IKO KAMA IFUATAVYO:-

1. Zaburi juu ya uumbaji na mwanadamu (Zaburi 1hadi zaburi ya 41) hii ina shabihiana na mwanzo.
   ***Mwisho wa kitabu hiki ni (Zab. 41-13)***

2. Zaburi juu ya Waisraeli na kukombolewa (zaburi ya 42 hadi zaburi ya 72) hii inafanana na kutoka.
   ***Mwisho wa kitabu hiki ni (Zab. 72-18-19)***

3. Zaburi inayohusu ibada na hekalu (zaburi ya 73 hadi zaburi ya 89) hii ina fanana na Walawi.
   ***Mwisho wa kitabu hiki ni (Zab. 89-52)***

4. Zaburi juu ya Dunia (zaburi ya 90 hadi zaburi ya 106) hii inafanana na Hesabu
   ***Mwisho wa kitabu hiki ni (Zab. 146-48)***

5. Zaburi inayohusu sifa na neno la Mungu (zaburi ya 107hadi zaburi ya 150) hii inahusu kumbukumbu la Torati.
   ***Mwisho wa kitabu hiki ni (Zab. 150)***

- *Mstari wa mwisho wa kila kitabu kilichowekewa kivuli hapo juu ulikua unatenganisha kati ya kitabu kimoja na kingine lakini maajabu vilikuwa vinafanana wakati huo viliandikwa na watu tofauti na wakati tofauti.*

NJIA NYINGINE YA KUTAZAMA MGAWANYO WA VITABU HIVI.

| kitabu | Zaburi | Mwandishi | Yaliyomo |
|---|---|---|---|
| i | Zaburi 1-41 | Daudi | Nyimbo za Kuabudu |
| ii | Zaburi 42-72 | Daudi na kora | Nyimbo za Kutukuza |
| iii | Zaburi 73-89 | Asaph | Nyimbo za Kutukuza |
| iv | Zaburi 90-106 | Wasiojulikana | Nyimbo za Kutukuza |
| v | Zaburi 107-150 | Daudi na wasiojulikana | Nyimbo za Kusifu |

Jinsi zaburi ilivyotabiri habari za yesu kristo. **(Luka 24:44-48); (Luka 24:26-31)**, Yesu mwenyewe alieleza habari za kufa na kufufuka kwake na ondoleo la dhambi na kuhesabiwa haki kwa kila amwaminiye yeye alisema zilitabiliwa kwenye Zaburi.

**Zifuatazo ni baadhi za tabiri na nukuu kutoka katika Zaburi zilizotimia kwenye maisha ya Yesu na Agano jipya.**

| Na. | Jinsi ya zaburi ilivyotabiri | Utimilifu wa zaburi katika maisha ya Yesu |
|---|---|---|
| 1 | Kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo **(Zab. 16:8-11)** | Matendo ya Mitume 2:22-34 |
| 2 | Mateso ya Yesu msalanbani**(Zab 22:1-7)** | Marko 15:34; Mathayo 26:28-29; Luka 32:21-23 |
| 3 | Ubora na thamani ya sadaka ya kifo cha Yesu msalabani, kukubaliaka mbele za Mungu kuliko sadaka yoyote ya agano la kale. **(Zab. 40:4-9)** | Ebrania 10:1-18 |
| 4 | Kupaa kwa Yesu Kristo na kuwapa karama za huduma. **(Zab. 68:16-20)** | Efeso 4:7-12 |
| 5 | Kutwaa mwili na kufanyika mwanadamu ili afanane na wanadamu alipe fidia ya dhambi za wanadamu na kufanyika mmiliki wa vyote. (Zab. 8:3-9) | Ebrania 2:5-10 |
| 6 | Uungu na umilele wa Yesu Kristo. (**Zab. 102:25-27)** | Ebrania 1:8-12; Yohana 1:1-3; |
| 7 | Kukataliwa kwake na waashi (yaani wakuu wa dini) mafarisayo na masadukayo wajenzi wa nyumba ya Mungu yaani mwamini. **(Zab. 118:21-22)** | 1 Petro 2:5-7; Mathayo 21:42; Marko 20:17; Matendo ya Mitume 4:11 |
| 8 | Kufanyika mfalme na mwana wa Mungu Atakayetawala milele.**(Zab 2:6-7)** | Yohana 12:12-13; Ebrania 1:5-6; Mathayo 3:16-17; Rumi 1:1-4; Luka 1:31-35 |

| | | |
|---|---|---|
| | Ufalme wa daudi ulivyotabiliwa utakavyofanana na ufalme wa Yesu Kristo ulio wa milele na wa haki na mfano wa mzaliwa wa kwanza wa Mungu.<br>**(Zab. 89:20-28)** | Kolosai 1:18-20; Ufunuo 1:5; Mathayo 11:27 |

## NINI WANDISHI WA ZABURI WALIKUSUDIA KUANDIKA WALICHOANDIKA KUPITIA UVUVIO WA ROHO MTAKATIFU?

Kama ambavyo maelezo yanavyoyaeleza hapo juu, kuwa sehemu kubwa ya zaburi ni utabiri wa masihi na habari ya wokovu wake ambao unapatikana Kwa njia ya kuamini injili ya huyo masihi, (Rum 1:1-3),

Ni dhahiri malengo makuu ya Waandishi katika ilikuwa ni kuitangaza injili ya Mungu yaani watu wamuone kristo katika usomaji wao kama ndiye masihi ajaye Kwa ajili ya kuwakomboa

Ushahidi unaonesha kuwa hata Daudi mwenyewe alimuona kristo ingawa alikuwa akiishi bado katika agano la kale, lakini kutokana na kitabu cha 1Petro 1:4-12, unaonesha kama manabii katika agano la kale waliandaka Kwa Habari za masihi japo lugha yao haikuwa wazi Bali Kwa mifano na mafumbo **( *1 Petro 1:8-12)***

Hata hivyo Kuna baadhi ya maandiko ambayo nimeyaorodhesha hapo juu katika jedwali la mwisho, yanaonesha baadhi ya maandiko machache kutoka kwenye zaburi yanavyomuonesha masihi lakini sio waziwazi, japo mitume wa kristo waliofundishwa usomaji mzuri au kanuni sahihi za usomaji na kristo mwenyewe siku orobini kabla ya kupaa kwake **( *Luka 24:44-45)*** wametutafsiria baadhi ya hayo maandiko yalivyo maanisha Kwa namna yanavyomtabiri kristo kama masihi kama tumevyoainisha kwenye jedwali hilo.

Kama ambavyo tumeona Daudi ndio amebeba karibia nusu ya kitabu cha zaburi, ukisoma Kwa umakini utagundua Daudi alikua grammatically sehemu ya masihi, yaani katika ya uandishi sehemu nyingi Daudi imejiweka yeye kiwakilishi cha masihi, hilo tunaliona kwenye baadhi ya maandiko mfano;

**Zaburi 16:9-10**

[ 9]Kwa hiyo moyo wangu unafurahi, Nao utukufu wangu unashangilia, Naam, mwili wangu nao utakaa kwa kutumaini._

[10]Maana hutakuachia kuzimu nafsi yangu, Wala hutamtoa mtakatifu wako aone uharibifu_ .

Kama ukisoma vizuri unaona kama Daudi anazungumza kuhusu kufa kwake na kuzikwa kwake kuwa Mungu hataiacha nafsi iharibike. Lakini ukija kuona maana ya huo mstari katika katika kitabu cha matendo ya mitume Kwa ufafanuzi wa mitume

**Matendo ya mitume 2:25-31**

[25] Maana Daudi ataja habari zake, Nalimwona Bwana mbele yangu siku zote, Kwa kuwa yuko upande wa mkono wangu wa kuume, nisitikisike.

[26]Kwa hiyo moyo wangu ukapendezewa, ulimi wangu ukafurahi; Tena mwili wangu nao utakaa katika matumaini.

[27] Kwa maana hutaiacha roho yangu katika kuzimu; Wala hutamtoa Mtakatifu wako aone uharibifu.

[28] Umenijurisha njia za uzima; Utanijaza furaha kwa uso wako.

[29]Waume, ndugu zangu, mniwie radhi, niseme kwa ujasiri mbele yenu habari za baba yetu mkuu, Daudi, ya kuwa alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo.

[30]Basi kwa kuwa ni nabii, akijua ya kuwa Mungu amemwapia kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa viuno vyake atamketisha mmoja katika kiti chake cha enzi;

[31]yeye mwenyewe akitangulia kuyaona haya, alitaja habari za kufufuka kwake Kristo, ya kwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuona uharibifu.

Kumbe kwenye zaburi 16, Daudi alikuwa kama mwakilishi wa masihi yaani alikaa grammer, ya muigizaji Kwa maneno mengine akijiongelea kama mwakilishi wa kristo. Maana hata Leo kaburi lipo na hajafufuka na nafsi yake Wala mwili haujafufuka..

Nimalizie hivi licha ya kumtumia Daudi sana Kwa kuhitimisha haya maelezo ya uchambuzi wa kitabu za zaburi Kwa uchache, waandishi wengine pia walikuwa na lengo hilo hilo kuwa wanaongelea Kwa Habari za wokovu KUPITIA masihi Kwa maana ya ukilingana na kitabu cha **(Luka 24:44-45 , na Luka 24: 26-27**), Hivyo lengo la kitabu cha Zaburi ni kitabu kinachoelezea kuzaliwa , kuteswa , kufa na kufufuka Kwa kristo yaani katika zaburi upo ujumbe wa kiroho ambao ni injili kamili ambapo asomaye anahitajika kuona hivyo..

Tuhitimishe Kwa kusema biblia ni kitabu kimechobeba ujumbe mmoja ambaye ni masihi yesu kristo na ndio kitu mhimu Kwa asomaje na kuelewa vzuri, yeyote

aaminiye atapokea  uzima wa milele ambao Mungu alituahidia kuanzia mwanzo Hadi ufunuo.

**NB: Luka 24:44-45, na Luka 24: 26-27**.

Kama maandiko na Zaburi isemavyo Yesu Kristo ni bwana na mwokozi wa maisha ya wanadamu wote ili kila amwaminiye apate msamaha wa dhambi na uzima wa milele katika yeye. Hivyo na mimi  mwalimu Anil Michael naamini kwa kusoma Zaburi utampenda Mungu na kumwamini Yesu Kristo.

# ISAYA

## UTANGULIZI NA UCHAMBUZI WA KITABU CHA ISAYA

### MTUNZI NA JINA LA KITABU.

Kama kitabu kinavyojieleza mwandishi ni Isaya mwana wa Amozi **(Isaya 1:1),** kiongozi wakati wa Ahazi.

Isaya alikuwa mwana wa mtu aitwaye Amozi Biblia haijaeleza kuhusu Amozi baba yake Isaya alikuwa mtu wa namna gani lakini jina Isaya maana yake ni **BWANA NI WOKOVU** Isaya alianza kuona maono ya Mungu baada ya kifo cha mfalme Uzia **(Isaya 6:1).**

Ilikuwa mapema kabla ya wakati wa Daniel, Ezekiel, Yona. Biblia haijataja sana undani wa

Isaya lakini maandiko yanaonyesha kuwa Isaya alioa mke nabii na akazaa nae watoto **(Isaya 8:3)** mwanamke huyo alimuoa kwa agizo la Mungu kwa sababu Mungu alifanya maisha yake kama ishara au kitu cha kujifunza kama vile Osea na Ezekiel.

Alikua ni mtu msomi wa mambo ya kimataifa aliyetumia muda wake katika mji wa Yerusalemu ambako alikutana na Wafalme na akawashauri juu ya mambo ya uhusiano wa kimataifa.

Ingawa Isaya alikuwa msomi na mshauri wa mambo ya mahakama na ushirikiano wa kimataifa alishauri sana wafalme kumtumainia Mungu kuliko kutegemea mataifa yenye nguvu mara nyingi wafalme waligoma na kumchukia lakini Isaya aliendelea kushauri na kuhubiri kwa vitendo hata ilimlazimu kutembea Uchi bila mavazi **(Isaya1-6)** ilikuonya. Wafalme wamtegemee Mungu kuliko mataifa yenye nguvu **(Isaya 26:3-4).**

Isaya ni nabii pekee wa agano la kale aliye tabiri habari za kuja kwa Yesu Kristo kuliko manabii wote wa agano la kale, hivyo Isaya ni nabii mwinjilisti akitumia neno wokovu mara nyingi zaidi ya 20 kusisitiza nia ya Mungu kutaka kuwaokoa watu wote.

Desturi za kale zinaeleza kwamba aliuawa wakati wa utawala wa Manase kwa njia ya kukatwa msumeno **(Waebrania 11:37).** kwa sababu kuwa alisema na kutabiri kifo cha Sennacherib mfalme wa Ashura katika **(Isaya 37:14-38).** Hivyo aliamuliwa achinjwe kwa msumeno ni mbali sana kufikiri kwamba Isaya aliishi hadi baada ya kifo cha Sennacherib miaka ya 31 K.K.

## MUDA WA KUANDIKWA.

## 740-680 K.K

Isaya alikuwa na huduma ndefu sana iliyoanza **740 hadi 680 K.K.** Huduma yake ilianza mapema kabisa mwishoni mwa utawala wa **Uzia (790-789 K.K)** na ikaendelea hadi utawala wa **Yotham (739-731 K.K). Ahazi (731-715 K.K)** na **Hezekia (716-686 K.K).** Tangu kusimama kwa wakuu wa watakatifu Isaya alitumika tangu nyakati za **Tiglath-pileser (745-727 K.K)** hadi nyakati za **Sennacherib (705-681 K.K)** wa Asiria. Inaonekana Isaya alifanya huduma kwa miaka 50.

Pia Isaya hakutabiri kuhusu Israeli peke yake bali alitabiri nchi 11 ikiwemo **Kush, Misri, Yuda, Ashuru, Babeli, Syria, Moabu n.k.**

## NIA NA MAKUSUDI.

**All people are called to repents of sin and trust in God alone (12:2, 26; 3-4, 50:10)**

Isaya alitoa kusudi la kitabu "Wokovu ni wa Yahwe" Na hii ni dhahiri kwa ukweli kwamba neno "wokovu" linaonekana mara Ishirini na sita zaidi ya manabii wengine waliojumuishwa kwa sababu hii Isaya amekua akiitwa "Nabii Mwinjilisti" kwa sababu anasema mara nyingi sana kuhusu wokovu na kazi ya wokovu ya Masihi. Kwa kweli mengi yamesemwa katika kitabu hiki juu ya utu na kazi ya Masihi zaidi ya vitabu vyote katika Agano la kale.

Kwa mtazamo mwingine Isaya ni kitabu kikubwa maana kina sura sitini na sita , sura thelathini na tisa za kwanza zinashabihiana na vitabu vingine vya Agano la kale zinazozungumzia kuja kwa Mashihi na sura Ishirini na saba za mwisho zinashabihiana na vitabu Ishirini na saba vya Agano jipya kwa sababu

zinazungumzia juu ya Masihi na mpango wake na ufalme wake kama mtumishi wa Mungu kwa sababu zinazungumzia juu ya Masihi na mpango wake na ufalme wake kama mtumishi wa Mungu sura 1-39 zinazungumzia hitaji la mwanadamu juu ya wokovu na 40-65 zinaonyesha wokovu wa Mungu katika Masihi na ufalme wake.

Lengo kuu la kitabu cha Isaya watu na mataifa waache maovu na kutegemea msaada na nguvu za giza na za kibinadamu bali wamtegemee Mungu kama muumbaji na mtoa uzima **(Isaya 42:5)** pia ni Mungu anayewapenda na amejaa rehema na msamaha.

## MGAWANYIKO WA KITABU CHA ISAYA.

Isaya ni kitabu kipana sana kinaitwa biblia ndogo kwa sababu kinafanana na kubeba ujumbe mzima wa biblia, hivyo unaweza kukigawa mara mbili.

### 1. SURA 1 HADI 39; HII NI AGANO LA KALE.

Kwa sababu ujumbe uliopo hapa unafanana na vitabu vingine unaowaita watu kutubu ili kuepuka hukumu ya adhabu itakayo wapata na hasara ya kumuacha Mungu na kutegemea Miungu mingine.

### 2. SURA 40 HADI 66; HILO NI AGANO JIPYA

Kwa sababu katika sura hizi zimebeba ujumbe wa wokovu na ujio wa Masihi Yesu Kristo kama njia ya wokovu wa wanadamu wote na kuleta habari njema za kutia moyo.

## AINA NYINGINE YA MGAWANYIKO WA KITABU CHA ISAYA

**Sura ya 1 hadi ya 40**

Wito na ushauli kwa wafalme wa Yuda na mataifa pamoja na mimi na wewe kumtegemea Mungu tu na si vinginevyo hata kama kunahatari kiasi gani lakini mwanzo ushauli huu wengi waliukataa hata Mungu alimuamuru Isaya kutembea uchi **(Isaya 20:1-6)** mwaka mzima kusisitiza watu wamtegemee Mungu na si mataifa yenye nguvu pamoja na adhabu Mungu anaahidi kutaka kuwasamehe na kuwahurumia **(Isaya 10:2023)** na kubakiza masalia katika hayo masalia atamleta masihi.

**Sura ya 40 hadi 45**

faraja na kutia moyo sehemu hii pia ninaonesha wema na upendo wa Mungu kwa wanadamu inaonesha utabiri wa wazi wazi ujio wa Yesu Kristo kama

Masihi wa ukombozi atakae kuja kuteswa, kufa na kufufuka kwa ajili ya dhambi zao kama njia ya Mungu kuondoa uovu na zambi zao ili wapate kibari mbele za Mungu kwa haki ya Mungu si kwa matendo na kutokutii kwao lakini wanaokolewa kwa neema ya Mungu na kwa sadaka ya Mungu wanahesabiwa haki bure na Mungu wamekuwa watoto wa Mungu kwa njia yake Mungu kupitia kufa na kufufuka kwake Yesu Kristo mfano **sura 42,49,50,53** n.k, zinaonesha kwa uwazi na upana kazi ya Masihi wa Mungu.

**Sura 56 hadi 66**

Sura hizi zinadili na kuwakaribisha na kuwaita watu wa mataifa kumuabudu Mungu na kumtafuta Mungu maadamu anapatikana na mtu mbaya na aache njia zake mbaya na mtu yeyote asiye tenda haki abadilishe mawazo yake (atubu) na kumrudia Bwana na Mungu atamlehemu na amkumbuke muumba wake na Mungu atamsamehe **(Isaya 55:68)** Yesu alisema mambo yote aliyofanya na yaliyompata yalitabiliwa na manabii na Musa **(Luka 24:25-27).**

Kwa ufupi tuone jinsi kitabu cha Isaya kilivyo tabiri habari za Yesu Kristo mwokozi wetu ikumbukwe kitabu cha Isaya kiliandikwa miaka 760 kabla ya kuzaliwa kwa Yesu.

**UTABIRI WA YESU KRISTO KATIKA KITABU CHA ISAYA UTIMILIFU WAKE KATIKA AGANO JIPYA**

| AHADI NA UTABIRI WA YESU KRISTO KATIKA KITABU CHA ISAYA | UTIMILIFU KATIKA AGANO JIPYA |
|---|---|
| Kuzaliwa kwa Yesu Isaya alitoa unabii kuwa **(Isaya 7:14)** | **(Mathayo 1:22; Luka 1:31-35)** |
| Atazaliwa kutoka katika ukoo wa Daudi **(Isaya 11:1-3; Isaya 9;6-7)** | **(Matendo ya Mitume 13:16-21; Luka 7:22; Mathayo 11:22)** |
| Yeye ni mwenye mamlaka na nguvu na mwokozi **(Isaya 9:6-8)** | **(Luka 22:11; Yohana 3:16; mathayo 28:18)** |
| Mtangulizi wake Yohana mbatizaji **(Isaya 40:3-4)** | **(Mathayo 3:1-3)** |

| | |
|---|---|
| Huduna yake ya wokovu kwa masikini na wafungwa nao walielewa watapata haki na kuitangaza haki ya Mungu<br>**(Isaya 61:1-4; Isaya 42:1-4; Isaya 60:1-6)** | **(Luka 4:16-21; luka 7:22; Mathayo 11:22)** |
| Ataleta wokovu kwa watu wote kwa njia ya amnai (Isaya<br>57:11-13) | **(Warumi 3:16; Tito 3:4-5)** |
| Uwezo na nguvu za Yesu katika kushinda maadui **(Isaya**<br>**49:24-26)** | **(Mathayo 12:28-29; Luka 11:20-22)** |
| Kujitoa kwa watu kwa ajili ya zambi zetu na kuwafidia zambi zetu na makosa yetu sote **(Isaya 53:1-11)** | **(Mathayo 8:16-17, 1Pero 2:24)** |

# MATHAYO

**Mwandishi (*Author*)**

Inasadikika kuwa Mathayo ambaye alikuwa ni miongoni mwa wanafunzi wa Yesu ndiye aliyeandika kitabu hiki. Mathayo huyu alikuwa mtoza ushuru huko Palestina kwa Warumi hadi pale alipoitwa na Bwana kumfuata, mwanzoni aliitwa Lawi wa Alfayo (*Math 9:9-13, Marko 2:14-15*).

*NB; Kwa kusema kabisa Injili hizi Nne (Mathayo, Marko, Luka na Yohana) hazieleweki waandishi wake maana hakuna jina lililoandikwa kwa kila kitabu kuonyesha kuwa ni nani aliyeandika. Hii hata hivyo, haishangazi kwa sababu <u>Injili</u> hutofautiana na <u>Nyaraka (Barua)</u>. Barua za Paulo zinaanza na jina lake ambacho ni kitu cha kawaida kwa barua katika Ulimwengu. Hakuna mwandishi wa Injili aliyejitaja jina lake moja kwa moja, lakini kadri unavyoenedelea kusoma utakuta mwandishi amejulikana katika kitabu chake alivyo andika na wanajulikana sana kulingana na desturi. Kujulikana kwa waandishi wa Injili kuna endana na ushahidi wa ndani na nje wa mwandishi.*

Je, ni sababu zipi zinatufanya au zilifanya wana historia waka amini kuwa aliye andika kitabu hiki ni Mathayo ambaye alikuwa ni mwanafunzi wa Yesu na siyo Mathayo mwingine maana majina yanaweza kufanana?

- Mwandishi anaonekana ni mtu anayejua vizuri historia na utamaduni wa Wayahudi, maana Wayahudi walikuwa wanategemea kuja kwa Masihi.
- Mwandishi anaonekana alilelewa katika familia ya kikuhani (Walawi), maana ameandika juu ya historia ya ukoo wa Yesu mwana wa Daudi (*Math :1-17*)

**Tarehe na Mahali (*Date and Location*)**

Tarehe kamili ya kuandikwa kwa kitabu hiki haijulikani, lakini ina kisiwa kuwa Injili hii iliandikwa kati ya mwaka 50BK na 70BK. Hii ni kutokana na sababu kuu zifuatazo;

- Inakadiriwa inaweza kuwa iliandikwa baada ya mtawanyiko wa wanafunzi pale Yerusalemu (*Matendo 8:4*). Hii ni kwasababu kabla ya wakati huo, kanisa la kwanza halikuwa hitaji wa maandishi yoyote ya Injili maana mitume wengi walikuwepo kutoa mafundisho na maelekezo ya muhimu kwa kanisa, mfano mitume walikusanyika Yerusalemu ili kutoa tamko juu ya namna wamataifa washiriki katika wokovu bila kushika sheria yote ya Musa kama kutahiriwa nk. (*Matendo 15:6-11*).
- Pia inakadiriwa kuandikwa kabla ya mwaka 70BK kwasababu unabii wa kubomolewa kwa mji wa Yerusalemu ambao ulitolewa na Bwana Yesu (*Math 24:1-28*) hauonekani au hakuna maelezo ya kutimia kwake katika kitabu cha Mathayo.

Mahali ambapo Injili hii iliandikwa ina sadikika ni maeneo ya Uyahudi (Palestina)

**Makusudi (*Themes*)**

Mathayo aliwaandikia Wayahudi kuwaonesha kuwa ***Yesu Kristo ni "Mfalme wa Wayahudi"***
***(Masihi)***.

Kutokana na mkanganyiko uliokuwepo kwa Wayahudi, na kama ushahidi wa swali alilouliza Yesu Kristo kwa wanafunzi wake katika **Sura ya 16:13-15**, Mathayo aliwaandikia kuwajibu maswali yao juu ya Yesu Mnazarethi. Yesu Kristo alikuwa amewaeleza kwamba yeye ni Masihi wao. Je, alikuwa ni Masihi aliye elezwa katika Agano la Kale aliyetabiriwa na Manabii? Kama ni hivyo kwa nini Walimu wa dini walishindwa kumpokea? Na kwanini aliweka Ufalme ulioahidiwa? Je utakuwepo

kweli na kama utakuwepo ni lini? Kwa hiyo Mathayo akawa anawaandikia kuwajulisha kuwa Masihi ni huyu ambaye amekuwa akisubiriwa.

Mathayo katumia ushahidi ufuatao kuthibitisha kuwa Yesu Kristo ni Mfalme wa Wayahudi na Masihi aliyetabiriwa na kusubiriwa na Wayahaudi na kwa ulimwengu;

1. Ukoo wa Yesu Kristo (Math 1:1-17) (*The Genealogy Of Jesus Christ)*

Mathayo ameifungua Injili yake na hivi vizazi, ambavyo vinafuatilia uzao wa mababu wa Yesu kupitia upande wa baba yake (upande wa Yusufu mumewe Mariamu aliye mzaa Yesu), kama ilivyo desturi ya Kiyahudi **Ms 16.** Ingawa Yusufu **hakuwa baba mzazi wa Yesu** (*Math 1:20*), alikuwa **baba yake kisheria (halali)**.

Kwakuwa Mungu aliahidi kuwa Masihi atakuwa wa uzao wa Ibrahimu (*Mwa 12:3; 22:18; Gal 3:16*) na Daudi ( *2Sam 7:12-19; Yer 23:5*), Mathayo anafuatilia uzao halali wa Yesu mpaka kwa watu hawa wawili ili kuweza kuwaonesha Wayahudi kuwa Yesu alikuwa wa uzao unaostahili kuweza kuwa Masihi.

Neno "Kristo" (Gk *Christos*) maana yake "mpakwa mafuta"; ni sawa na neno la Kiebrania

"Masihi" (*Dan 9:25-26*)

a) Tangu mwanzo Mathayo anathibitisha kuwa Yesu ni Mpakwa Mafuta wa Mungu.

Aliyepakwa mafuta na Roho Mtakatifu (*Isa 61:1; Lk 4:18; Yn 3:34; Mdo 10:38*)

b) Alipakwa mafuta **kama nabii** kuleta maarifa na kweli (*Kum 18:15*) **kama kuhani** ili kutoa dhabihu na kufuta hatia (*Zab 110:4; Ebr 10:10-14*), na **kama mfalme** kutawala, kuongoza na kuthibitisha ufalme wa haki (*Zak 9:9*).

2. Kutembelewa na Mamajusi wa Mashariki (Mt 2:1-12) (*The Visit of the Wise Men)*

Watu hawa huwenda walikuwa katika tabaka la watu wa dini waliosoma kutoka katika eneo ambalo ni Iran ya sasa. Walibobea katika unajimu, udaktari na sayansi ya asili (*astrology, dream interpretation, study of sacred writings, the pursuit of wisdom, and magic*). Ujio wao ulitokea wakati Yesu akiwa kati ya siku 40 (*Luk 2:22*) na miaka miwili hivi (*Mt 2:16*). Watu hawa inaonekana walikuwa na utamaduni wa kuwasujudu wafalme, kwa wao

haikuwa tatizo kusujudu kwa Yesu japo alikuwa katika hali ya utoto mchanga, na walifanya hivyo bila kufahamu uungu na ukuu na ufalme wa Yesu (*Mt 2:11*). Umuhimu wa habari hii ni kwamba

a) Yesu anastahili heshima ya kifalme kwa wanadamu wote, na

b) Mataifa na Wayahudi wote wamehusishwa katika katika mpango wa Mungu wa ukombozi (*Mt 8:11; 28:19, Rum 10:12*)

3. Kuingia Kwake Yerusalemu kwa Shangwe (Mt 21:4-11) (*The Triumphal Entry)*

Yerusalemu ni kiini cha maisha ya dini ya Israel, ni mji mashuhuli ambao Bwana aliuchagua na mji uliobeba historia kubwa kwa Israel lakini kwaajili ya ukombozi wa ulimwengu kwa njia ya Yesu Kristo. Kitendo cha Yesu kuingia mji huu akiwa juu ya Punda na kutandikiwa nguo na majani chini huku akishangiliwa kulionesha hali ya Ufalme aliokuwa nao Yesu (*Mt 21:7-8, Yh 12:13)* kwa hali hiyo ni ukiri kuwa Yesu ni Mfalme (*2Fal 9:13).* Mathayo katumia rejea ya maandiko ya manabii (*Isaya na Zekaria*) walio tabiri juu ya Yesu kuingia mji kama Mfalme (*Zek 9:9, Isa 62:11).*

4. Hukumu ya Mataifa (Mt 25:31-46) (*The Final Judgment)*

Mathayo karejea katika mafundisho yake Yesu vile alivyowaeleza kwa habari ya hukumu ya mwisho juu ya wanadamu wote (mataifa yote) kuwa yeye kama <u>Mfalme</u> ataketi kitini pake kwaajili ya kutoa hukumu juu ya mataifa yote (*Mt 25:31-46).*

5. Ukiri wa Yesu mbele ya Pilato (Mt 27:11) (*Jesus Before Pilate)*

Yesu baada ya kukamatwa na kufikishwa kwa Pilato aliulizwa swali "<u>Wewe ndiwe mfalme</u> <u>wa Wayahudi?</u>" na jibu la Yesu lilikuwa "<u>Wewe wasema</u>" kwa tafsiri rahisi maana yake ni "Ndiyo" yeye ni mfalme wa Wayahudi. Mara kadhaa jibu la "wewe wasema" Yesu kalitumia kutoa jibu la mbadala wa "Ndiyo" (*Mt 26:25, 64)*

6. Anuani ya hukumu yake na mateso yake na kufufuka kwake. (*Charges Agaist Him, Crucified And His Resurrection*

Katika hatua ya tano ya mateso ya Kristo, askari wa kirumi walifanya kitendo cha kumdhihaki Yesu kwa mvua nguo zake na kumvika vazi la kifalme na taji la miba kichwani pamoja na mwanzi mkono wake wa kuume na kupiga goti mbele zake kumsalimu "Salamu, Mfalme wa Wayahudi!" (*Mt 27:27-29)*

Juu ya msalaba wa Yesu iliwekwa anuani iliyoandikwa “HUYU NI YESU MFALME WA WAYAHUDI” (*Mt 27:37)*

Baada ya kufufuka Yesu alienda kwa wanafunzi wake na kuwaeleza juu ya mamlaka yake aliyonayo kwamba ni juu mbinguni na duniani, Yesu ni Mfalme mbinguni na duniani (*Mt 28:18*)

Mambo muhimu kwa kitabu cha Mathayo

Mathayo aonesha nabii za Agano la Kale zilizotimizwa kwa Yesu Kristo; -

| SN | TUKIO | SURA | AGANO LA KALE |
|---|---|---|---|
| 1 | Masihi kuzaliwa na bikira | 1:18-23 | Isa 7:14 |
| 2 | Mwana wa Daudi kuwa Mwokozi | 1:21 | Yer 23:6; 33:16 |
| 3 | Anatimiza unabii wa Agano la Kale | 1:22-23 | Zab 130:8; Isa 7:14; 8:8,10 |
| 4 | Masihi kuzaliwa Bethlehemu | 2:1-6 | Mik 5:2; 2Sam 5:2; Eze 34:23 |
| 5 | Mataifa kuja kumwabudu Masihi | 2:11 | Zab 72:8-14; Isa 60:1-3, 6 |
| 6 | Herode kuuwa watoto, Raheli kulilia wanawe | 2:16-18 | Yer 31:15 |
| 7 | Kurudi kutoka Misri | 2:14-15 | Hos 11:1; Kut 4:22,23 |
| 8 | Kuishi Nazareti | 2:23 | |
| 9 | Kama mtu ambaye kwa ajili yake mtangulizi wa Masihi alitumwa | 3:1-3 | Dan 7:14; Isa 40:3-5; Mal 3:1 |
| 10 | Tawi la Yese (Daudi) kumpokea Roho / apakwa mafuta na Roho | 3:16 | Isa 11:1-2; 61:1-2 |
| 11 | Mungu akimwelezea Mwanawe | 3:17 | Zab 2:7 |
| 12 | Huduma kuanza katika Galilaya | 4:13-16 | Isa 9:1-2 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13 | Huduma yake ya uponyaji | 8:17 | Isa 53:4-5 |
| 14 | Masihi kuwa mtendaji wa miujiza mwenye uweza | 11:4-6 | Isa 35:5-6 |
| 15 | Mtangulizi wa Masihi | 11:7-10 | Mal 3:1 |
| 16 | Mtangulizi kama Eliya aliyerudi | 11:14; 17:11-13 | Mal 4:5-6 |
| 17 | Masihi kama mtumishi mteule wa Bwana | 12:15-21 | Isa 42:1-4 |
| 18 | Wajibu wake kama mtumishiwa Mungu | 12:17-21 | Isa 42:1-4; 61:1 |
| 19 | Masihi kuwemo kaburini siku tatu machana na usiku | 12:39-40 | Yn 1:17 |
| 20 | Mioyo kufungwa kwa Injili | 13:14-15 | Isa 6:9-10 |
| 21 | Mafundisho yake kwa mifano | 13:34-35 | Zab 78:2 |
| 22 | Kuingia kwake Yerusalemu kwa ushindi | 21:4-5 | Zak 9:9; Isa 62:11 |
| 23 | Matawala ajaye juu ya punda | 21:1-9 | Zek 9:9 |
| 24 | Masihi kuja kwa jina la Bwana | 21:9 | Zab 118:26 |
| 25 | Watoto kumsifu Mwana wa Mungu | 21:16 | Zab 8:2 |
| 26 | Jiwe lililokataliwa kuwa jiwe kuu la pembeni | 21:42-44 | Zab 118:2223 |
| 27 | Yesu kama Mwana na Bwana wa Daudi | 22:41-45 | Zab 110:1 |
| 28 | Kuja kwa Mwana wa Adam | 24:30; 26:64 | Dan 7:13-14 |
| 29 | Kumpiga Masihi anayekuja, kondoo kutawanyika | 26:31, 55-56 | Zek 13:7 |
| 30 | Kumpiga mtumishi wa Mungu | 27:26-30 | Isa 50:6 |
| 31 | Masihi adhihakiwa na makutano | 27:26,41- | Zab 22:7-8 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 44 | |
| 32 | Vipande thelathini vya fedha kununulia shamba la mfinyanzi | 27:1-10 | Zek 11:1213 |
| 33 | Kupigia kura mavazi ya Yesu | 27:35 | Zab 22:18 |
| 34 | Mtumishi wa Mungu ahesabiwa na wahalifu | 27:38 | Isa 53:12 |
| 35 | Kilio cha Masihi cha kuachwa na Mungu | 27:46 | Zab 22:1 |
| 36 | Masihi kuzikwa katika kaburi la mtu tajiri | 27:57-60 | Isa 53:9 |

Mathayo aliandika Injili hii

1. Kuwapa wasomaji wake ushuhuda wa mtu aliyeshuhudia maisha ya Yesu
2. Kuwahakikishia wasomaji wake kwamba Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu na Masihi aliyesubiriwa sana na kutabiriwa na manabii wa Agano la kale
3. Kuonyesha kwamba ufalme wa Mungu ulidhihirika ndani na kupitia kwa Yesu katika njia ambayo haijawahi kutokea. Na kwa njia ya Yesu kila amwaminiye apate kuokolewa na kuingia ndani ya huo Ufalme wa Mungu.

# LUKA

**Mwandishi (*Author*)**

Katika uandishi wa kitabu hiki mwandishi hajajitaja jina lake moja kwa moja, lakini mwandishi amejulikana kwa uandishi wake na kwa aliye mwandikia. Mwandishi ni **Luka Tabibu** (Daktari) Wakolosai 4:14 na alimwandikia vitabu viwili (Injili ya Luka pamoja na Kitabu cha Matendo ya Mitume) mtu mmoja aitwaye Theofilo (Lk 1:3-4; Mdo 1:1). Kuhusu mwandishi wasifu wake ni kama ifuatavyo; -

i. Luka alikuwa ni mtu wa mataifa aliyeokoka (Myunani) aliyezaliwa Antiokia ya Shamu (Syria)

ii. Ni mwandishi pekee wa kitabu cha Biblia asiye Myahudi.

iii. Alikuwa ni mtu msomi mwenye kazi ya Utabibu

iv. Hakuwa miongoni mwa wale wanafunzi 12 wa Yesu. Lk 1:2

v. Alifanya kazi ya Injili pamoja na Paulo, naye Paulo alimwita mtenda kazi pamoja nami (Filemoni 24; 2Timotheo 4:11) vi. Ndiye aliyekuwa mwandishi wa matukio yote ya kazi ya umisheni ya Paulo (Mdo 16:10-17; 20:521:18; 27:1-28:16) vii. Kwa kuchunguza sana kwa ungalifu aliandika hakika ya mambo tangu mwanzo wa ukristo kwa Theofilo ambaye alikuwa amekwisha fundishwa kuhusu habari za Yesu Lk 1:3-4. Hii ilihusisha sehemu mbili; -


1. Kuzaliwa kwa Yesu, maisha na huduma, kifo, kufufuka na kupaa (**Injili ya Luka**)

2. Kumwagwa kwa Roho pale Yerusalemu na maendeleo yaliyofuata ya kanisa la kwanza (**Kitabu cha Matendo ya Mitume**)

Hivyo daktari Luka aliandika vitabu viwili yaani Inili ya Luka na Kitabu cha Matendo ya Mitume

Luka mwenyewe anaonekana katika habari za Biblia mara ya kwanza alipojiunga na Paulo na kikundi chake mjini Troa (Mdo 16:10-11). Luka alifuatana na Paulo Kwenda Filipi (Mdo 16:12, 16), akabaki huko Paulo na wenzake walipoendelea na safari yao (inavyo onekana katika neno “wakaenda zao”, siyo “tukaenda”) Mdo 16:40; 17:1. Inaonekana kama Luka aliishi Filipi kwa muda. Paulo alipofika Filipi tena katika safari yake ya Kwenda Yerusalemu mwishoni mwa safari ya tatu, Luka alijiunga tena na kikundi cha Paulo. Haya yanaonekana tena Luka alipojiingiza katika masimulizi yake kwa kutumia neno “sisi”

(Mdo 20:5 -6) . Tazama ramani




Ramani inayo onesha miji ya zamani kipindi cha huduma ya umisheni ya mtume Paulo.

Tangu wakati ule, Luka alishikamana na Paulo. Jambo hili linaeleza kwa nini safari ya baharini kwenda Palestina na matukio yaliyofuata huko Yerusalemu na Kaisaria yalielezwa kwa kina (Mdo 20-26). Paulo na kikundi chake walikuwa Palestina kwa muda wa miaka miwili au zaidi (Mdo 24:24), na bila shaka Luka alitumia nafasi ile kwa kuwahoji mashaihidi walio ona kwa macho maisha ya Yesu, iliyatumie maneno yale katika Injili yake. Alikuwa mtu mwangalifu aliyejitahidi sana ili habari zake kuhusu Yesu ziwe na maana na ziwe sawa kabisa (Lk 1:1-4)

Luka alisafiri pamoja na Paulo katika safari ile yenye matukio mengi ya kuelekea Rumi (Mdo 27:1; 28:16), naye aliishi pamoja naye wakati wote wa miaka miwili ya kifungo chake huko (Mdo 28:30; Kol 4:14; Flm 24). Ingawa Luka alikuwa karibu sana na Paulo katika muda wote wa miaka miwili, maelezo kuhusu nafsi yake ni haba kabisa. Inaonekana kama alikuwa mtu mnyenyekevu, aliyeweza kutegemewa kila wakati, asiyejidai kitu. Mzee Paulo alipofungwa tena baada ya kufunguliwa kwa muda, alikuwa katika baridi ya gerezani na kuona ukiwa, huko akingojea hukumu yake ya kifo, ni Luka pekeyake alivumiliana pamoja naye (2Tim 4:11)

Luka alipokuwa huko Rumi pamoja na Paulo alikutana na Marko (Kol 4:10, 14; Flm 24). Marko pia alikuwa ameandaa maandiko ya Injili, na Luka aliweza kutumia baadhi ya habari za Marko, akiziunganisha na habari alizozikusanya mwenyewe, na hivyo aliweza kukamilisha kitabu chake.

**Tarehe na Mahali (*Date and Location*)**

Injili hii inasadikika iliandikwa kati ya mwaka **60 – 63 BK** huko Rumi

**Somo Kuu (*Theme*)**

Yesu, Mwokozi aliye Mungu-Mwanadamu kamili

**Nia na Makusudi (*Purpose and Themes*)**

Kusudi la Luka limeelezwa katika mistari minne ya kwanza ya Injili hii;

[1] Kwa kuwa watu wengi wametia mikono kutunga kwa taratibu habari za mambo yale yaliyotimizwa katikati yetu, [2] kama walivyotuhadithia wale waliokuwa mashahidi wenye kuyaona, na watumishi wa lile neno tokea mwanzo, [3] nimeona vema mimi nami, kwa kuwa nimejitafutia usahihi wa mambo hayo yote tangu mwanzo, kukuandikia kwa taratibu, Theofilo mtukufu, [4] upate kujua hakika ya mambo yale uliyofundishwa. (Lk 1:1-4) Union Version Bible

Luka aliandika Injili hii kwa Mataifa ili kutoa kumbukumbu iliyo kamili na sahihi "kwa habari ya mambo yote aliyoanza Yesu kufanya na kufundisha hata siku ile alipochukuliwa juu" (Mdo 1:1b-2a). Akiandika chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu, Luka alitaka Theofilo na wadadisi na walioamini wengine Wamataifa kujua kwa uhakika Ukweli halisi kuhusu yale ambayo walielekezwa kwa midomo (Lk 1:3-4). Kwamba Luka aliwaandikia Mataifa, hiyo inaonekana katika Injili nzima; kwa mfano, anafuatilia uzao wa Yesu wa kibinadamu hadi kwa Adamu (Lk 3:23-38) na sio tu hadi kwa kwa Ibrahimu kama alivyofanya Mathayo (Mt 1:1-17). Katika Luka, Yesu anaonekana wazi kama **Mwokozi Mungu-Mwanadamu** ambaye alitolewa na Mungu kwa ajili ya ***wokovu wa uzao wote wa Adamu***.

**Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. (Lk 19:10) Union Version Bible**

Maisha yake makamilifu kama Mwana wa Mtu na wakati huo huo Mwana wa Mungu unaonekana wazi kwa ukweli kwamba kuzaliwa kwake katika Ukoo kumeanzia tangu enzi za Adamu (Lk 3:38, tofauti kabisa na jinsi Mathayo aliyo elezea amekwenda nyuma hadi enzi za Ibrahimu pekee). Hekima zake zinaonekana katika Lk 2:40-52 na maadili yake na ukamilifu wake unashuhudiwa wakati wa ubatizo wake kwa njia ya sauti ya Baba yake kutoka Mbinguni na kwa upako wa Roho Mtakatifu Lk 3:21-22.

**"Yesu ndiye pekee tuliyenaye na ni Mkamilifu Kimwili, Kiakili na Kiroho"**

**Upekee wa Injili ya Yohana (*The Uniqueness of Luke's Gospel*)**

Injili ya Luka ni Injili ya kihistoria. Hakuna waandishi wengine waliotoa tarehe za matukio aliyoyaandika (Lk 1:5; 2:1 na 3:1-2). Yeye mwenyewe alikuwa ni mwanahistoria na mjuzi katika uandishi.

Injili ya Luka ni ya kimafundisho ya Mungu. Luka alikuwa ni mshirika wa Paulo katika huduma za Injili, pia yeye mwenyewe alikuwa muhubiri wa neno la Mungu, Mchungaji na Mishenari, hivyo alikuwa na uhakika wa mafundisho aliyo kuwa akiyatoa kuwa ni ya kiMungu. i. Luka amefundisha juu ya Ubinadamu na Asili ya Yesu Kristo (Lk 1:35; 4:41; 9:35) ii. Amefundisha juu ya Toba ya kweli na wokovu na ukombozi (Lk 19:10) iii. Ametoa mafundisho juu ya Roho Mtakatifu (Lk 1:15, 35, 42, 67; 2:25-26; 3:22; 14:1, 14, 18; 10:21;

24:49) iv. Ameeleza juu ya Maombi (Lk 11:1-13; 22:39-44)

v. Ametoa fundisho juu ya maisha ya watu (10:38-42; 19:1-10; 24:13-35)

**Tabia za injili hizi tatu**

Kila injili ni ya tofauti na nyingine katika kiini au mawazo makuu ya mwandishi. Lakini yapo matukio mengine mengi amabyo injili hizi tatu zimeyaeleza kila moja.

**A. Matukio Yanayofanana Kwa Kila Injili**

1. Tangazo la kuja kwa Yesu lililo tolewa na Yohana Mbataizaji (Mt 3, Mk 1, Lk 3)
2. Ubatizo wa Yesu (Mt 3, Mk 1, Lk 3)
3. Majaribu ya Yesu (Mt 4, Mk 1, Lk 4)
4. Mabadiliko ya Yesu mlimani (Mt 17, Mk 9, Lk 9)
5. Kuteswa, kuuawa, kuzikwa kwa Yesu (Mt 26-27, Mk 14-15, Lk 22-23)
6. Kufufuka kwa Yesu (Mt 28, Mk 16, Lk 24)

## B. Kuzaliwa Kwa Yesu Kusivyo Kwa Kawaida

Kuzaliwa kwa yesu kunaonekana ni kwa tofauti kwa sababu: -

1. Manabii wa Agano la Kale walitabiri juu ya kuzaliwa kwake
2. Malaika walitangaza kuzaliwa kwake
3. Roho Mtakatifu aliwathibitishia watu juu ya kuzaliwa kwake (Mt 1-2, Lk 1-2) 4. Yesu alizaliwa na mwanamke bikira

## C. Mifano ya Bwana Yesu

Bwana Yesu katika kufundisha kwake alitumia zaidi mifano na miujiza. Moja ya makusudi ni kutoa mafundisho muhimu na ya kweli ya kiroho.

Katika injili hizi tatu kuna jumla ya mifano isiyopungua thelathini. Miongoni mwa mifano hiyo ni Mfano wa Ufalme wa Mungu (Mt 13), Mwana mpotevu (Lk 15). Katika injili ya Yohana hakuna mifano yoyote ya Bwana Yesu. Yeye alikazia mambo mengine.

## D. Ufalme Wa Mbinguni Na Ufalme Wa Mungu

Katika injili hizi tatu neno "Ufalme wa mbinguni" na "Ufalme wa Mungu" limetajwa sana. Ufalme wa mbinguni na ufalme wa Mungu ni maneno mawili tofauti. Lakini neno Ufalme wa Mbinguni linaonekana zaidi katika injili ya Mathayo. Ni kwa nini Mathayo ametumia neno hili zaidi. Itakumbukwa kuwa Mathayo aliwaandikia Wayahudi. Wayahudi hutumia neno Mbinguni kuepuka kutaja jina "Mungu" kwa sababu jina Mungu ni takatifu sana kiasi cha kutoweza kulitaja. Hivyo hutumia neno Mbinguni badala ya Mungu.

- Ufalme wa Mungu ni halisi/Kweli, anatawala juu ya viumbe wake. Ni utawala wa kiroho, hauonekani kwa mamcho ya mwili, upo ndani ya mioyo ya waamini. (Lk 17:20b, 21b)
- Ufalme wa Mungu utakuja na utakuwa dhahiri hapa duniani. Hii itatokea pale ambapo "Mwana wa Adamu atakapo kuja katika utukufu na mataifa yote yatakusanyika mbele zake" (Mt 25:31a,

32a). mwana wa Adamu ataonekana na kutawala hapa juu ya nchi. Manabii walitabiri jambo

hili (Isaya 11:1-10; Zakaria 13:1-6; Malaki 4:1-3; Mt 3:1-3; Mk 1:14-15)

## E. Miujiza ya Bwana Yesu

Yesu alionesha kuwa yeye ni Masihi kwa njia ya mafundisho yake na miujiza. Miujiza aliwafanyia watu waelewe uhitaji mkubwa wa Mungu katika maisha yao. Miujiza ya kuonekana ilidhihirisha kuwa Yesu ana nguvu kuweza kukidhi mahitaji ya kiroho ya watu.

Marko ameandika miujiza mingi zaidi ya Mathayo na Luku. Ameandika jumla ya miujiza ishirini. Hii ndiyo sababu injili ya Marko inaitwa ni Injili ya Matendo.

*Hitimisho*

**Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. (Lk 19:10)** Union Version Bible

Kilichomfanya Yesu aache enzi na mamlaka yake huko mbinguni na kuja kuzaliwa na kuvaa mwili wa binadamu ni ili kutuokoa sisi wanadamu na dhambi zetu.

Hakuna mwanadamu awezaye kujiponya au kujiondolea dhambi isipokuwa amemwamini huyu Yesu Kristo. Luka kaandika injili yake kuonesha njia ya wokovu wa mwandamu kuwa ni kwa Yesu pekee. Wokovu huu ni kwa kila mtu aminiye kuwa Yesu ni Bwana na Mwokozi wa maisha naye ataokoka.

**9 Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini**
**moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. 10 Kwa maana**
**kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata**
**wokovu. 11 Kwa maana andiko lanena, Kila amwaminiye hatatahayarika. 12 Kwa**
**maana hakuna tofauti ya Myahudi na Myunani; maana yeye yule ni Bwana wa**
**wote, mwenye utajiri kwa wote wamwitao; 13 kwa kuwa, Kila atakayeliitia Jina la**
**Bwana ataokoka.**

**(Warumi 10:9-13)** Union Version Bible

# MATENDO YA MITUME.
# (ACTS)

<u>UTANGULIZI:</u>

1. Kitabu cha matendo ya mitume ni DARAJA (Bridge) linalounganisha vitabu vya Injili na Nyaraka na Ufunuo, kama si kitabu hiki cha matendo ya mitme tungeruka Injili hadi Warumi mambo yote tunayoyapata katika kitabu cha matendo tusingeyapata, tusingejua jinsi kanisa lilivyoanzishwa pia tusingejua Injili ilifikaje Rumi. Tusingejua habari za Mitume na waliyoyafanya baada ya Yesu kufufuka. pia tusingejua makanisa yaliyotajwa kwenye Ufunuo na nyaraka jinsi yalivyoanzishwa.

2. Mwandishi ni Dr. Luka Matengo **1:1, Luka 1:1-4**, kabila Myunani, Nyumbani kwao inaonekana ni kama Troa, Jimbo la Bithinia. **16:6-8.** Licha ya kuwa hajitaji lakini ukichunguza katika maandiko haya utamwona akijitaja, kwa kutumia Neno la wingi, sisi, Tukang'oa nanga takatifu **(16:10-17, 20:5-15, 21:1-18, 27:1, 21:16)** pia nimwandishi pekee alie myahudi.

3. Sehemu alikoandikia ni Rumi au Kaisali
4. Kusudi la kuandika Dr. Luka aliandika ili kumweleza theophilo aliekuwa afisa katika serikali ya kirumi kuwa ukristo aupingani na serikali ya kirumi.

5. Kitabu cha matendo kilichoandikwa kama mwaka wa 64 BK.
6. Kitabu kina sura 28. mistari 1007

7. Mstari mkuu wa kitabu ni 1:8" lakini mtapokea nguvu akisha kuwajilia juu yenu roho mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu na katika uyahudi wote na samaria, na hata mwisho wan chi.

8. Wasemaji wakuu wa  kitabu cha matendo ya mitume
    a. Kuanzia sura ya 1:1 hadi 12:13 msemaji mkuu alikuwa mtume Petro
    b. Kuazia sura ya 13:1 hadi 28:31, msemaji mkuu alikuwa mtume Paulo

9. Kitabu hiki kingefaa kiitwe matendo ya roho mtakatifu, kwa sababu matendo yote yaliyo elezwa katika kitabu hiki ya metendwa na roho mtakatifu.

10. Muundo wa kitabu Dr. Luka amekiandika kihistoria kijiografia, akionyesha roho mtakatifu kuwa ndie ufunguo wa mafanikio yote ya injili.

**KITABU KIMEGWANYIKA KATIKA SEHEMU KUU TATU NA ANDIKO KUU LA MGAWANYO WA KITABU NI MATENDO 1:8**

A. **SEHEMU YA KWANZA – SURA YA 1 HADI YA 7**

(Mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu)

B. **SEHEMU YA PILI – SURA YA 8 HADI YA 12**

(Kupanuka kwa kanisa, mtakuwa mashaidi wangu katika Uyahudi na Samaria)

C. **SEHEMU YA TATU – SURA YA 13 HADI YA 28**

(Kuenea kwa kanisa, mtakuwa mashahidi wangu hata mwisho wa Nchi)

**UPEKEE, UZURI NA UMUHIMU WA KITABU CHA MATENDO YA MITUME.**

1. **NI KITABU PEKEE CHA HISTORIA KATIKA AGANO JIPYA.**

ni kitabu muhimu kinachoonyesha historia ya kanisa na jinsi zilivyoenea ulimwenguni na ni kitabu kinachotumiwa na watu wengi wa Kikristo na wana historia.

2. **KITABU KIPEKEE KINACHOFUNDISHA ROHO MTAKATIFU NA FUNGUO YA MAFANIKIO YA INJILI NI ROHO MTAKATIFU.**

Luka anatmia neno Roho mtakatifu Zaidi ya mara 50, pia neno roho mtakatifu limejitokeza katika kila kurasa hii ni kuonyesha kuwa roho mtakatifu ndiyo kiini cha mafanikio katika huduma ya injili.

3. **KITABU KINACHOFANANA NA KITABU CHA MWANZO.**

Kitabu chwa mwanzo kinaonyesha mwanzo wa uumbaji wa ulimwengu, mwanzo wa dhambi, mwanzo ukombozi, mwanzo wa Imani n.k

Pia na kitabu cha matendo ya mitume ni kama kitabu cga mwanzo katika kanisa kinaonyesha mwanzo wa kanisa, mwanzo wa huduma ya ushemasi, mwanzo wa manung'uniko kanisani, mwanzo wa mtu kufa kwa ajili ya Kristo, mwanzo wa wahumini waongo (mfano safira na anania) n.k

Hivyo kinafanana sana na kitabu cha mwanzo kinachoonyesha mwanzo wa ulimwengu na hiki kitabu cha matendo kinaonyesha mwanzo wa kanisa.

4. **KITABU KINACHOONYESHA UTENDAJI WA HUDUMA KWA AJILI YA KRISTO.**

Kitabu kinafundisha kuwa huduma zote tunazozifanya lazima zilenge kuonyesha kuwa Yesu Kristo kuwa ni bwana na mwokozi wa maisha yetu (Matendo 26:17-18). kitabu kinatuonyesha ujumbe wa mhubiri lazima ubakie kuwa Yesu Kristo ni Bwana.

Hivyo uponyaji, mafanikio, msaada, maadili mema, sifa binafsi sio ujumbe bali ujumbe ni YESU KRISTO NI BWANA NA MWOKOZI hayo mengine yafanyike lakini ya walete watu kwa Kristo.

**NB:** In any every spiritual service must be Jesus alwayas be the center healings Entertainment deliverance prosperity and all things its good but cannot become the Message **THE MESSAGE MUST REMAIN CENTER AND FOCUSED UPON JESUS IS CHRIST.**

5. KITABU KINACHOHUSU WATU NA HUDUMA (UINJILISTI)

Hiki ni kitabu pekee kinachoonyesha huduma ya uinjilisti na kinaonyesha mtumishi wa Mungu ni mtu anaye watumikia na kuwahuduia watu kwa ajili ya mambo na faida ya Mungu sio mtu anayetafuta mambo yake binafsi.

**NB:** A servant of God must be a servant of the people for profit and interest of God not self.

6. NI KITABU KINACHOHUSU KANISA

Kitabu cha matendo ya mitume ni kitabu kinachoonyesha maana ya kanisa, lilianza lini na jinsi lilivyoenea ulimwenguni na nia yake na nguvu yake na ushawishi wake

KANISA NI NINI

kanisa sio jengo wala dhehebu wala kampuni kanisa ni watu waliotengwa na Mungu na waliomwamini Yesu Kristo na walio kubali msamaha wa dhambi zao kwa njia ya kifo cha msalaba cha Yesu Kristo ***(kifupi kanisa ni mtu aliyepokea roho mtakatifu au kusanyiko la watu waliojawa na roho ya bwana(Matendo ya mitume 1:8; 2:1-30)).***

MGAWANYIKO WA KANISA

kwa asili kanisa ni moja tu na Yesu analijenga kanisa moja tu hivyo kanisa hilo limegawanyika sehemu kuu mbili nazo ni:

1. KANISA LISILOONEKANA (ORGANISM CHURCH/INVISIBLE CHURCH)

hili ni kusanyiko la watu waliomwamini Yesu kristo walioandikwa katika kitabu cha uzima ambao sisi wanadamu hatuwajui anawajua Mungu ambao ni watakatifu waliopo mbinguni pamoja na wale ambao ni waamini wa kweli waliopo duniani (ufunuo wa yohana 3:5-8)

Alionekani kwa sababu hatuwezi kuwajua isipokuwa Mungu yeye anawajua watu wake ambao ni waamini wa kweli.

***NB: NDUGU YANGU MWAMINI YESU ILI UANDIKWE KWENYE KITABU CHA UZIMA NA KUURITHI UZIMA WA MILELE***

2. KANISA LINALOONEKANA (ORGANIZATION CHURCH/VISIBLE CHURCH)

hili ni kanisa ambalo tunaliona na kulitambua lenye waumini, jengo, viongozi, katiba kwa ufupi ni taasisi ya dini ya kikristo.

(Cheo, uzuri wa majengo, uzuri wa huduma sio sababu ya kukufanya uurithi uzima wa milele, bali kumwamini Yesu Kristo na kukubali kazi ya msalaba ndani ya moyo wako ndio kumekufanya kuwa kanisa la Mungu na kuurithi ufalme wa milele)

***NB: KANISA NI ORGANIZATION AND ORGANISM HIVYO KANISA NI MWAMINI MMOJA MMJOA ALIYEMWAMINI MUNGU NA KUMIRI YESU KRISTO KUWA BWANA NA MWOKOZI WAKE PIA NI JENGO NA NI TAASISI.***

***ZIFUATAZO NI NGUZO ZITAKAZO KUFANYA ULIJUE KANISA LA KWELI LILE LILILO KATIKA KITABU CHA MATENDO YA MITUME.***

1. solar scripture (iwe ni ya kibibliasio kihisia)
2. solar faith (mafundisho yake yawe ya kiimani)
3. solar Christ (mafundisho yote yamuelekee Kisto kuwa Bwana na mwokozi, kanisa limtangaze Yesu, limuinue Yesu, Limuabudu Yesu sio mchungaji au kiongozi wake)
4. solar Grace (wokovu kwa Neema, utumishi kwa neema, mwenendo kwa neema sio kwa juhudi wala bidii zetu)
5. Priesthood for all (ukuhani kwa wote, wote tumefanyika kuwa makuhani kwa Yesu, wote tunajifunza kwa Yesu, wote tunahaki ya kumuomba Mungu, kumtolea Mungu na wote tunamtegemea Yesu).

# 1 WAKORINTHO

### Mtunzi Na Jina La Kitabu (*Author and Recipients*)

Paulo ndiye mwandishi wa kitabu hiki maana amejitaja mwenyewe mara nyingi. (1 Kor 1:1; 16:21)

Usomaji wa makini wa kitabu cha Matendo na hata nyaraka mbalimbali unaonyesha muhtasari wa Paulo jinsi alivyojihusisha na kanisa. Kulikua na safari yake ya kwanza kwa Wakorintho (Mdo 18:1), iliyofuatiwa na; -

1. Barua ya kwanza kwa Wakorintho (ambayo hii ilipotea). (1 Kor 5:9). Halafu ilifatiwa na,

2. Barua ya pili kwa Wakorintho (ambayo ndiyo 1 Wakorintho). Halafu kulifuatiwa na,

3. Barua ya tatu kwa Wakorintho (ambayo nayo ilipotea) (2 Kor 2:3-4). Halafu kuatiwa na,

4. Barua ya nne kwa Wakorintho (ambayo ndiyo 2 Wakorintho)

Hapa ieleweke kwamba barua mbili zilizopotea ni kwa sababu hazikuwa zimekusudiwa na Mungu kuwa sehemu ya maandiko.

**Muda Wa Kuandikwa (*Date*)**

Barua hii iliandikwa kati ya miaka ya 53-55 BK ikieleza mwisho wa miaka mitatu ya kukaa kwa Paulo huko Efeso (1 Kor 16:5-9; Mdo 20:30). Kwahiyo kitabu hiki kiliandikwa Efeso.

**Historia na Jiografia ya Mji wa Korintho (*Historical & Geographical background of Corinth*)**

Mji Korintho ulikuwa maili 46 (kilometa 74) magharibi mwa Athene (makao makuu ya Akaya),

(ramani 1 na 2). Ulikua chini ya dora/koloni la Rumi, pia ulikua ni miongoni mwa miji ya Akaya (wagiriki/wayunani). Kipindi mtume Paulo anafika katika mji huu katika safari yake ya pili ya umisheni, ulikua unatawaliwa na Gavana wa kirumi aitwaye Galio. (Mdo 18:12).

Korintho ulikua ni mji mkubwa na sehemu ya ardhi iliingia katika maji ya bahari (rasi) ya Aegean na bahari ya Adriatic inayounganisha Peloponnesus na Northern Greek. Paulo na wenzake walikua wameshangazwa na mafanikioa ya Injili ya haki ya Mungu ilivyokua imeenea Korintho. Kama mji ulikua na vitu vingi na mji wa anasa. Mji ulikua na madini na mahekalu yaliyokuwa mazuri hasa kwa hekalu la Aphrodite lililokuwa juu futi 1800 (mita 550) kilele kiliitwa Acrocorinthus. Katika maandishi ya Kiyunani ilikuwa ni nchi ya utajiri sana. Neno “Msichana wa Kikorintho” lilimaanisha ni “Malaya”. Neno “kutenda kama Mkorintho” ilimaanisha kufanya “anasa”. Utajiri na vitu vya Korintho viliwekwa kuzunguka hekalu la Aphrodite n ahata Malaya wake. Kwa maana hii kukawa na methali iliyosema na kutahadharisha “Si kila mtu ni msafiri wa Korintho”.

**Nia Na Madhumuni (*Purose*)**


Ili kuelewa nia na madhumuni ni vizuri tukielewa historia fupi. Kulingana na Matendo, Paulo alikuwa na waongofu kutoka kwa wayahudi na hawa walikuwa ni watakatifu. Wengi wao walitoka watika maeneo ya kuheshimiwa japo wengine walikuwa katika nafasi mbaya (1 Kor 1:26-31). Hali ya kiuchumi ilikuwa nzuri kwao (1 Kor 7:20-24; 11:21-34) na wengine wao walitoka katika upagani (1 Kor 6:9-11). Kwa kuwa wengine walikuwa ni Wayunani walijivuna (1 Kor 1:17; 2:1-5).

Waweza kuona ni kwa jinsi gani anasa ilivyokuwa imeliharibu kanisa la Korintho kiroho na hata kimaadili. Nia ya waraka huu ni maisha mapya ya kikristo na watakatifu walioitwa na utakaso wa kila namna ya maisha. Maisha haya mapya katika Kristo yanaitwa kwa njia mpya ya Roho Mtakatifu (1 Kor 3:16, 17; 6:11, 19-20). Hekima ya Mungu imedhihilishwa ili itubadili katika sehemu zote za kibinafsi na hata kijamii.

Kwahiyo 1 Wakorintho iliandikwa kama ya kichungaji ili kurekebisha matatizo na fujo zilizokuwa katika kanisa (1 Kor 1:11), kumtumaini mwanadamu au ulimwengu zaidi ya Mungu (1 Kor 1:21-30), uasherati (1 Kor 5:1-13; 6:9-20), ibada za sanamu (1 Kor 10:20-22) na maswali kuhusiana na talaka na ndoa, chakula, ibada, karama za roho, na hata ufufuo. Kwa sababu ya mashaka yao ya dini na uasi waliokuwa wakifanya, mafundisho ya uongo na Imani potofu zilitawala kanisa.



*Picha 1: Ramani Ikionesha Miji Kipindi Cha Safari Ya Kwanza Na Pili Ya Mtume Paulo.*




*Picture 2: The Setting of 1 Corinthians.*

Pia katika kitabu hiki Paulo ameandika kujibu na kutoa suluhu ya changamoto ambazo zilionekana kwa kanisa la Wakorintho kutoka kwa familia ya Kloe (1 Kor 1:11). Changamoto ambazo zilionekana kwa kanisa hilo zimegawanyika katika makundi mawili (02) kama ifuatavyo;-

1. Changamoto za kiroho (kikanisa)
2. Changamoto za kifamilia (kijamii)

**Changamoto za kiroho (kikanisa)** ***(Spiritual or Church Problems)***

Miongoni mwa changamoto za kikanisa au kiroho zilizolikumba kanisa la Wakorintho ambazo

Paulo alialifiwa ni; -

i. Migawanyiko ndani ya kanisa kutokana na ubatizo (1 Kor 1:10-17; 3:1-23)

ii. Mashitaka miongoni mwa waumini isivyofaa kutokana na fitina na dhuruma (1 Kor 6:1-8)

iii. Kula vyakula vilivyotolewa sadaka kwa sanamu (1 Kor 8:1-13) iv. Wanawake kufunika vichwa ndani ya kanisa (1 Kor 11:2-22)

v. Kula meza ya Bwana isivyofaa (1 Kor 11:17-22; 26-34)

vi. Matumizi mabaya ya karama (1 Kor 12:1-31; 14:1-25)

vii. Kukosekana kwa upendo ndani ya kanisa (1 Kor 13:1-13)

viii. Kukosa utaratibu wa ibada (1 Kor 14:26-40)

ix. Fundisho baya juu ya ufufuo (1 Kor 15:1-34)

**Changamoto Za Kifamilia (Kijamii)** ***(Family & Social Problems)***

Miongoni mwa changamoto za kifamilia au kijamii zilizolikumba kanisa la Wakorintho ambazo

Paulo alialifiwa ni; -

i. Uasherati na uzinzi (1 Kor 5:1-8)

ii. Migogoro ya ndoa (1 Kor 7:1-40)

iii. Mgawanyiko kati ya wenye uwezo na wasio nao. (1 Kor 11:20-22)

**Majibu Na Suluhu Ya Paulo Kwa Changamoto Za Kanisa La Korintho**

***Changamoto za kiroho (kikanisa) (Spiritual or Church Problems)***

| SN | CHANGAMOTO | MAJIBU |
|---|---|---|
| 01 | Migawanyiko ndani ya kanisa kutokana na ubatizo (1 Kor 1:10-17; 3:1-23) (*Division in the Church due to Baptism*) | Paulo anasisitiza zaidi kuwa kuhubiri injili ni bora zaidi ya kubatiza (1Kor 1:17a)<br>Paulo anasihi kutotumia hekima ya dunia hii kama wao walivyowagawa hao watumishi (Apolo, Paulo na kefa) katika uweza wao na huduma. Bali wanapaswa kuwaona wote ni watenda kazi katika Kristo kwani kila mmoja anahuduma yake na Kristo ndiye msingi wa yote. (1Kor 1:17b; 18-31; 3:4-23; 12:5-7)<br>Paulo anaonya wakorintho kuacha tabia za kale za mwilini (1kor 3:1-3)<br>Paulo aliwakataza migawanyiko anasihi kanisa kunena mamoja na kuwa na shauri moja (1Kor 1:10) |

| | | |
|---|---|---|
| 02 | Migawanyiko miongoni mwa waumini isivyofaa kutokana na fitina na dhuruma (1 Kor.6:1-8) *(Division in the Church due to Lawsuits agaist belivers)* | Paulo anasihi tofauti kati ya waumini zitatuliwe chini ya uongozi wa kikanisa, migogoro ya waumini isitoke nje ya kanisa ili kutunza ushuhuda wa Kristo. (1Kor 6:11)<br>Paulo anaeleza juu ya kujitenga na dhuruma pamoja na fitina maana ufalme wa Mungu sio wa hao fanyanyayo hayo (1Kor 6:9-11) |
| 03 | Kula vyakula vilivyotolewa sadaka kwa sanamu (1 Kor 8:1-13) *(Eating food offered to idols)* | Viongozi pamoja na wenye kuonekana wamesimama kiimani walipituka kwa ujuzi wao hata kujipa haki ya kula vyakula vilivyotolewa sadaka kwa masanamu kutokana na mazoea yao (1kor 8:7; 10:12). Paulo anaonya kwa kufanya hivyo kunawaangusha walio wachanga kiimani na kuwarudisha nyuma kiroho. (1Kor 8:9-13). |
| | | Pia anasisitiza juu ya kulinda Imani za wengine, *kwanini kukwaza?!*. Hapa kisiwe chakula tu bali kitu chochote ambacho kitadhoofisha Imani ya ndugu ni bora kisifanyike ili kujengana kiroho. (1Kor 8:13; 10:23-24)<br>Paulo anatoa katazo la kutokula vyakula hivyo kwani ni sawa na mtu kushiriki pamoja na mashetani, maana nyuma ya sanamu kuna roho ya mashetani (1Kor 10:14; 18-22) tena wasiwe waabudu sanamu, wala washereti wa kuabudu miungu na kumjaribu Mungu. (1Kor 10:7--9).<br>Kwa msisitizo Paulo aliagiza kama ikibainika mtu huyo yupo miongoni mwa kanisa hata kuchangamana nae hairuhusiwi (1Kor 5:11) |

| | | |
|---|---|---|
| 04 | Wanawake kufunika vichwa ndani ya kanisa (1 Kor.11:2-22) *(Head coverings)* | Kufunika kichwa kwa mwanawake anapokua hadharani tangu karne ya kwanza kwa jamii ya kirumi ilimaanisha kuwa huyo mwanamke ni ameolewa.<br>Paulo alilenga mwonekano na uhusiano kati ya mwanamke na mwaume lakini pia kati ya mke na mume. Anaeleza mtiliriko wa kimamlaka kati ya mume na mke kuwa mume ni kichwa cha mkewe, na mke anapaswa ajitiishe chini ya mumewe kwa taswira hiyo Paulo amelinganisha kuwa Yesu ni kichwa cha kanisa na kanisa lapaswa kujitiisha chini ya Yesu. (1kor 11:3)<br>Kimaongozi kanisa lipo chini ya Kristo, na Kristo chini ya Baba, vivyo hivyo na mke chini ya mume, nae mume chini ya Kristo.<br>Kwahiyo mwanamke aliyendani ya ndoa alipaswa awe katika viashilia kuwa yupo ndani ya ndoa kwa kufunika kichwa awapo katika haraiki ya watu au kanisani (1Kor 11:5). Lakini hapa ieleweke kuwa zipo ishara nyingi katika jamii mbali mbali na ambazo zinapaswa kuonesha kuwa mwanamke yupo ndani ya ndoa kama vle ***pete ya ndoa*** n.k kutokana na jamii husika. (Mwa 2:22-23, 1kor 11:8-10)<br>Sasa katika kanisa la korintho kulionekana wanawake walio olewa kutofunika vichwa vyao kitu ambacho kilionesha ni kuvunja heshima ya waume (vichwa) zao, pia ni kama mwanamke kuonekana anahitaji mwanume au hajaolewa (ishara ya uzinzi). Paulo kaandika ili mambo hayo yasimamiwe vizuri. (1kor<br>11:5-6)<br>Vivyo hivyo kwa jamii ya kiyahudi wanaume hawakupaswa kuwa katika mwonekano wowote wa kike, kwa kufunika kichwa wala kuacha nywele ndefu. (1Kor 11:7; 14; Kumb 22:5). Mwanaume hapaswi kuonenakana katika hali ya kike maana yeye ni utukufu wa Mungu nae mke ni utukufu wa mume<br>(1kor 11:7).<br>Paulo kaandika haya si kwa kuwakandamiza wanawake bali mwanaume na mwanamke wote kwa Mungu ni sawasawa kwani wameumbwa kwa mfano wa Mungu na wanapaswa kumtegemea Mungu (1kor 11:11-12; Mwa 1:27-28) |

| | | |
|---|---|---|
| 05 | Kula meza ya Bwana isivyofaa (1 Kor 11:17-22; 26-34) *(Badly conduct of Lord's Supper)* | Paulo alionya kanisa juu ya ulaji mbaya wa meza ya Bwana, maana kati yao kulikua na mgawanyiko kati ya wenye uwezo na wasio na uwezo hata wale wenye uwezo wakawa wanakula na kushiba na kunywa hata kulewa na wale walio hawana uwezo wakiwa na njaa. (1kor 11:20-21).<br>Kwa kukosa utaratibu ndani ya kanisa kulionesha ishara ya kudharau kanisa la Mungu (1kor 11:22)<br>Paulo anaeleza maana ya meza ya Bwana (1kor 11:26) na pia anaeleza hasara za kula meza hiyo vibaya kwa kutopambanua (1kor 11:30).<br>Kabla ya mtu kula meza ya Bwana ni lazima ajihoji mwenyewe hali ya utakatifu na usafi wa moyo wake. Kukiri dhambi zake na kuzitubia. (1kor 11:28-29)<br>Paulo anashauri kwa kanisa kuwapo na utaratibu wa kungojeana wakati wa kushiriki meza ya Bwana (1kor 11:33) |
| 06 | Matumizi mabaya ya karama (1 Kor 12:1-31; 14:1-25) *(Badly conduct of Spiritual Gifts)* | Katika kanisa kulionekana kutengenezwa kwa magawanyiko juu ya karama za Roho. Paulo anajaribu kutumia lugha ya mwili na viungo vyake (1kor 12:1227). Jambo ambalo lilionekana kwao ni kuwekea mkazo kwenye karama ya aina fulani tu na hata wale wasio na hiyo karama kujiona kama sio sehemu ya mwili yaani kanisa (1kor 12:16-17). Kwa muonekano wa maelezo ya Paulo (1kor 14:18) kunaonekana yamkini karama ya kunena kwa lugha ndiyo ilikua ni bora zaidi kwa wakorintho kuliko zingine, kwamba kulikuwa na majivuno nani ni bora zaidi ya mwingine, kitu ambacho kilivunja Imani za wengine na kujiona duni.<br>Kulikua hakuna utaratibu mzuri wa matumizi ya kunena kwa lugha katika ibada zao, zaidi Paulo anawataka wahutubu (*prophesy*). (1kor 14:7, 26).<br>Ndani ya kanisa anasisitiza kuwe na kuhutubu zaidi ya kunena kwa lugha ili kulijenga kanisa na kuwafanya wale wasio amini kuamini. (1kor 14:3, 5, 12, 2425). Akili itumike ili wasio amini nao waamini, hivyo kufasiri lugha kuwepo (1kor 14:20-23) |

| | | |
|---|---|---|
| | | Paulo anatoa utaratibu katika kunena kwa lugha ndani ya kanisa na unabii (kuhutubu) pia (1kor 14:27-32; 39-40)<br>Paulo anaeleza kuwa karama zipo tofauti kila mmoja hupewa na Roho lakini zote hulenga kuimalisha kanisa kwa kufaidiana ili yule asiye na ya aina fulani basi hunufaika kwa mwenye nayo. (1kor 12:4). Huduma nazo pia kila mmoja hupewa ya kwake nazo hulenga kumtumikia Bwana mmoja, hivyo kila huduma ya mtu iheshimiwe (1kor 12:5-6). Iwe karama au huduma au utendaji wa kazi kwa Bwana hutolewa kwa Roho ili kufaidiana na kujengana (1kor<br>12:7,11)<br>***1kor 14:34-35. Ni kweli wanawake watakiwi kunena ndani ya kanisa?*** Paulo mwenye japo amekataza wanawake walio olewa kusali na kuhutubu ndani ya kanisa bila kufunika vichwa vyao (1kor 11:5, 13). Lakini katazo hilo sio sheria kwa makanisa yote kwani wanawake bado wamepewa karama na Roho na wanatenda kazi ndani ya kanisa (Mdo 2:17; 21:8-9). Yamkini katika mistari hii, 34-35 Paulo anakataza wanawake kusema chochote au kukinzana wakati wanaume wakiwa wanahutubu ndani ya kanisa (*women to speak up and judge prophecies*) kwasababu itakuwa ni kama kudharirisha hali ya mwanaume kama kichwa (*Undermine male headship*). Lakini pia yamkini Paulo akawa anazingatia sheria ya uumbaji kuwa mwanamke alitoka kwa mwanaume na yupo kwaajili ya mwanaume. (*woman's creation "from" and "for" the man*) (1kor 11:8-9; Mwa 2:20-24) pia katika agano la kale jamii ya Israel mwanaume alikua ni mtawara (*male headship*). Wanawake hawajazuiwa kutumika kanisani bali katika huduma zao staha kwa waume zao izingatiwe. |
| 07 | Kukosekana kwa upendo ndani ya kanisa (1 Kor 13:1-13) *(the way of Love)* | **Chanzo cha mgawanyiko ndani ya kanisa la korintho na migogoro mingine yote ni kwasababu ya kukosekana kwa Upendo.**<br>Paulo kaanza na kuizungumzia karama ya kunena kwa lugha kitu ambacho kwa kanisa la korintho lionekana ni bora zaidi, sasa anaeleza kuwa kama hakuna Upendo hiyo karama ni bure (1kor 13:1).<br>Katika yote upendo ndio unaoshika nafasi ya kwanza, kwani unapokuwepo mengine yote hufunikwa ndani yake. (1kor |

| | | |
|---|---|---|
| | | 13:13) |
| 08 | Kukosa utaratibu wa ibada (1 Kor 14:26-40) *(Orderly worship)* | Kwa muonekano wa ibada zao Paulo anaeleza kuwa walikua wanakusanyika kwa hasara (1kor 11:17; 14:26)<br>Paulo kwa kuona kukosekana kwa utartibu wa ibada wakati wa kusanyiko akasisitiza kuwepo na utaratibu wa ibada zao (1kor 14:28-33; 40) |
| 09 | Fundisho baya juu ya ufufuo (1 Kor 15:1-34)*(The bodly resurrection of*<br>*Christ from dead)* | Watu wengi zamani kutoka katika jamii za wagiriki wa kirumi (*Greco Roman*) waliamini mtu akifa basi ndo mwisho wa kila kitu, kitakachobaki ni kivuli cha huyo marehemu kuwa chini ya dunia.<br>Hali ya kuwa na mwili mwingine baada ya kufa hawakuamini hilo na ilionekana kama ni ujinga na upuuzi kwao mtu kusema kuwa kuna ufufuo wa wafu (Mdo 17:31-32).<br>Paulo mwenyewe alikutana na watu hao kipindi cha safari zake za umisheni huku Athene (Mdo 17:22-32) unaona jinsi walivyosikia habari za ufufuo walifadhaika. Na katika jiografia Athene na Korintho ni miji ambayo ipo karibu sana (*ona picha 1*) hivyo kulikuwa na mwingiliano mkubwa na elimu hiyo potofu nayo ilienea na kuzungumzwa sana lakini pia iliharibu kanisa.<br>Paulo anasema mazungumzo hayo mabaya yanaharibu tabia njema (1kor 15:3334)<br>Kwakuwa kulikuwa na mwingiliano wa watu hawa katika jamii ya kanisa la korintho Paulo kaandika kuondoa mkanganyiko huo ambamo wapo miongoni mwao waliamini hayo mafundisho potofu, kuwa mtu atafufukaje? au atavaaje mwili mpya nawakati mwiliwake umezikwa na umeoza? (1kor 15:12; 35)<br>Paulo pia anawaeleza juu ya ufufuo kuwa Yesu ndiye mwenye kufufua katika miili ya mbinguni ya utukufu na sio katika miili ya damu na nyama (1kor 15:3558; 6:14) |

*Changamoto Za Kifamilia (Kijamii) (Family & Social Problems)*

| SN | CHANGAMOTO | MAJIBU |
|---|---|---|
| 01 | Uasherati na uzinzi (zinaa)(1Kor5:1-8) *(Sexual immorality defiles the church)* | Paulo alielezwa juu ya hali ya zinaa ndani ya kanisa kama ya watu wasio mjua Mungu kabisa (1kor 5:1) lakini pia bado kama kanisa ilionekana kama ni jambo la kawaida (1kor 5:2), jambo ambalo pia Bwana alilikataza kufanyika tangu mwanzo (Kumb 22:30). |
| | | Paulo kaandika kukazia uzinzi hautakiwi ndani ya kanisa maana kuilea dhambi mwisho huenea kabisa na kusababisha madhara makubwa (*amechukulia mfano wa chachu yaweza chashusha donge zima*). Aliona ni bora mtu wa zinaa aondolewe ndani ya kanisa maana hulichafua kanisa na kuzuia wengine wasioamini kuja kwa Yesu (1kor 5:9-13)<br>Anasisitiza kuitunza miili yetu maana ni hekalu la Roho Mtakatifu, sasa pale mtu anapofanya zinaa kwanza anaunganika na kahaba na kua mwili mmoja naye, pili analichafua hekalu la Roho Mtakatifu na tatu anaharibu uhusiano na Bwana. (1kor 6:15-20). Miili hii siyo yetu bali ni ya Bwana ni mali yake hivyo tumtukuze kwa hii.<br>Mara zote mazingira na hali ya kijiografia huathili sana maisha ya kiroho ya mwamini/kanisa. Mfano kama maeno kuna uzinzi mkubwa, wizi, anasa, majivuno nk, yote hayo huharibu maisha ya kiroho ya mwamini. Tabia hizo kwakua zipo katika mazingira ya kila siku huingia ndani ya moyo wa mwamini taratibu taratibu hata mtu kujikuta naye huyafanya hayo bila kua na habari. Hivyo kama kanisa lapaswa kuwa makini sana na hali ya mzingira yake. Yesu anataka uaminifu katika maisha yetu yote haijalishi ni mambo gani yanayotendea katika jamii inayotuzunguka. |
| 02 | Migogoro ya ndoa (1 Kor 7:1-40) *(Principles for marriage)* | Inaonekana kulikuwa na migogoro katika ndoa hata kufikia hatua ya kupeana talaka. Paulo anawataka wanandoa kuwa waaminifu katika ndoa zao na kutotalakiana na kuachana. Pia kaeleza maelekezo mengine mengi yanayo husu ndoa na wanandoa. (1kor |

| | | |
|---|---|---|
| | | 7:1-40) Kwasababu ya zinaa ni afadhali kila mtu aoe awe na mke wake mwenyewe. Na ukioa usimwache mke wako bali umpende na umtimizie mahitaji yake yote. |
| 03 | Mgawanyiko kati ya wenye uwezo na wasio nao. (1 Kor 11:20-22) *(social distinctions between rich and poor)* | Kwa kukosekana kwa upendo kulikuwa na matabaka ya wenye uwezo na wasio na uwezo, Paulo kaagiza kuwa kanisa ni mali ya Mungu na liheshimiwe, upendo kati ya ndugu na udumu, (1kor 11:22; 13:4-7) |

***NB***: Yapo mambo mengi yaliyokuwa yanatendeka kwa wayahudi kama ishara ndani ya jamii zao kama kuosha miguu (*footwashing*), kufunika kichwa kwa wake (*head covering for wives*), busu (*kiss*). Paulo katika kuhitimisha kwake (1kor 16:20) kawaagiza wakorintho wasalimiane kwa busu takatifu, swali; *Je, nasi tunatakiwa kusalimiana kwa busu takatifu?* Busu lilikuwa ni ishara ya salamu hasa kwa ndugu au rafiki wa karibu (Math 26:49-50) katika jamii ya kiyahudi kipindi cha karne ya kwanza. Kwa jamii zetu salamu ya busu haitakiwi ili mbadala wake tunaweza kufanya ishara ya kupeana mikono (*handshake*), kukumbatiana (*hug*) au kuinama (*bow*) ili kutunza utakatifu, heshima ya umri na kijinsia. Kama mila na taratibu za jamii zetu ambazo hazikinzani na Biblia (Neno la Mungu) pia zaweza kufuatwa lakini pale zinapo kwenda kinyume na Neno zisifanyike kwa waamini.

*Mambo muhimu katika kitabu hiki;*

1. *Kanisa ni hekalu la Roho Mtakatifu. Hivyo, watu wanaoliunda kanisa wanapaswa kufanya kazi kwa Umoja kwa kujengana kila mmoja (1kor 1:10-4:21 hasa 3:10-16; 14:12)*
2. *Wakristo wanatakiwa kulijenga kanisa katika namna nne zifuatazo:*
   a. *Kuwa makini na wale wenye Imani ambazo nyepesi kuvunjika (1kor 8:1-9:18; 10:28, 33)*
   b. *Kwa kuwavuta wasio waamini (ambao hawajaokoka) katika wokovu (1kor 9:19-23; 10:27, 32-33)*
   c. *Kuendesha ibada kwa namna ambayo itawavuta wasio amini ili kuamini (1kor 14:16, 23-25)*
   d. *Katika ibada za pamoja wakristo wanatakiwa kutumia karama za roho sio kwa kujivunia kuwa nayo au kwa kushindana nani anayo*

*bora zaid ya mwingine, bali ni kwa kulijenga kanisa (1kor 11:2-16; 12:12-30; 14:1-35)*

3. *Muunganiko wa kijinsia kati ya mwanaume na mwanamke (ndoa) unatakiwa uwe ni ndani waamini katika Kristo. Tendo la ndoa lapaswa kuwa kwa wanandoa pekee. (1kor 5:1-13; 6:12-20; 7:5, 9, 36)*

4. *Ubatizo na meza ya Bwana ni muhimu (Baptism and Lord's Supper). Bado yote hayo si muhimu zaidi ya mtu kuamini Injili na kuishi sheria za Mungu (1kor 1:14-17; 10:1-5; 11:17-34; 15:29-34)*

5. *Ufufuo wa Yesu (pamoja na wamwamio) kutoka katika wafu ndio kiini muhimu chwa Imani ya Kikristo. (1kor 6:14; 15:1-58)*

***Love*. The main way unity of faith will be seen is throught love (1Cor 8:1; 13:1-14:1; 16:14)**

# KITABU CHA WAGALATIA

## MWANDISHI

## PAUL.

Wasomi kwa ujumla wanakubaliana kwamba barua hii iliandikwa na mtume Paul (wagalatia 1:1)

## HISTORIA FUPI YA MWANDISHI

**(Short history of Paul)**

## MAHALI ALIPOZALIWA MWANDISHI

Paulo ( ni kirumi) alijulikana kwa muda mrefu kama Sauli wa Tarso  Sauli ni kiunani alikuwa amezaliwa katika familia ya kiyahudi katika mji uitwao Tarso ya kirikia (Mdo 21:39) mji wa Tarso kwa sasa unapatikana Uturuki.

## ELIMU YAKE

Alikuwa msomi wa chuo cha Hillel chini ya mwalimu maarufu Gamalieli (Mdo 22:3) katika masomo yake alikomaa saana katika Dini ya Wayahudi  na Torati na alikuwa ni Mfarisayo mwenye elimu (Mdo 23:6)

## KABILA LAKE

Hakuwa Myahudi tu lakini kwa Ushahidi wake alikuwa ni Mfarisayo mwana wa Farisayo (Mdo 23:6) Mwebrania kutoka katika kabila la Benjamini ( Wafilipi 3:4-5)

## KAZI YAKE

Aikuwa anafanya kazi ya kutengeneza na kuuza Mahema wakati wa ujana wake (Mdo18:3)

## HALI YA FAMILIA

Alikuwa mjumbe wa baraza la Sanhedrin ndio maana tunaamini kuwa Paulo alikuwa na mke na Watoto kwa vile sifa za mtu kuwa mjumbe wa baraza hilo lazima awe na elimu na aijuwe Torati na awe na mke na ndoa hiyo lazima iwe na watoto.

## UPINZANI WA PAULO KWA KANISA

Shauku yake kama kijana Myahudi wa dini alikuwa ameelekeza nguvu zake katika kulitesa kanisa kama Mfarisayo kijana (Mdo 26:4-5) aliidhinisha kifo cha Stephano kwa kupigwa mawe (Mdo 7:58-83) katika hali ya kuendelea kupinga ukristo akizani yuko sahihi alikuwa akiwatesa wanaume na wanawake waliomwamini kristo akiwachukulia kuma waasi wa dini ya Mafarisayo na Torati alitesa kanisa akishirikiana na makuhani (Mdo26:10-11), (Wagalatia 1:13)

## KUBADILIKA KWA PAULO

Kadiri alivyozidi kuharibu kanisa la kristo ikiwa mwaka wa 33 -35 alipokuwa akienda Damaski

Kwa kusudi la kuwakamata na kuwafunga wakristo Yesu mwenyewe alimtokea na kumwambia asilitese tena kanisa bali akaeneze Injili katika Mataifa ( Mdo 9:1-19), Wagalitia 1:16) Paulo alibadilika na aliweza kuwa mjumbe nzuri wa Injili katika Mataifa. ( 1Wakoritho 9:22)

## MATUKIO MUHIMU KATIKA MAISHA YA PAULO

| MWAKA | TUKIO | MAANDIKO |
|---|---|---|
| 33BK | Kuokoka kwa Sauli wa Tarso | (Mdo 9:22-26)<br>(Wagalatia 1:13-16 |
| 33-35 | Safari ya Kwenda Dameski | (Mdo 9: 10-29)<br>(Wagalatia 1:15-20) |
| 45BK | Barnaba amfuatA Paulo Tarso ili amsaidie huduma pale Antokia ya shamu | (Mdo 1:25-26) |

| | | |
|---|---|---|
| 46BK | Sauli kuja Yerusalem mara ya pili | (Mdo 11;27-30),<br>(Wagalatia 2:1-10) |
| 47BK | Safari ya kwanza ya kimisheni | (Mdo 13:14) |
| 49BK | Aliandika waraka huu wa Wagalatia akiwa pale Antokia ya shamu | (Mdo 14:280,<br>(Wagalatia 2:11-14) |
| 50-52BK | Safari yake ya pili ya kimisheni katika mwaka huo aliandika vitabu viwili Wathesalonike wa kwanza na wa pili akiwa pale Koritho<br>( Ugiliki) | (Mdo 18:11-22)<br>(Mdo 15:36 |
| 53-56BK | Safari yake ya tatu ya kimisheni akiwa Efeso<br>( Uturuki) aliandika Wakoritho wa kwanza alipokuwa Makidonia aliandika Wakoritho wapili na kutoka huko koritho aliandika kitabu cha Warumi | Mdo 18:23)<br>Mdo 21:14) |
| 57BK | Kukamatwa kwa Paulo akiwa yerusalemu | (Mdo 21:27) |
| 58-60BK | Kifungo cha miaka 2 Katika mji wa kaizalia | (Mado 23:31)<br>(Mdo 26:32) |
| 61-62BK | Akiwa kifungoni huko Rumi aliandika nyaraka 4 zifahamikazo kama nyaraka za gerezani yani Filemon,Wakorosai,Waefeso ,Wafilipi | (Mdo 28:30-31) |
| 62-67BK | Mtume Paulo alifunguliwa na kufanya safari kadhaa na akaandika nyaraka mbili yani Timotheo wa kwanza na Tito akiwa huko Makidonia | |
| 67-68BK | Alikamatwa tena akiwa gerezani huko Rumi Italia akaandika Timotheo wa pili kama mkono wa bye bye na waraka wake wa mwisho baada ya muda mfupi akafariki kwa kukatwa kichwa huko Italia | |

## MUDA WA KUANDIKWA

## MWAKA 49BK

Barua hii iliandikwa kwaajili ya wakristo waliokuwa Galatia ya kusini maeneo ya Asia ndogo yaani Uturuki ya leo inasadikika makanisa haya yalianzishwa mapema katika safari yake ya kwanza ya kimisheni.Barua hii iliandikwa Galatia kuhusu jimbo lote ambalo wenyeji wake na makanisa ya kusini aliyoyatembelea Paulo katika safari yake ya kwanza ya kimishemi yaani Antiokia ,Ikonio,Listra na Derbe.

## NIA NA MAKUSUDI

- Waraka huu umekuwa ukiitwa na wasomaji wengi kuwa ni "**msingi wa ukombozi wa ukristo"** ukionyesha kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo kulituacha huru na dhambi Pamoja na sheria na adhabu ya Torati (Warumi8:1-5) Paulo aliandika kitabu hiki baada ya kusikia kuwa walimu wa uwongo (Judaizers) waliwafundisha na kuwalazimisha kushika sheria za kiyahudi ili wapate ukombozi mf.kutahiriwa na kuishi katika sheria za agano la kale kama Wayahudi badala ya kuishi kwa Imani na neema katika kristo Yesu

- Pia waalimu wa sheria hawakuishia kufundisha watu injili ya uwongo bali walipinga hata utume wa Paulo ndio maana katika Waraka huu Paulo aliandika kwa ukali sana na akithibitisha utume wake na haya yote yalitokea kwa muda mfupi baada ya kumaliza kazi yake ngumu ya Umisheni huko Galatia. Walimu wa uwongo walizunguka katika maeneo yale yale kupinga Utume wake na huduma yake .

- Paulo alitaka kumuonyesha Yesu Kristo utimilivu wa sheria kwa kufufuka kwake tumehesabiwa haki bure( Wagalatia 2:20), (3:13),(4:5-6),(1:3-4) Pia kuonya na kukemea mtu au kikundi chochote kitakachofundisha Waumini kutegemea kitu chochote kupata Baraka,ulinzi n.k kwa Mungu isipokuwa kwa Imani katika Kristo Yesu basi kilaaniwe.(Wagalatia 1:7-9).

## MGAWANYIKO WA SURA ZA WAGALATIA

Wagalatia ina kurasa sita imegawanyika katika sehemu kuu tatu, sura mbili za mwanzo Paulo anatetea juu ya utume wake na ujumbe wake kwamba umekuja kwa ufunuo wa Yesu kristo. Halafu sura ya tatu na nne anaelezea kuwa tumeokolewa kwa neema kwa njia ya Imani pasipo matendo ya sheria lakini neema

siyo kwamba leseni ya kutenda dhambi Sura ya tano na sita anaonesha kwamba Wakristo tuishi kwa nguvu ya Roho Mtakatifu ili tuweze kuwa wakamilifu na kuushinda mwili

## SURA YA KWANZA NA YA PILI.

## UTETEZI JUU YA UTUME NA UJUMBE KWA PAULO.

Paulo anaanza kwa kujitambulisha na kujitetea kuwa yeye siyo Mtume wa wanadamu wala hakutumwa na mtu bali kristo Yesu (Wagalatia 1:1) pia katika mstari wa 11 anazibitisha Utume wake kwa historia fupi kujibu tuhuma za walimu wa uwongo waliokanusha utume wake na katika Sura ya pili anaelezea uhusiano wake na mitume wengine.

## SURA YA TATU NA YA NNE

## UKOMBOZI KWA NEEMA KWA NJIA YA IMANI SIO LESENI YA KUTENDA DHAMBI

Paulo anaanza kwa kuwauliza Wagalatia enyi Wgalatia msio na akili ni nani aliyewaloga (Wgalatia3:1)na kuwalaumu kwa kuacha njia ya kweli ya kuishi kwa neema kwa njia ya Imani na kufuata mafundisho ya uwongo ya sheria na taratibu za kiyahudi ambazo zinawatia utumwani akitumia Ushahidi mbalimbali kuonyesha kuwa Mungu ametuletea Wokovu kwa njia ya Imani siyo matendo ya sheria akidhibitisha kwa fact mbalimbalikama ahadi ya Ibrahimu ambayo (Wagalatia 3:15-18) mf. wa Ajili na Sara, Yakobo na Essau na pia kwa uzoefu wao wenyewe Wagalatia waliopokea kipawa cha Roho Mtakatifu pasipo sheria kwa kuamini tu ( Wagalatia 3:2-5) akithibitisha tumepata haki mbele za Mungu kwa njia ya Imani. Lkini mwandishi anaonya kuwa neema hiyo siyo kibali cha kuishi katika dhambi . (Wagalatia 3: 19-29)

## SURA YA TANO NA YA SITA

## KUISHI MAISHA MATAKATIFU KWA NGUVU YA ROHO MTAKATIFU.

Paulo anaanza kwa kuonyesha uhuru tulionao katika kristo Yesu(Wagalatia 5:2-15) wakusamehewa dhambi na kuwa huru mbali na ile sheria ya Torati siyo sababu ya kuufuata mwili bali ndio sababu ya kutenda matendo mema na kuacha maovu na kwa kuwezeshwa kwa nguvu za Roho Mtakatifu (Wagalatia 5:16-21) pia akisisitiza kuishi kwa kufuata tabia ya Rohoni yani tabia ya Mungu maana sisi tumepokea wokovu kwa neema yake hivyo imetupasa kuonesha matendo yanayo wakilisha Roho wa kristo aliondani yetu ( Wagalatia 5: 22-26) hayo yatawezekana kwa nguvu ya Roho Mtakatifu na sio juhudi makini kwa binadamu lakini tusichoke kutenda

mema maadamu tutavuna kwa wakati wake tusipozimia roho kwa hiyo kwa kadri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote neem ana hasa jamaa waaminio

# HISTORIA YA PAULO

**(Short history of Paul)**

Paulo (ni Kirumi) alikuwa anajulikana kwa muda mrefu kama Sauli wa Tarso (Sauli ni Kiyunani). Alikua amezaliwa katika familia ya Kiyahudi katika mji uitwao Tarso ya Kirikia (Mdo 21:39). Hakua Myahudi tu lakini kwa ushuhuda wake alikua ni Mfarisayo mwana wa Mfarisayo (Mdo 23:6),

Muebrania wa Waebrania (alizungumza Kiebrania ni Kiaramaiki), wa kabila ya Benjamini (Wafilipi 3:4-5), na alikua amefundishwa kufanya biashara ya mahema wakati wa ujana wake (Mdo 18:3). Wakati wa ujana wake alikuwa ameshawahi kwenda Yerusalemu na ushuhuda wake alikua amejifunza chini ya mwalimu maarufu wa Torati aitwaye Gamalieli mwalimu wa shule ya Hillel (Mdo 22:3), Katika masomo yake alikua amekomaa sana katika dini ya wayahudi na wafuasi wake wengi. (Wagalatia 1:14).

Alifahamu vizuri tamaduni za Kiyunani na kulimfanya aelewe hata vile vilivyoandikwa kwa lugha hiyo. Pia alikua raia wa Rumi kwa sababu alizaliwa chini ya utawala wa Kirumi. (Mdo 22:28).

## Hali Ya Familia Yake (*family background*)

Alikua mjumbe wa baraza la Sanhedrin, ndiyo maana tunaamini kuwa Paulo alikua na mke na watoto, kwa vile sifa za mtu kuwa mjumbe wa baraza hilo ni lazima awe na elimu na anaijua Torati, awe na mke na ndoa hiyo lazima iwe na watoto.

## Upinzani Wa Paulo Kwa Kanisa (*Saul's Persecution Against The Disciples of The Lord*)

Shauku yake kama Myahudi wa dini alikua amelekeza katika kulitesa kanisa. Kama mfarisayo kijana (Mdo 26:4-5) aliidhinisha kifo cha Stefano kwa kupigwa mawe (Mdo 7:58-83). Katika hali ya kuendelea kupinga ukristo akiwa pamoja na wanaume kwa wanawake kutoka kwa kuhani mkuu alitembea katika miji na kuriharibu kanisa la Kristo. (Mdo 26:10-11, Gal 1:13).

**Kubadilishwa Kwa Paulo (*The Conversion of Saul*)**

Kadili alivyo zidi kuriharibu kanisa la Kristo akiwa katika njia ya kwenda na Dameski kwa kusudi hilo Paulo alikutana na utukufu wa aliyefufuka Kristo, ambaye alileta mapinduzi katika maisha yake (Mdo 9:1-19; Gal 1:16). Katika sinagogi la Dameski Sauli (Paulo) alimnena Yesu kama mwokozi (Mdo 9:20, 22). Alikaa Arabia na Dameski kitambo kabla ya kwenda Yerusalemu (Mdo 9:19; Gal 1:17)

Paulo aliweza kuwa ni mmoja wa walioteuliwa kubeba ujumbe wa Bwana wa Injili kwa mataifa. (Mdo 9:15; 1Kor 9:22)

**Matukio Muhimu Katika Maisha Ya Paulo (*Major Events in the Life of the Apostle Paul*)**

| MWAKA | TUKIO | ANDIKO |
|---|---|---|
| 33 BK | Kuokoka kwa Sauli wa Tarso | Mdo 9:22-26, Gal 1:13-16 |
| 33-35 BK | Wakati huu Sauli alikua Dameski, Yerusalemu | Mdo 9:10-29, Gal 1:15-20 |
| 33 BK | Sauli alienda Tarso | Mdo 9:30 |
| 45 BK | Barnaba alimfuata Tarso ili amsaidie huduma ya pale Antiokia ya Shamu | Mdo 11:25-26 |
| 46 BK | Sauli kuja Yerusalemu mara ya pili | Mdo 11:27-30, Gal 2:1-10 |
| 47 BK | Safari ya kwanza ya kimisheni | Mdo 13 -14 |
| 49 BK | Aliandika waraka wa Wagalatia akiwa pale Antiokia ya Shamu | Mdo 14:28, Gal 2:11-14 |
| 49 BK | Kutembelea Yerusalemu mara ya tatu | Mdo 15 |
| 50-51 BK | Safari ya pili ya kimisheni | Mdo 15:36 -18:22 |
| 51-52 BK | Akiwa Korintho aliandika Waraka wa Wathesalonike wa Kwanza na wa Pili | Mdo 18:11 |
| 53-56 BK | Safari ya tatu ya kimisheni, akiwa Efeso aliandika 1Wakorintho na alipokua Makedonia, aliandika 2Wakorintho, na kutoka Korintho aliandika Warumi | Mdo 18:23 -21:14 |
| 57 BK | Kukamatwa kwa Paulo Yerusalemu | Mdo 21:27 |
| 58-60 BK | Kifungo cha miaka miwili Kaisaria | Mdo 23:31 – 26:32 |
| 60 BK | Safari ya Paulo kwenda Rumi | Mdo 27 – 28 |

| | | |
|---|---|---|
| 61–62 BK | Kifungo cha miaka miwili Rumi, aliandika nyaraka za Filemoni, Wakolosai, Waefeso, Wafilipi | Mdo 28:30-31 |
| 62-67 BK | Mtume Paulo alifungwa na kufanya safari kadha na kuandika nyaraka za 1Timotheo, Tito, akiwa Makedonia | |
| 67-68 BK | Kifungo cha mwisho cha mtume Paulo, huko Rumi na kuuawa kwake na Mfalme Nero | |

# WAEFESO

**(Kristo Utajiri Wa Mungu Kwetu)**

**Mwandishi (*Author*)**

Kama ilivyo katika mstari wa kwanza katika waraka wa gerezani Paulo ndiye anaonekana kuwa ni mwandishi, kichwa chake kimeanza "kwa waefeso" na kwa ushahidi wa saini yake Efe 6:24 **Muda Wa Kuandikwa (*Date*)**

60-61 BK

Paulo alikua ni mfungwa alipokua anandika barua hii (Efe 3:1; 4:1; 6:20). Japo wasomi wengi wanasema iliandikwa barua hii alipokua Kaisaria (Mdo 24:27) miaka ya 57-59 BK au (Rumi 28:30) miaka ya 60-62 BK, inaonyesha kuwa alikua kifungoni Rumi. Inaaminika kwamba Wafilipi, Wakolosai na Filemoni ziliandikwa pia kwa wakati mmoja (Fil 1:7; Kolo 4:10; Filemon 1:9). Kwa kuwa Waefeso haituonyeshi kuachiliwa kwa Paulo kama ilivyo katika Wafilipi 1:19-26 na Filemoni 1:22, wengi wanasadiki kwamba Waefeso iliandikwa mapema kabisa kabla ya kifungo chake huko Rumi miaka ya 60BK, alipokuwa akihifadhiwa katika nyumba aliyokuwa amekodi (Mdo 28:30), na baada ya Paulo kuachiliwa aliandika 1Timotheo na Tito na akakamatwa tena, na aliandika 2Timotheo na baadae alikufa kishujaa katika Rumi.

Wefeso, Wafilipi, Wakolosai na Filemoni hizi ni nyaraka zinazoitwa Nyaraka za Gerezani kwasababu ziliandikwa kipindi Paulo akiwa katika vifungo. Kila barua ya hizi ina kumbukumbu ya hali hii (Efe 3:1; 4:1; 6:20; Fil 1:7, 13; Kolo 4:10, 18; Filemon 1:9, 10).

## Nia Na Makusudi Ya Kuandikwa Kitabu Hiki (*Theme and Purpose*)

Katika Waefeso Paulo anaonesha siri kubwa "kanisa ambalo ni mwili wa Kristo" na Kristo kama kichwa cha kanisa na (Ef 1:22-23), waumini kama washirika wake walio barikiwa kwa kila namna ya Kiroho katika Kristo (Efe 1:3; 2:11-22).

- Kusudi la Paulo ni kutoa mtazamo kwa upana kuhusu utajiri wa Baraka zake Kristo ambaye ni kichwa cha kanisa, mwili wa Kristo (waumini).
- Kusudi la pili ni kwa waumini kujua jukumu lao, ni kushika na kutembea katika hali inayoendana na nafasi waliyopewa na Mungu katika wito wao ndani ya Kristo (Efe 1:18-23;

3:14-21; 4:1).

- Pia imeunganisha na sehemu ya vita vya Ibilisi kwa wakristo (Efe 6:10-18), kwahiyo Paulo anaandika juu ya maisha ya kiroho ya mwamini, kutembea kwao hata ustawi wao.

Neno "Kristo" katika Waefeso limeonekana mara 35, na limeonekana humu zaidi ya nyaraka zingine. Paulo anaonesha umuhimu, uthamani na utajiri ulio katika Kristo.

Kitabu cha Waefeso tunaweza kukigawa katika sehemu tatu

**1. Utajiri na ubora wa mwamini ndani ya Kristo. Efe 1**

a. Tumebarikiwa kwa Baraka zote za Rohoni. Efe 1:3
b. Tmechaguliwa kwa kigezo cha kupendwa. Efe 1:4
c. Tumefanywa watoto wa Mungu. Efe 1:5
d. Tunao msamaha wa dhambi. Efe 1:7-8
e. Tumepewa Roho Mtakatifu. Efe 1:13-14
f. Tumeketishwa juu sana pamoja na Kristo. Efe 1:20-22 n.k

**2. Mwenendo umpasao Mkristo. Efe 3:1 – 6:9**

a. Kristo akae ndani yenu kwa imani na upendo. Efe 3:17-19
b. Unyenyekevu na uvumilivu na kuchukuliana. Efe 4:1-2
c. Kutunza umoja na ushirika wa kiroho. Efe 4:3-6
d. Kuacha uongo na kumpa Ibilisi nafasi. Efe 4:25-27
e. Kumfata Mungu kama watoto wanaopendwa. Efe 5:1-2
f. Kuacha uasherati na maneno ya upuuzi. Efe 5:3-5 n.k

**3. Vita vya kiroho (*spiritual warfare*) Efe 6:12-18** Ni aina gani ya vita wakristo hupigana?

- ✓ Wakristo hupigana vita vya kiroho na wala si vya kimwili. Efe 6:12

Maadui zetu huwa ni akina nani?

- ✓ Juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya. Efe 6:12 (*against the rulers, against authorities, against the cosmic powers over this present darkness, against the spiritual forces of evil*)

Wapi vita hupiganwa?

- ✓ Vita hupiganwa katika ulimwengu wa roho. (Efe 6:12) (*in the heavenly places*)

Ni mbinu/siraha gani adui hutumia?

- ✓ Adui hutumia njia za hila. Efe 6:11 (*the schemes of the devil*)

Ni siraha gani zitumike katika kupambana na adui?

- ✓ Haki, Injili ya Amani, Imani, Wokovu na Neno la Mungu. (Efe 6:13-17) (*the whole God's armor*).

Silaha hizi ni maisha halisi ya Mkristo katika Bwana na utendaji kazi wake huambatana kwa maombi mengi. (Efe 6:18)

NB: Wakristo hatuwezi kushindana na nguvu za giza kwa nguvu zetu, kushinda kwetu kunategemea uwezo wa nguvu za Mungu utendao kazi ndani yetu (Efe 1:19) anaotupatia kwa njia ya maombi (Efe 6:18). (*Christians cannot stand on their own agaist superhuman evil powers. They must rely upon the* ***strength*** *of the Lord's* ***might*** *(Eph 1:19). He supplies this power primarily through prayer (Eph 6:18*).

# WAKOLOSAI.

Kitabu kinapata jina kutokana na watu waliopelekewa watu wa mji wa kolosai, kolosai ni mji uliokuwa chini ya dola la Rumi uliokuwa ukipatikana (Asia Ndogo) kwa sasa mji huu unapatikana Uturuki.

Ingawa mji wa Kolosai ulikuwa katika njia kuu ya kutoka shamu kwenda Efeso aionekani Paulo aliwahi kutembelea Wakolosai katika kipindi cha safari zake za injili zilizoandikwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume **(Kolosai 1:4, 2:1)**

Kolosai ilikuwa katika eneo lile la Asia ndogo ambalo Paulo alikatazwa kuhubili katika safari yake ya pili ya kueneza injili **(Matendo ya Mitume 16:6-8)**

Kanisa la Kolosai labda lilianzishwa wakati wa kuishi kwake Paulo huko Efeso wakati wa safari yake kuu ya tatu, ambapo waongofu katika Efeso waliongoza injili katika miji ya jirani **(Matendo ya Mitume 19:8-10)**

Historia inaonyesha Paulo akufika Kolosai wakati wa kuandika barua hii wala akuanzisha kanisa la Kolosai bali Epafra anaonekana kuwa mtu aliye simamia kanisa hilo na wenda ndiye aliyealianzisha **(Kolosai 1:17)**

Pia kanisa hili lilikuwa likikutana katika nyumba ya Filemoni **(Kolosai 4:9; Filemoni 1:2; Filemoni 1:10-12),** pia kwa sababu ya salamu za Paulo katika **(Kolosai 1:2)** Wakolosai iliandikwa “kwa Wakolosai.

**JINA NA MTUNZI WA KITABU:**

Kwa ushahidi wa historia ya kanisa la kwanza na wa biblia yenyewe unathibitisha kuwa Paulo ndiye mwandishi amejitaja mwenyewe katika salamu **(Kolosai 1:2)** na kwa kuwapo kwa saini yake na kwa neno lake yeye mwenyewe **(Kolosai 4:18).**

**NB: “NEEMA IWE PAMOJA NANYI NYOTE”** hii ilikuwa saini ya Paulo na alitumia katika vitabu vyake na alitumika katika vitabu vyake vyote. **(Kolosai 4:18; Filemoni 1:25; Tito 3:15; 2 Watesalonike 3:18; Efeso 6:24; Wafilipi 4:23; 1 Watesalonike 5:28; Wagalatia 6:18; 1 Timotheo 6:21; 2 Timotheo 4:22) n.k.**

**MUDA WA KUANDIKWA**

Paulo aliandika nyaraka nne zote kipindi cha kufungwa kwake kwa mara ya kwanza huko Rumi kwa kosa la kuhubili injili alikuwa ameshitakiwa na mafalisayo

wakuu wa dini kwa kuhubili habari za Yesu Kristo aliyekufa na kufufuka. Hii ina maana ya kwamba aliandika **60-61 B.K**

Katika 60-61 B.K Paulo alikuwa katika kifungo cha miaka miwili huko Rumi aliandika nyaraka nne ambazo ni Filemoni, Wakolosai, Waefeso na Wafilipi (**Matendo ya Mitume 28:30-31).**

## HISTORIA KWA UFUPI ILIYOPELEKEA EPAFRA KUMTEMBELEA PAULO GEREZANI NA PAULO KUAMUA KUANDIKA WARAKA HUU KWA WAKOLOSAI.

Mafundisho yale yalikuwa ya aina ya Unostiki, yaani aina ya falsafa iliyounganisha imani ya Kikristo na siri mbalimbali za upagani. Huko Kolosai mafundisho yale yalikuwa na alama fulani za Uyahudi, hasa kuhusu sherehe za kidini. Dini za Unostiki zilipendelea mambo ya siri na sherehe mbalimbali **(Kol 2:16, 20-21).**

Nia kubwa ya walimu wale wa uongo ilikuwa juu ya vitu walivyoviona kuwa vimekabiliana na kuwapa matatizo, kama vile wema na ubaya, roho na vitu, Mungu na wanadamu. Wao wakiamini kwamba vitu vyote ni vibaya, walidai kwamba Mungu aliyekuwa mtakatifu hakuweza kukaribia wanadamu waliokuwa wenye dhambi. Maana yake katika maoni yao ilikuwa kwamba, Yesu Kristo hakuweza kuwa Mungu na mwanadamu pia.

Kwa hiyo walifundisha kwamba, kulikuwa na viumbe vingi sana katikati ya Mungu wa wanadamu, ambavyo kwa sehemu vilikuwa roho na kwa sehemu vitu, na viumbe vile viliziba pengo lililokuwepo kati ya Mungu na wanadamu. Viumbe vile vilivyokuwa karibu zaidi na Mungu vilifanana naye sana, na vile vilivyokuwa karibu zaidi na wanadamu havikufanana na Mungu, lakini kwa pamoja vilitawala ulimwengu wote na vitu. Mtu alipaswa kuviabudu na kupata kibali hicho kama alitaka ulinzi wao dhidi ya nguvu za uovu zilizofanya kazi ulimwenguni **(Kol 2:8, 18).**

Kufuatana na mafundisho yale, Yesu Kristo alikuwa kiumbe kimoja wapo kati ya vile vilivyofanana na Mungu. Paulo aliona wazi kwamba kama maneno yale yangekuwa kweli, kifo cha Kristo hakikuweza kusafisha dhambi na kuwapeleka wanadamu kwa Mungu. Kristo hakuwa mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu. Paulo alihakikisha kwamba Yesu Kristo ni Mungu naye yuko juu ya kila kiumbe cha ulimwengu wa roho na ulimwengu wa vitu **(Kol 1:15-19;2:9).** Kwa kweli, yeye ni Mwumbaji wa vitu vyote, mwokozi wa wanadamu na mshindi juu ya nguvu zote za

uovu **(Kol 1:20-22; 2:15).** Katika yeye, Mungu alifanyika mwanadamu naye ameunganika na watu wake aliowaokoa kama vile kichwa kilivyounganika na viungo vingine vya mwili **(Kol 1:18; 2;19).**

Umoja huo baina ya Yesu na watu wake una maana sana katika maisha ya waamini. Maana yake ni kwamba, mwamini pia ana ushindi juu ya uovu, na matokeo yake, anaweza kuwa na tabia ile ile ya Kristo katika maisha yake **(Kol 3:3-5.10)**

**NIA NA MAKUSUDI.**

- ❖ Paulo alianza barua yake akishukuru kwa imani ya Wakolosai naye anaomba kwamba ukuaji wao wa Kikristo uendelee **(Kol 1:1-14).** Kisha anaonyesha lengo la

ujumbe wake, ambao ni **ukuu wa Kristo na kazi yake ya wokovu na ukweli wa msingi wa Kristo unakaa ndani yake, nao hauwezi kubadilishwa ili ufae kwa falsafa ya wanadamu (Kol 1:15-23).**
Kuna aina mbalimbali za ukweli ambazo Paulo anazifundisha kila mahali. naye anapenda waamini wote wasimame imara ndani yake **(Kol 1:24-2:5).**

- ❖ Kitabu hiki kimoja kiini chake ni kristo kama kichwa wa mamlaka na nguvu zote

**(2:10),** bwana wa uumbaji **(1:16-17)** mwanzilishi wa ukombozi **(1:20-22; 2:1315).** ni ya waumini **(1:11, 29),** mkombozi na mwisho wa waumini **(1:14, 20-22; 2:11-15),**mwenye mamlaka **(1:15,19; 2:9),** Muumbaji wa vitu vyote **(1:16-17),** kichwa cha kanisa **(1:18),** Mungu mwanadamu aliyefufuka **(1:18; 3:1),** na mwokozi wa yote **(1:28; 2:3, 20:3 3:1-4)**

kupinga mafundisho ya uongo ya sheria ya kidini pamoja na falsafa yaletayo utumwa na mzigo kwa waamini **(Wakolosai 2:4-3:4), (Wakolosai 2:4-5,2:11)** na yanapingana na neema, uhuru na ukweli ya kristo

**MGAWANYIKO WA KITABU**

Kutokana na ujumbe wake mkuu wa kitabu kuwa yesu, hivyo kimgawanyiko kutokana na kweli kuu za yesu na fundisho kuu: kimegawanyika sehemu mbili

1. **YESU NI BWANA WA UUMBAJI NA MWOKOZI WA WANADAMU NA MWENYE NGUVU NA MAMLAKA JUU YA UUMBAJI WOTE: (WAKOLOSAI SULA 1-2)**

Baada ya salamu tu anaeleza ukweli kuu ya Yesu Kristo kama muumbaji na mwenye mamlaka akithibitisha kuwa yesu ni Mungu na mwokozi akipinga mafundisho yote yanayo kataa uungu wa Yesu akiwasii kudumu katika kweli hii (Wakolosai 1:15-23)

### 2. YESU BWANA WA NEEMA NA NGUVU YA MAISHA MAPYA TUMAINI LA UZIMA KWA KILA AAMINIYE (WAKOLOSAI SULA YA 3-4)

Katika sehemu hii mwandishi anaonyesha mwenendo mpya unao tokana na imani katika neema ya Yesu Kristo ambao ndio msingi wa kutenda matendo mema uletao matumaini katika Yesu Kristo na sio taratibu za kidini, dhehebu, falsafa, ustaalabu wa jamii bali neema ya Yesu Kristo ndio nguvu ya kila aaminio akionya kua mafundisho ya uongo huleta mzigo, masumbufu, uzia kwa waamini furaha ya kweli katika Yesu Kristo.

Tuhitimishe Kwa kusema biblia ni kitabu kilichobeba ujumbe mmoja ambaye ni masihi Yesu Kristo na ndio kitu muhimu Kwa asomaye na kuelewa vizuri, yeyote aaminiye atapokea  uzima wa milele ambao Mungu alituahidia kuanzia mwanzo hadi ufunuo.

***NB: "WAKRISTO HATUWEZI KUSHINDANA NA NGUVU ZA GIZA KWA NGUVU ZETU, KUSHINDA KWETU KUNATEGEMEA UWEZO WA NGUVU ZA MUNGU UTENDAO KAZI NDANI YETU ANAOTUPATIA KWA NJIA YA MAOMBI".***

# WATHESALONIKE WA KWANZA

(Kristo: Ahadi ya Mungu kwetu)

### MTUNZI NA JINA LA KITABU:

Kama ilivyoelezwa katika 1:1 na 2:18, Paulo ndiye mwandishi wa 1 Wathesalonike na kitabu kinapata jina lake kutokana na  watu na sehemu walikopelekewa ujumbe huu mji wa Thesalonike, ni mji unaopatikana bala la ulaya nchi ya ugiriki upande wa kaskazini.

**MUDA WA KUANDIKWA:**

**51-52 B.K** ilikuwa ni kipindi cha safari yake ya pili ya kimisheni katika bala la ulaya

- Paulo alikuwa amelazimika kukimbia thesalonike baada ya wiki 3 tu za utume alizofanya huko thesalaonike (**(Matendo 17:1-12).**

- Hivyo aliogopa kwamba uwenda dhuruma na ushawishi wa Wayahudi ungewakatisha tamaa wanafunzi wake lakini Timotheo walipofika Korintho toka Thesalonike walimpa ripoti Paulo kuhusu hali ya kanisa la kule Thesalonike na kumwondolea wasiwasi kuwa kanisa hilo changa lilikuwa linaendelea vizuri katika imani yao **(1Thes 5:7)** isipokuwa hawakuelewa vizuri mambo fulani hasa ufufuo na ujio wa Yesu Kristo mara ya pili.

- Hapo Paulo akawaandikia kwa furaha barua hii **(1Thes 7:9)** tuliyonayo mpaka leo ikiwaimiza na kuwaelimisha zaidi kuhusu mambo ya mwisho na ni barua tulivu na ya kirafiki ingawa inatoa maonyo upande wa maadili **(1Thes 1:1-3:13;4:13-17;5:1-11;5:16-28).**

**MAHALI MWANDISHI ALIPOKUWA**

Barua mbili kwa Wathesalonike ziliandikwa kutokea Korintho, baada ya miezi kumi na nane (mwaka mmoja na miezi sita) **(Mdo 18:1-11)** tangu alipofukuzwa kutoka huko Thesalonike. **(Mdo 17:4-10)**

Mtume Paulo alipokuwa akiishi huko Korinthoali andika barua ya kwanza mapema kipindi hicho baada ya Timotheo kuwa amerudi kutoka Thesalonike akiwa na taarifa za kanisa **(1Thes 3:5-7)** na barua ya pili ilitumwa baada ya majuma machache (au miezi michache). Hivyo barua hizi mbili zinakadiliwa kuandikwa kati ya mwaka **51-52 B.K**

**NIA NA MAKUSUDI.**

Paulo ndiye aliyekuwa Thesalonike kwa kipindi cha majuma matatu **(Md 17:1-12),** na hivyo uwenda hakuwa amewafundisha kwa muda wa kutosha. Kwahiyo kusudi la waraka huu kwa Wathesalonike unaweza kufupishwa kama ifuatavyo.

- Alikuwa akishukuru kwa kile Mungu anachotenda kwa maisha ya Wathesalonike **(1:1-12).**
- Alikuwa akiwatakia na kuwatahadharisha na maneno yaliyokuwa yakidhoofisha huduma yake **(2:1-12).**

- ❖ Alikuwa akiwataka waimarike katika mateso na hata msongamano ili wasije wakarudia upagani wao **(3:2-3; 4:1-12).**
- ❖ kujibu maswali na kufundisha maisha ya mkristo baada ya kufa **(4:1-13).**
- ❖ kujibu maswali kuhusiana na " siku ya Bwana" **(5:1-11),.**
- ❖ alikuwa akihusika na matatizo yaliyokuwa yakiinuka katika maisha yao kama kanisa **(5:12-13, 19-20).**

**MGAWANYIKO WA SURA KITABU CHA WATESALONIKE.**

Kitabu cha wathesalonike kina kurasa tano (5)

1. **ALIKUWA AKISHUKURU KWA KILE MUNGU ANACHOTENDA KWA MAISHA YA WATHESALONIKE** (sura ya kwanza hadi ya tatu)

    - ❖ Katika sura hizi tatu paulo anamshukuru mungu na kuonyesha furaha yake kwa kinsi wathesalonike wanavyoendelea vizuri na kusimama katika Imani **(1Thes 1:2-10),** akiwakumbusha jinsi akivyoenenda akiwa kwao **(1Thes 2:1-13),** na kuonyesha furaha yake ya kutaka kuwatembelea tena **(1Thes 2:17-20)** na jinsi alivyofurahi baada ya kupata ripoti yao kutoka kwa Timotheo **(1Thes 3:5-7).**

2. **ALIKUWA AKIWATAKA WAIMARIKE NA KUWATIA MOYO KATIKA MATESO ILI WASIJE WAKARUDIA UPAGANI WAO (**waishi maisha ya kumpendeza Mungu).
    - ❖ Paulo anawakumbusha na kuhimiza kudumu katika maagizo ya Bwana wetu Yesu Kristo maana hayo ndiyo mapenzi ya Mungu kutakaswa kwenu, mwepukane na uasherati; kila mmoja wenu ajue kuuweza mwili wake katika utakatifu na heshima; si katika hali ya tamaa mbaya, kama mataifa yasiyomjua Mungu **(1Thes 4:1-15).**

***(Christian should live of completely holiness (4:9))***

3. **KUJIBU MASWALI NA KUFUNDISHA MAISHA YA MKRISTO BAADA YA KUFA (5:1-28).**
    - ❖ Paulo anaeleza juu ya siku za mwisho na kuwatoa wasiwasi wanafunzi wake kuja kwa kristo ambako kumetajwa katika sura ya tano Kristo anaoneshwa kama tumaini la waaminio katika wokovu: sasa, na hata atakapokuja atatuokoa na ghadhabu kama kumbukumbu ya mateso **(1:10; 5:4-11),** na atatupa tuzo **(2:19),** atatuimarisha **(3:13),** atatufufua **(4:13-18),** kututakasa wale wote waliokuwa wakimtumaini **(5:23).**

# WATHESALONIKE WA PILI

**(Kristo: Zawadi ya Mungu kwetu)**

## MTUNZI NA JINA LA KITABU:

Kama ilivyo katika 1 Wathesalonike, barua hii pia imeandikwa na Paulo **(2 Wathesalonike 1:1; 3:17).**

## MUDA WA KUANDIKWA:

51-52 B.K.

Kwa sababu historia zinalingana na ile ya 1 Wathesalonike na uamini kwamba haikuandikwa mbali sana baada ya barua ya kwanza, labda baada ya miezi sita.

Kwa kuwa hali ya kanisa ilikuwa ni sawa, hivyo, hata mateso yalionekana kuongezeka **(1:4-5),** hii pamoja na sababu zingine zilimfanya Paulo aandike barua hii akiwa Korintho **1 au 52 B.K**.  baada ya Sila na Timotheo wabebaji wa barua ya kwanza na walikuwa wamerudi tena na habari mpya za maendeleo.

## NIA NA MAKUSUDI:

Wathesalinike wa pili ina makusudi matatu ya maendeleo ambayo Paulo aliyasikia

1. Habari za mateso waliyokuwa wakikabiliana nayo **(1:4-5).**

2. Taarifa ya barua ya uongo ya Paulo na upotofu mwingine wa mafundisho ya Paulo kuhusiana na "siku ya Bwana" **(2:1f),**

3. Njia ambayo wengine walikuwa wakiamini kutokana na kurudi kwa Bwana. Imani hii ilitumika vibaya kwani hawakujishughulisha na kazi yoyote, hivyo, Paulo akaandika ili kuwahimiza na kukemea uvivu huo uliokuwa unaendelea kukomaa **(3:5-15).**

Ili kutoshereza mahitaji yaliyo katika waraka huu, Paulo aliandika waraka huu ili awafariji na kuwasahihisha  Kwa kufanya hivi aliandika mambo matatu: (3)

1. Alikuwa akiwaeleza zawadi na adhabu ambayo itatokea mbeleni katika hukumu ya Mungu **(1:3-10);**
2. Kufafanua matukio yanayohusiana na siku ya Bwana ili kukomesha uongo ya kwamba siku imekwisha wadia **(2:1-2);**
3. Kutoa maelekezo ya ndani ambayo kanisa lilipaswa liyatende ili kuwakosoa waliokuwa wakipinga kufanya kazi **(3:6-15).**

**HIVYO WATHESALONIKE IMEGAWANYIKA KATIKA SEHEMU TATU.**

1. **ALIKUWA AKIWAELEZA ZAWADI NA ADHABU AMBAYO ITATOKEA MBELENI KATIKA HUKUMU YA MUNGU** (Kuwatia moyo walio amini) ;( *sura ya kwanza).*
   - ❖ Mwandishi anawatia moyo walioamini kuendelea katika imani hiyo na kuwa wavumilivu na kuchukulia mateso hayo ndio ishara hasa ya hukumu iliyo haki ya Mungu, ili mhesabiwe kuwa mwastahili kuuingia ufalme wa Mungu, ambao kwa ajili yake mnateswa, kwa kuwa ni haki mbele za Mungu kuwalipa mateso wale wawatesao ninyi; na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi wakati wa kufunuliwa kwake bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake**. (2 Thes 1:5-8)**

**2. KUFAFANUA MATUKIO YANAYOHUSIANA NA SIKU YA BWANA ILI KUKOMESHA UONGO YA KWAMBA SIKU IMEKWISHA WADIA (2:1-17);**

- ❖ Mwandishi anajibu hoja za kuja mara ya pili huku akiwataka wasifazaishwe upesi hata kuiacha nia yao, wala msisitushwe, kwa roho, wala kwa neno, wala kwa waraka unaodhaniwa kuwa ni wetu, kana kwamba siku ya bwana imekwisha kuwapo.

Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yoyote; maana haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu **(2 Thes 2:3-4)** na kuwakumbusha kuwa ile siri ya kuasi yatenda kazi mpaka sasa lakini yupo azuiae ambaye ni roho mtakatifu kupitia kanisa **(2Thes 2:7).**

Kusudi la sura hii 2 ni kurudi kwa Kristo katika hukumu utakapowekwa chini uasi wote na kuleta kuhukumu na pili ni kumwonesha Kristo hukumu ijayo.
***(Jesus death and resurrection a basis for the Christian hope)***

2. **KUHIMIZA WAAMINI KUFANYA KAZI KWA AJILI YA MAHITAJI YA KIUCHUMI WASIJIFICHE KWENYE HUDUMA.**
   - ❖ Mwandishi aliwakemea vikali wale walioacha kazi na wavivu wasio na shughuli za kiuchumi bali wamejificha kwenye huduma wakikwepa majukumu yao ya kujenga uchumi wao kwa mahitaji yao na akisisitiza ya kuwa asiyefanya kazi na asile.(ki ufupi huduma sio ujasiliamali wala kanisa sio kampuni) **(2 Thes3:6-12).**

Pia aliwaagiza na kuwaonya katika Bwana Yesu watende kazi kwa utulivu na kula chakula chao wenyewe, lakini ninyi ndugu msikate tamaa katika kutenda mema. **(2Thes 3:12-13).**

***(Christians must not take advantage of the charity of fellow Christians (3:6-15)***
***(Christian must never ignore their responsibility to work)***

# MIKA

**(NI NANI KAMA MUNGU)**

**MWANDISHI NA JINA LAKITABU:**

Kitabu kimepata jina lake toka kwa mwandishi wake Nabii Mika. Ni kidogo sana

Kinachojulikana kuhusu mwandishi huyu zaidi ya kile ambacho unaweza kujifunza kutoka katika kitabu hiki na katika **(Yeremia 26:18).**

Jina la Mika limefupishwa toka katika jina la Mikaya linalo maanisha kwamba ni nani kama wewe Yehwe na Mika ameandika ukweli huu katika **(Mika 7:18)** aliposema *"nani Mungu kama wewe"*

Kwahiyo kitabu cha mika kimeandikwa na mika mwenyewe kwa ushaidi wa mwandishi anajitaja mwenyewe (Mika 1:1).

Mika alikuwa anatokea Moresheth (Mika 1:10) linganisha na (1:14) mji wa Yudea kama maili 25 Kusini Magharibi kwa Yerusalemu karibu na mji wa Wafilisiti Gatha. Moresheth ilikuwa katika Milima ya rutuba ya Yuda karibu na kaishi mji wa biashara ya Kimataifa.

**MUDA WA KUANDIKWA:**
**700:K.K**

Nabii mika alihudumu muda mmoja Isaya  kwa ushaidi**(Mika 1:1 na Isaya 1:1)** na Inahisiwa Mika wenda alikua mwanafunzi wa Isaya **(Isaya 8:18)**

Mika anatueleza katika mstari wa 1 kwamba alitabiri kipindi cha Yothamu **(750-732 K.K)** Ahazi **(736716 K.K)** na Heaekia **(716-687 K.K.)** Mika alikuwa akizungumza na Yuda lakini wakati huo huo alizungumza na Ufalme wa Kaskazini wa Israeli na akatabiri kuanguka kwa Samaria (1:6) sehemu nzuri ya huduma yake ilitokea kabla ya mateka wa Assiria 722 K.K yamkini kati ya 700 K.K.

**NIA NA MAKUSUDI:**

1. Mika anaonesha jinsi watu walivyoshindwa kuishi katika hali ya Agano ambalo Mungu amelifanya na Israel ambalo kulikuwa na Baraka kama wangetii **(Kumbukumbu la Torati 28: 1-14),** na laana kama wasingetii na halafu kuondolewa katika nchi ya ahadi **(Kumbukumbu la Torati 28:15-68).**

Katika kuendelea Mika anaonesha kwamba Islaeri ilipokea adhabu kutokana na makosa yao ya kuvunja amri za torati nan a mwenendo wa matendo yao ya dhambi na kutokana na dhambi zao. Huku hii ilikua haki yao kutokana na wingi wa dhambi zao. **(Mika 1:2-16)**

2. Mika anaonyesha jinsi Mungu alivyo wa rehema na upendo na alivyo mvumilivu kwa watu na kutaka kuwasamehe maovu yao **(Mika 7:18-20)** kwa njia ya rehema zake mwenyewe na kuwaletea ukombozi wa kudumu **(Mika 6:6-8)** kwa Mungu alivyo wa upendo anatangaza kuwasaheme na kuahidi kumleta yesu kristo kwa ajiri ya dhambi zao **(Mika 5:1-6 na Mathayo 2:1-6).**
    - Kwa kifupi kitabu cha Mika kinaonyesha hukumu ya mateso waliyopaswa kupata wa Islaeri kwa ajili ya makosa yao lakini Mungu aonyesha rehema na upendo wake wa kutaka kuwasamehe watu wake.

      Hivyo kitabu kinaanza na kuonyesha hukumu ya mateso ambao ni mshahara wa dhambi **(Mika 1:2-16)** na kina maliza msamaha na rehema na ahadi ya kumleta Yesu kristo kama kipawa cha rehema ya Mungu.

Kitabu kinamaliza na maneno ya matumaini Mungu Yule Yule aliyeghadhibika ni Mungu Yule Yule atakae turehemu. **"*Ni nani aliye Mungu kama wewe mwenye kusamehe uovu na kuliachilia kosa la watu urithi wake waliosalia hashiki hasira yake milele kwa maana yeye hufurahia Rehema*" (7:18).**

Mwandishi anastahajabu wema wa Mungu na kuahidi kuwa yeye mwandishi Nabii Mika anasema, "Lakini mimi nitamtazama Bwana nitamngojea Mungu wa Wokovu wangu Mungu wangu atanisikia" **(Mika 7:7).**

***For the wages of sin is death; but the gift of God is eternal life through Jesus Christ our Lord***

**MWONEKANO WA YESU KRISTO KATIKA MIKA:**

Agano la kale aliye ubiri yesu kristo kwa ahadi kwa njia nyingi kwa ahadi, mafumbo, lugha ya picha na mifano. Hivyo hata Mika alimuhubiri Kristo kwa njia hii ya mafumbo na Lugha ya picha

Mika amwonyesha Yesu Kristo kama Mungu wa Yakobo **(Mika 4:2),** Muhukumu wa Ulimwengu **(Mika 4:3)** na mtawala atakayezaliwa katika mji wa Bethelemu **(Mika 5:2)** linganisha. Mathayo 2:1-6). Makuhani walimnukuu

Mika 5:2 kujibu swali la Herode la mahali atakapozaliwa Masihi.

Mungu wa rehema na upendo. **(Mika 6:8).**

# KITABU CHA WAEBRANIA

**MWANDISHI.**

Mwandishi wa kitabu hiki hajulikani wala hajajitaja ndani ya kitabu ila pengine inawezekana Paul, Barnaba, luka, Apolo.

Lakini anapewa nafasi kubwa kati ya wote Mtume Paulo kuna sababu 3 zinazotufanya tuhisi kuwa ni mtume Paulo ndie mwandishi.

1. **SIGNATURE/SAHIHI YA PAULO.**

   Inayoonekana katika kitabu hiki (Waebrania 13:25) neema na iwe nanyi nyote. Maneno haya yamejitohoza katika vitabu vya Paulo na alikuwa akiyatumia kama sahihi yote mfano Tito 3:15, Wakolosai 4:18, 2 Timotheo 4:22, 1 Timotheo 6:21, Filemoni 1:25, Galatia 6:18, 2 Wathesalonike 3:18, 1 Wathesalonike 5:28 kwa ushahidi huu tunaisi kuwa mwandishi ni Paulo na sio hao wengine.

2. **WRITTING STYLE/ JINSI AU AINA YA UANDISHI**

   Mwandishi anaonekana alikuwa analifahamu sana agano la kale pamoja na historia na tamaduni za wayahudi.

   Mwandishi anaonekana akitumia vizuri agano la kale kuwavuta watu kwa Yesu, mwandishi ananukuu mistari zaidi ya 60 kutoka katika agano la kale yaani zaburi mara 24, vitabu vya Musa yaani *(Mwanzo, Kutoka, Lawi , kumbukumbu la Torati, na Hesabu)* mara 23 na 1 Samwel mara moja na nukuu nyingine kutoka katika vitabu vya historia na manabi

   Ifatayo ni mifano na nukuu za kutoka agano la kale alizotumia mwandishi

| Na. | Waebrania | Agano la Kale |
|---|---|---|
| 1 | Waebrania 1:7 | Imenukulika toka zaburi 104:4 |
| 2 | Waebrania 1:8-9 | Imenukuliwa toka zaburi 45:6-7 |
| 3 | Waebrania 1:10-12 | Imenukuliwa toka Zaburi 102:25-27 |
| 4 | Waebrania 1:13 | Imenukuliwa toka Zaburi 110:1 |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | Waebrania 2:6-8 | Imenukuliwa toka Zaburi 8:4-6 |
| 6 | Waebrania 2:12 | Imenukuliwa toka Zaburi 22:22 |
| 7 | Waebrania 3:8 | Imenukuliwa toka Zaburi 95:8-11 |
| 8 | Waebrania 4:4 | Imenukuliwa toka Mwanzo 2:2 |
| 9 | Waebrania 6:13 | Imenukuliwa toka Mwanzo 22:16-17 |
| | Waebrania 13:5 | Imenukuliwa toka Yosua 1:5 |
| | Waebrania 13:5 | Imenukuliwa toka Torati 31:6-8 |

Kwa ushaidi wa uandishi huu wa uandishi unafanana sana na uandishi wa kitabu cha Rumi na Galatia ambavyo ameandika Paulo na kwa kipindi hicho Paulo alikuwa ni mmoja ya watu waliofahamu sana Torati na Agano la kale hivyo tunampa nafasi kubwa wenda akawa ndiye mwandishi wa kitabu hiki cha Waebrania.

3. **MWANDISHI ALIKUWA ANAMFAHAMU TIMOTHEO (WAEBRANIA 13:23)**

   Kwa kule kutaja habari za Timotheo kama mtu anayefahamiana naye kunatufanya kuhisi ni Paulo kwa sababu Paulo ndiye alikuwa akifanya kazi ya Injili pamoja na Timotheo katika maeneno mengi pia Paulo alimtambua Timotheo kama mwanawe wa kiroho kwa ushaidi huu tunaishi kuwa mwandishi ni Paulo.

   Kiufupi mwandishi ajulikani ila anaisiwa kuwa ni Mtume Paulo.

## MWAKA WA KUANDIKWA KITABU HIKI 67-68BK (BAADA YA KUZALIWA KRISTO)

Inaaminika kitabu hiki kiliandikwa wakati wa utawala wa Rumi ulipoanzisha mateso makali dhidi ya wakristo ilikuwa kabla ya kufa kwa Mtume Paulo na kabla ya kubomolewa kwa kanisa mwaka 70 BK

## LENGO KUU/MADHUMUNI/UJUMBE MKUU WA KITABU CHA WAEBRANIA.

i. Kitabu cha Waebrania kuliandikwa kwa kuwatia moyo na kujenga Imani kwa Wayaudi na kwa watu wanaoijua sana Torati ili wamuelekee Yesu Kristo kama utimilifu wa Agano la kale.

ii. Waebrania ni kitabu cha utetezi (apologetics) kina kitetea ukuu wa Yesu na ubora wa huduma ya Yesu ubora wa agano jipya ambalo Mungu amelifanya kupitia kazi ya msalaba wa Yesu ulimwengu unapata ondoleo la dhambi na upatanisho na Mungu baba kwa njia ya Imani.

**NB:** Mwandishi analenga kuwatia moyo Wakristo Waebrania wanaorudi nyuma anawasihi wamwelekee Yesu kama utimilifu wa agano la kale hivyo kitabu hiki kimegawanyika katika sehemu kuu mbili

a) UKUU WA YESU (THE FIVE GREATEST OF JESUS) SULA 1HADI 6
b) UPEKEE NA UMUHIMU WA HUDUMA YA YESU (VERY IMPORTANT AND UNIQUE OF JESUS SERVICE) SULA 7 HADI 11

## 1. UKUU WA YESU (THE FIVE GREATEST OF JESUS) SULA 1HADI 6

### i. JESUS IS GREATER THAN PROPHET (YESU NI MKUU KULIKO MANABII) Waebrania (1:1-3)

| Na. | Yesu | Manabii |
|---|---|---|
| 1 | Alizaliwa na Bikira Maria kwa uwezo wa Roho Mtakatifu (mathayo 1:18-23) | Alizaliwa kwa jinsi ya kibinadamu |
| 2 | Jina lake ni lenye nguvu na mamlaka (Matendo 3:6) | Majina yao hayana nguvu wala mamlaka (majina ya kawaida) |
| 3 | Yesu alikufa na akafufuka naye yu hai milele | Manabii hufa lakini hakuna aliyefufuka mpaka siku ya mwisho watakapofufuliwa |

### ii. JESUS IS GREAT THAN ANGELS WAEBRANIA (1:4-14), WAEBRANIA (2:5-6)

| Na. | Yesu | Malaika |
|---|---|---|
| 1 | Yesu ni Muumbaji wa vyote (Yohana 1:3), (Kolosai 1:16) | Ni viumbe vilivyoumbwa |
| 2 | Ni mkombozi wa wanadamu | Ni watumishi wa wanadamu |
| 3 | Ni mwana wa Mungu wa pekee | Ni watumishi watumika mbele |

| | | |
|---|---|---|
| | | za Mungu |
| 4 | Ni Mfalme mwenye nguvu | Wajumbe wenye nguvu |

### iii. JESUS IS GREATER THAN MOSES (MUSA) WAEBRANIA (3:1-6), YOHANA (1:17)

| Na. | Yesu | Musa |
|---|---|---|
| 1 | Ni mwana wa Mungu wa pekee (Yohana 3:16) | Mtumishi wa Mungu (Yoshua 1:2) |
| 2 | Ameleta Neema na kweli na msamaha wa dhambi | Ameleta sheria na hukumu (torati) |

### iv. JESUS IS GREATER THAN JOSHUA (YESU NI MKUU KULIKO YOSHUA) WAEBRANIA (4:1-13)

| Na | Yesu | Yoshua |
|---|---|---|
| 1 | Jemedari wa vita vya kiroho vinavyopiganwa katika ulimwengu wa roho | Jemedari wa vita vya kimwili vinavyopiganwa katika ulimwengu wa mwili |
| 2 | Hutoa pumziko la milele katika ufalme wa Mungu kwa watu wote | Hutoa pumziko la muda mfupi tu hapa duniani kwa Israeli pekee |
| 3 | Huturithisha mbingu mpya | Aliwarithisha nchi ya kaanani |

### v. JESUS IS GREATER THAN HIGH PRIEST (YESU NI MKUU KUHANI MKUU) WAEBRANIA (5-7)

| Na | Yesu | Haruni |
|---|---|---|
| 1 | Kuhani pekee aliyeshinda Mauti | Alizuiliwa na Muti (Hakuishinda) |
| 2 | Kuhani aliyetoa damu yake mwenyewe | Alitoa damu ya wanyama |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Aliingia patakatifu pa mbinguni mara moja milele | Aliingia patakatifu pa duniani mara moja kila mwaka |

## 2. UPEKEE NA UMUHIMU WA HUDUMA YA YESU (VERY IMPORTANT AND UNIQUE OF JESUS SERVICE)

Katika sehemu hii mwandishi anaelezea ubora na upekee kabisa wa huduma za Yesu ambazo aziwezi kufanywa na mtu yeyote isipokua Yesu peke yake

### i. SADAKA YA DAMU YA YESU (BLOOD SACRIFICES)

Ukweli ni kwamba damu ya Yesu peke yake ndio inaweza kuondoa dhambi zetu, kutuletea upatanisho kwa maana ikiwa damu ya mbuzi na mafahari na ndama na ngombe walinyunyiziwa wenye uchafu hazikutosha kuwaondolea dhambi.

Basi si zaidi damu yake yesu ambaye kwamba alijitoa nafsi yake mwenyewe kuwa sadaka isiyo na mawaa itusafishayo dhamiri zetu na kulipa fidia ya dhambi zetu na kuleta upatanisho kwa Mungu baba ni damu tu ya Yesu atuna damu nyingine iwezayo kufanya kazi hii kwa sababu zote zina hati na mawaa lakini damu ya Yesu ndio aina hatia wala dhambi lakini ilimwagika kwa ajili ya wenye hatia na wenye dhambi hivyo ni ya kipekee na ya muhimu (Waebrania 9:11-22).

### ii. AMEFANYIKA MJUMBE NA MZAMINI WA AGANO JIPYA

Kwa kule kufa na kufufuka kwake Yesu amefanyika mjumbe na mzamini wa agano jipya na rehema na ondoleo la dhambi, Kwa sababu hii ni mjumbe wa agano jipya ili kwa mauti yake ikiisha kufanyika kua ukombozi kwa makosa yetu yaliyokua chini ya agano la kwanza la sheria. Sasa basi kwa kile Yesu kuzamini agano hili hakuna hukumu ya adhabu juu yao kwa walio mwamini Kristo Yesu kwa sababu sheria ya uzima ulio katika kristo yesu umewadhamini na kuwaacha huru mbali na hile sheria ya dhambi na mauti.

Maana yasiyowezekana katika sheria kwa vile ilivyo dhaifu kwa sababu ya mwili Mungu kwa kumtuma mwanaye mwenyewe katika mfano wa mwili alihukumu dhambi katika mwanae ili sisi sote tuwe huru na tufumbuliwe macho yetu na kugeuzwa mioyo yetu na tuziache guvu za giza na uelekea nuru tuzishinde na nguvu za shetani na

kumtegemea Mungu wa kweli kisha tupate msamaha wa ondoleo la dhambi na urithi kama wana wa Mungu kwa njia ya Imani ya kumwamini yesu kama mzamini na mjumbe wa agano la rehema na msamaha. **(Warumi 8:1-4)**

# KITABU CHA PETRO WA KWANZA

## MWANDISHI

- Petro mwanafunzi wa Yesu aliyeshuhudia matukio mbalimbali ya maisha ya Yesu Kristo huduma yake miujiza kufa na kufufuka kwa Yesu kristo.

- Alizaliwa mwaka wa 0-1 kabla ya Kristo, aliitwa Simoni/Semioni.

- Petro alikuwa mwana wa mtu mmoja aliyeitwa Yohana (Yona) **(Mathayo 16:17, Yohana 1:42)** alikuwa myahudi aliyeishi kapenahumu kazi yake ilikuwa uvuvi pia alikuwa na familia **(Mathayo 4:17-19, Mathayo 8:14).**

- Petro alikua ni myahudi aliyeshika mafundisho ya torati lakini hakuwa na elimu wala hakusoma **(Matendo ya Mitume 4:13-14).**

- Petro anamaliza barua hii kwa kukiri jukumu la sila(silwano) aliyemsaidia kuandika barua hii **(1Petro 5:12)** na inawezekana ndiye sila(silwano) aliyeipeleka barua hii na bila shaka sila(silwano) ni yule yule aliyetajwa mara kwa mara katika **(Matendo ya Mitume 15:22, 18:5), (2korintho 1:19), (1Watesalonike 1:2-1).**

- kutoka na msaada huu wa sila(silwano) katika barua hii ni sanifu Zaidi kuliko ambavyo ingetazamiwa kutoka kwa Petro aliyekuwa mvuvi wa Galalilaya aliyekuwa hana elimu **(Matendo ya Mitume 4:13-14)**, sila(silwano) alitumia vipawa vyake kumsaidia Petro kuwasilisha ujumbe wake**(1Petro 5:12)** .

## HISTORIA YA HUDUMA YA YESU NA PETRO

- Mara ya kanza Yesu alikutana na Petro katika bonde la Yordan **(Yohana 1:28-35)** Mara baada ya muda mfupi walikutana tena Galilaya ambapo Petro alikuwa miongoni mwa waamini wa kwanza walioacha kazi yao na kumfuata Yesu.
- Baada ya muda huduma ya Yesu ilipoongezeka alichagua mitume kumi na mbili kutoka kwa wanafunzi wake wengi Petro alikuwa wa kwanza kuchaguliwa kuwa miongoni mwa mitume wawe watenda kazi pamoja na Yesu **(Mathayo 10:2)**

Alikuwa mwanafunzi mdadisi aliyependa kuuliza maswali na kujibu maswali kwa njia hii alijifunza vitu vingi **(Mathayo 15:15), (Mathayo 16:16), (Mathayo 14:28).**

- Yesu aliona uwezo wa uongozi uliokuwa ndani ya Petro akampa jina jipya Kefa (kwa kilatin Petrus lenye maana yake jiwe/mwamba **(Yohana 1:42)** na ndio maana hata leo tunamtambua Semioni kama Petro (peter) majina yote mawili yana maana moja yaani Petro na kefa katika lugha ya kiunani na kiaramiki **(Mathayo 16:18).**
- Petro alionekana ni mtu mwenye upendo mkubwa sana kwa Bwana Yesu kiasi cha kuwa tayari hata kufa, mtu mwenye Imani sana pamoja na mapungufu yake kadhaa.
- Kutokana na upendo, shahuku na bidii ya Petro aliyokuwa nayo kuna baadhi ya mambo ambayo aliyafanya Petro na Yesu na mitume wengine hawakupata kabisa nafasi ya kufanya.
    - Bwana Yesu kutumia chombo(mtumbwi/boti) wa petro katika huduma yake
    - Kutembea juu ya maji
    - Kulipiwa kodi na Bwana Yesu kwa fedha iliyotoka katika kinywa cha samaki **(Mathayo 17:24-27)**
    - Kumtambua Yesu Kristo kama mwana wa Mungu aliye hai
    - Kumkata sikio mmoja wa maaskari waliokuja kumkamata Yesu wakiwa bustanini
- Ingawa petro alifanya makosa mara nyingi kama kumkana Yesu mara 3 hadharani kwa sababu ya uwoga **(Mathayo 26:70-75).**

- Kukosa subira na kukata tamaa na kurudi kuvua samaki badala ya kusubilia ahadi ya Yesu aliyomuahidi **(Yohana 21: 1-4)**.

- Lakini hayo yote Mungu kwa upendo wake aliruhusu yampate mtumishi wake Petro ili kumjenga awe imara ma aweze kuwaimarisha wengine **(Luka 22:32)** na hatimae mtumishi wake aweze kuwa bora na mwisho wenye ukuu na utukufu zaidi **(Kumbukumbu la Torati 8:16).**

- Petro alitambua makosa yake akatubu na Yesu akamsamehe na kumuonyesha upendo na kumsaidia pia akampa heshima ya kuwa kiogozi wa kwanza wa kanisa hatimae Petro akawa na mwisho bora na ukuu zaidi kwa sababu ya rehema na upendo wa Yesu kristo kwa watu wake

**HISTORIA YA PETRO NA KANISA.**

- Yesu aonyesha upendo wake kwa wote wanaotubu na kumrejea yeye na kuwasamehe kabisa pamoja na mapungufu aliokuwa nayo Petro Yesu alimpa kazi ya kulichunga, kulilisha na kulianzisha kanisa ulimwenguni kwa neema Petro akawa kiongozi wa kwanza wa kanisa **(Yohana 21:15-17), (Mathayo 16:18).**

- Mnamo mwaka 33 BK Mungu alitimiza ahadi yake aliyoahidi katika vitabu vya manabii aliachia nguvu ya roho mtakatifu ilikuwa ni siku ya 50 tangu kufa na kufufuka kwa Yesu kristo yani Yesu alipokufa alikaa siku 40 akapaa mbinguni siku ya 10 roho mtakatifu akashuka siku **PENTECOSTAL.**

- Maana ya **PENTE COSTAL** ni muunganiko wa maneno mawili Pente maana yake 5 na Costal maana yake 10, ukizidisha 5 mara 10 unapata hamsini sawa sawa na siku hamsini alizochukua Yesu kama kufufuka kwake hadi siku ya kushuka kwa roho mtakatifu siku ya kwanza kanisa lilipozaliwa ulimwenguni.

- Mfano **PENTE GONI** maana yake ni umbo au jengo la pembe tano yaani pente 5 goni jengo.

- Mfano **PENTA TEUCH** maana yake vitabu vitano PENTE tano TEUCH vitabu, Ndio vile vitabu 5 vilivyo andikwa na Musa kwa ujumla vinaitwa **Pentateuch**

- Siku hiyo Pentecostal Petro akiwa amejaa roho mtakatifu alihubiri watu wengi sana wakaokoka **(Matendo ya Mitume 2:1-35).**

- Siku chache baadae petro aonyesha msimamo wake, uzalendo wake, upendo wake, kwa Yesu dhidi ya maadui wa ukristo (**Matendo ya Mitume 4:8-13), (Matendo ya mitume 5:18-21).**

- Kwa kuwa Petro alilelewa mila za kiyahudi aliwaona watu wengine ambao sio wayahudi kama hawana haki ya kupokea wokovu hili lilikuwa kosa lakini Mungu alimfundisha kwa upole kwa njia ya maono mjadala **(Matendo ya mitume 10:9-16)** wakati mwengine Paulo alimkemea tabia yake ya upendeleo **(wagalatia 2:11-20**)

- Baadae Petro alibadilika akaihubiri injili katika mataifa mbalimbali ikiwemo Asia ndogo yani Uturuki, korinto yaani ugiriki ya leo, baadae alienda Rumi yaani Italia.

- Petro alikufa huko Rumi kwa kuitetea na kuihubili injili mnamo mwaka **65-67 BK** kwa kumsulubisha kichwa chini miguu juu kwa amri ya mfalume Nero wa Dola ya Rumi, kwa kukataa kusurubishwa kama Yesu. Hadi leo kaburi la Petro lipo mjini Vatikani huko Italia(Roma) ambako kumejengwa jengo kubwa sana la kanisa katoliki lijulikanalo kama **Basilica ya Mtakatifu Petro.**

## TAREHE YA KUANDIKWA

Mwaka **63-64 BK** kipindi cha utawala mfalme Nero mwanzoni mwa kipindi cha mateso kabla mateso hayakuwa makali sana kama inavyonekana katika historia ya utawala wa Rumi mwandishi alitaka kuwatia moyo na kuwaonya na kuonesha neema ya Yesu Kristo kabla ya mateso hayajakuwa makali ili waendelee na imani na kujua Mungu yuko katikati yao akitimiza kusudi lake.

## MAHALI KILIPOANDIKWA NA WALIOANDIKIWA.

Petro aliandika barua hii akiwa huko Rumi yaani Itali ya leo, Petro hakuandika barua kwa kikundi maalum bali ilikuwa kwa watu wote ambao wangezunguka mingoni mwa makanisa makubwa **(1Petro1:1)** japo maeneo haya yalitajwa yako Uturuki ya leo.

Mwandishi anajitaja mahali alipokuwa Rumi akitumia jina la Babel akiufananisha mji wa Rumi na Babel ya zamani **(1Peter 5:13).**

## DHUMUNI

Yapo madhumuni mengi lakini tunaweza kuyagawa katika sehemu kuu mbili

***(1) Mwandishi anaonyesha Yesu kristo ndio tumaini letu sisi tuaminio na kumpenda Mungu wakati wa mateso majaribu na maudhi mbalimbali (1Petro:6-7)***

- Petro anatia moyo na kutuimarisha sisi tuliomuamini Yesu kuweka matumaini yetu kwa utukufu ujao kwa kumwangalia Yesu kristo wokovu wetu wa milele na kumfuata Yesu kama kielelezo kamili cha mateso ya wenye haki **(1Petro 2:21-24).**

***Those who suffer as Christian will be proven Faithfull when Christ returns.***

***(2) Wito wa kuishi maisha mtakatifu kama watumishi wa Mungu (1 Petro 2:11-25)***

- kitabu kinatutaka waamini kuishi katika ulimwengu huu kama wakazi wa muda (wageni na mabalozi wa Yesu kristo katika ulimwengu huu) **(1 Petro 1:1),(13:21),(2:11-12), (3:14),( 3:15)** na kuishi kulingana na wito wetu kama watu muhimu tuliopendwa na Mungu tukionyesha tabia njema, wema, imani, uvumilivu, upendo, uwaminifu **(1Petro2:4-12),(4:1-19)** na huku tukifundisha kweli, upendo, neema, uwaminifu na tabia za Mungu katika kristo Yesu huku tukilichunga kundi la Mungu kwa hiari sio kwa kulazimishwa au kwa kutafuta pesa ya aibu bali kwa moyo**(1 Petro 5:1-4).**

***Christian should live righteously in their home and in their society (1 Petro 2:2-11).***

# PETRO WA PILI

## MWANDISHI

**Petro**

## TAREHE YA KUANDIKWA

Inaonekana kama petro aliwandikia barua hii ijulikanayo kama walaka wa pili wa petro baada ya mwaka mmoja baada ya kuandika hule wa kwanza hivyo inasadikika iliandikwa mwaka 64-65BK

## MAHARI KILIPOANDIKIWA NA WAANDIKIWA

Inaonekana wazi kuwa petro aliwatumia barua hii kwa wale wale waliokuawamepata hile ya kwanza yaani maeneo ya asia ndogo ambayo maeneo hayo ni uturuki ya leo **(linganisha 2 petro 3:1 na 1petro 1;1 )**

## MWANDISHI ALIPOKUA

Inaonekana petro alikua gerezani lumi {italia} nae alijua atauwawa baada ya muda mfupi **(2petro1;14-15)**

## **DHUM**UNI

- Petro alindika barua hii mda mfupi aliposikia walimu wa uongo wamezunguka katika makanisa na kusababisha matatizo kutokana na mafundisho yao ya huzushi pia kuwapa taarifa waamini juu ya kifo chake ambacho kingetokea mda mfupi badae **(2petro1:14-15)**
- Petro anatumia barua hii fupi na kali sana kupinga madai ya walimu wa uongo waliodai kwamba neema ya kristo imewapa uhuru wa kutenda dhambi na makosa kama uzinzi , uwasherati, wizi na nk yasingekua kosa petro alipinga uzushi wao na kuonesha kuwa mtu anaokolewa kwa Imani ya kumuamini kristo lakini maisha yake yawe ya upendo usafi na kumchamungu (petro2:1-3) kuhusu mambo yanayolingana na barua hii soma walaka wa yuda

JINA ……………………………………………………………………………………………

## MASWALI

1: Je umejifunza nini kutokana na historia ya Petro?

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………

2. Petro na Yuda wote walikuwa wanafunzi wa Yesu na wote walimkosea Yesu kwa nini mwisho Yuda alijinyonga na Petro akawa kiongozi wa kwanza wa kanisa nini kilicho fanya Yuda kujinyonga na Petro kuwa kiongozi mzuri?.

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

(3) Unajifunza tabia gani ya Yesu kwa watu wake kutokana na historia ya Petro na Yesu?. ………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

**OUR GROUP MOTTO IS**
"WE ARE NOT BORN AGAIN TO SUFFER AGAIN".
**OR**
"WE BORN AGAIN TO LIVE AS ROYAL PRIESTHOOD"
**(1Petro 2:9-10)**

# MAFARISAYO NA MASADUKAYO

**(PHARISEES AND SADDUCEES)**

**Farisayo ni Nani?**

Farisayo ni moja ya madhehebu ya dini za Kiyahudi (Judaism) yaliyo pata nafasi sana mwaka 64 kabla ya kuzaliwa kwa Yesu madhehebu hayo yaliamini katika sheria za Musa na katika agano la kale.

Chama kingine kilikuwa cha Masadukayo vyama vile vilianzishwa karne ya pili KK ambapo ushawishi wa Kiyunani katika maisha ya Kiyahudi ulileta mafarakano kati ya wenyeji wa Uyahudi.

Mafarisayo wengi walitoka katika wafanyakazi na watu wa hali ya chini nao walijaribu kuhifadhi mapokeo ya desturi ya kiyahudi dhidi ya uharibifu wa mawazo ya kigeni na makusudi ya kisiasa. Masadukayo zaidi walikuwa watu wa hali ya juu na matajiri lengo lao kuu halikuwa kuhifadhi mapokeo bali walitaka kutumia mipango ya dini na jamii ya kiyahudi ili wapate Mamlaka ya kutawala (Ukuhani).

### Misimamo ya Kushika Sheria

Masadukayo walipokwisha pata mamlaka ya kikuhani, walizidisha makusudi yao kwa njia ya kusisitiza haja ya kutimiza sherehe za hekaluni. Kinyume chake, mafarisayo walitilia mkazo katika wajibu wa kutimiza sheria za kila sehemu ya maisha, wala si mapokeo ua hekaluni tu. Kwanjia hii Mafarisayo walipendekeza mapokeo ambayo walimu wa sheria (yaani waandishi) walitunga na kufundisha. Waandishi walikua wameongeza sheria za Musa iwe kanuni maalumu yenye mipango mingi isiyohesabika kuhusu mambo ya kushika sabato n.k (Mt 12:1-2; Mk 3:1-6; Lk 13:10-14), sherehe mbalimbali za utakaso (Mt 23:25; Mk 7: 1-9), kufunga (Lk 18:11-12), utoaji wa zaka (Mt 23:23) na kuapa viapo (Mt 23:16-22).

Wakiwa wanachama wa chama chanye kanuni kali namna hii, Mafarisayo wengi walijiona kua wao pekeyao waliku watu wa kweli wa Mungu, wakajitenga na wale wasio fuata imani na desturi zao. Jina lenyewe, Farisayo "lilikua na maana ya mtu aliejitenga" (Mdo 15:5; 26:5; Gal 2;12).

Mafarisayo walimlaumu Yesu kwakua hakushika sheria zao (Mt 12:10-14; 15:1-2; Yn 9:16), lakini Yesu aliwalaumu Mafarisayo kwa sababu wao hawakushika sheria ya Mungu. Walishughulika zaidi na kuhifadhi mapokeo yao kuliko kujenga maisha yenye tabia ambayo sheria ya Mungu ilikusudia (Mt 5:20; 15:1-10; 23:23-26), walijishughulisha na maonyesho ya nje kuliko ile tabia na nia safi ya moyoni. Walitafuta sifa ya wanadamu kuliko kumpendeza Mungu (Mt 23:2, 5, 27-28).

Lawama ya Yesu juu ya Mafarisayo iliwasababisha wamchukie. Katika hasira yao walikubali ata kushirikiana na Masadukayo (yaani makuhani ) ili wapate kumuondoa (Yn 11:47-53, 18:3) Ingawa Masadukayo walikua na mamlaka zaidi katika Sanhedrin (yaani baraza kuu la wayahudi lililomhukumu Yesu), Mafarisayo wengi pia walikua wajumbe wa baraza lile. Angalau Farisayo mmoja, Nikodemo, alikua mwamini wa Yesu (Yn 3:1; 7:45-52; 19:38-40)

### Mtazamo, Desturi na Imani Tofauti

Iwapo kushika sheria ilikuwa lengo kuu la mafarisayo, Imani nyingine za pekee zilizidisha mafarakano katika mahusiano yao na Masanduayo. Kwa mfano Mafarisayo waliamini kwamba kwa njia ya kiroho mtu anaendelea kuishi baada ya kufa kimwili, waliamini habari za ufufuo wa mwili na kuwepo kwa malaika, waliamini katika umilele wa nafsi na pia kuna dhawabu na adhabu baada ya kufa, Walikuwa mabingwa wa usawa wa binadamu, ambapo Masadukayo hawakuamini hayo yote (Mt 22:23; Mdo 23:8)

Imani ya Mafarisayo kuhusu ufufuo labda ilikuwa sababu moja kwamba wao walipendelea wakristo kidogo siku za kwanza za kanisa. Hawakukataa watu wengi sana walipo amini habari za kufufuliwa kwa Yesu iwapo Masadukayo waliwapinga Wakristo kwa hasira kubwa. Mafarisayo walionekana kama waliwaona kuwa ni wayahudi waaminifu walioshika dini vizuri na kutimiza desturi za kimsingi (Mdo 2:46-47; 4:1-2; 5:12, 17, 25-28).

Imani nyingi ya Mafarisayo ambayo pia ilikua kinyume cha imani ya Masadukayo ilikua kwamba, matukio yote yalikua chini ya uongozi na utawala wa Mungu, na wanadamu hawakua na haki ya kupingana na mambo yaliyopangwa na Mungu, kwahiyo waliona jambo la busara kama hawakuwapinga Wakristo, wasije wakapinga mambo ambayo Mungu aliyapenda (Mdo 5:34-39).

Tabia ile ya kuwavumili wakristo ilibadilika ghafla ambapo Mafarisao walielewa ushuhuda wa Stefano kuwa alisema kinyume cha sheria ya Musa. Wakati huo waligeuka kuwaudhi wakrsito kwa kauli, na kwa kweli Farisayo Sauli wa Tarso aliongoza adha ile (Mdo 6:13-14; 7:57-58; 8:3; 23:6)

Baada ya kubomolewa kwa Yerusalemu na Warumi mwaka 70 BK, Masudukayo na vyama vingine vidogo vya Kiyahudi vilififia. Jambo hili liliwaacha Mfarisayo watawale dini ya Kiyahudi peke yao. Hapakuwa na haja ya chama maalumu cha Mafarisayo tena, kwa sababu Uyahudi wote wakati ule ulifuata desturi na mapokeo ya Mafarisayo.

### Sadukayo ni Nani?

Ni miongoni mwa madhehebu/vyama viwli vyenye nguvu katika Israeli wakati wa Agano Jipya. Chanzo cha vyama vile kilikuwa katika karne ya pili KK ambapo ushawishi wa Kiyunani uliingilia katika maisha na dini ya Wayahudi.

### Mamlaka ya Kidini

Mambo mengine yaliyoaminiwa na Masadukayo yalizidisha mafarakano baina ya vile vyama viwili. Mafarisayo walifuata mapokeo mengi ya kimila na kidini, lakini Masadukayo hawakujali mapokeo hayo. Wao walitaka amri za Musa tu, yaani Torati. Hawakuamani habari za maisha ya kiroho baada ya kufa wala ufufuo kutoka kwa wafu, wala uongozi wa Mungu kabla ya kutokea mambo yenyewe wala habari za Malaika. Mambo hayo yote yaliaminiwa na Mafarisayo (Mt 2:23; Mdo 4:1-2; 23:7-8)

Ingawa Masadukayo hawakupatana na Mafarisayo, walishirikiana katika kumchukia Yesu (Mt 16:1-
4; 22:15, 23, 34)

Viongozi wengi wa makuhani wa wakati wa Agano Jipya walikuwa Masadukayo nao walisaidiwa na Wayahudi wa hali ya juu. Kuhani mkuu na mwenyekiti wa Sanhedrin (Baraza kuu la Wayahudi), alikuwa Sadukayo, na hivyo Masadukayo wenzake walipata sauti kubwa katika Sanhedrin (Mdo 4:1-
3; 5:17-21)

Masadukayo waliwachukia Wakristo wa kwanza kwa sababu mbili hasa; (1) Mitume walipolaumu Sanhedrin kuhusu kesi ya Yesu, waliwalaumu Masukayo waliyoitawala (Mdo 4:5-10; 5:27-28). (2) Ukuaji wa kanisa ulikuwa na msingi wa ufufuo ambao Masadukayo waliukataa (Mdo 4:1-2, 10, 17).
Wakati huo watu wengi hawakuwapenda Masadukayo, kwa hiyo waliogopa kutendewa mabaya kama wangewadhuru Wakristo. Ila Mafarisyo pia walipowachukia Wakristo, waliweza kutumia mamlaka yao dhidi ya Wakristo (Mdo 6:12-15; 7:58; 8:1; Fil 3:5-6)

Warumi walipobomoa Yerusalemu na hekalu mwaka wa 70 bK, Masadukayo walipoteza msingi wao wa ukuhani uliowapa nguvu. Baada ya muda mfupi chama chao kilikufa.

**Mapungufu ya Madhehebu Haya**

Masadukayo hawa japo waliamini sheria za Musa lakini bado hawakuyaelewa maandiko kuwa yalimtabiri Yesu na hivyo wao walimkataa na kumchukia na kufanya njama ya kumuua wakishirikiana na Mafarisayo. Japo madhehebu/vyama hivi viwili walikuwa ni mahasimu yaani maadui hawakupatana wao kwa wao kutokana na kupishana kwa itikadi zao lakini ilipofikia wakati wa kumuua Yesu waliungana pamoja.

Madhehebu yote haya mawili yalikuwa na mapungufu makubwa. Ni kweli walikabidhiwa Torati na walitakiwa kuwajibika kuyashika na kufundisha kama ielekezavyo Sheria ya Musa lakini wao hawakufanya hivyo. Mafarisayo walitanguliza ubinafsi na unafiki ambao Yesu aliwakemea na kuwasema hadharani (Mt 23:1-36) waliijua kweli lakini kwa kujihesabia haki, na kugeuza sehemu takatifu ya Mungu kwaajili ya manufaa yao na kutaka kupendwa na watu waliipotosha Torati kwa kuongeza mambo mengi ambayo hayakuwepo wakishirikiana na waalimu wa sheria (waandishi). Masadukayo nao waliegemea

sana kwenye siasa na kuwa vipofu kwa mambo ya kiroho. Wote hawa walikuwa kwazo kwa Yesu na kanisa la kwanza. Yesu naye aliwaonya wanafunzi wake wasifate namna ya mifano ya matendo ya mafarisayo wala masadukayo. ***"Imekuwaje hamkufahamu ya kuwa si kwa sababu ya mkate naliwaambia? Ila jilindeni na chachu ya Mafarisayo na Masadukayo. Ndipo walipofahamu ya kuwa hakuwaambia kujilinda na chachu ya mkate, bali na mafundisho ya Mafarisayo na Masadukayo. Mathayo 16:11-12"***

**Je, Dhehebu au Dini Vinaokoa?**

Hasha dhehebu au dini haiokoi maisha ya watu. Ni mashahidi wote leo hii watu wana dini zao au madhehebu yao lakini bado ni watenda dhambi, utakuta niwaongo, wasengenyaji, watu wa kulaumu, wanafiki, wasingiziaji, washirikina, hawaamini nguvu za Mungu, wanapenda mitindo ya kidunia, wanaziabudu fedha, wazinzi n.k. Waaminifu kushika taratibu za dini lakini sio maagizo ya Yesu na wala hawatembei katika njia za utakatifu ambayo ndio sifa kubwa ya Mkristo.

**Ukweli na Msaada ni Huu**

Yesu ndiye msingi na kichwa cha kanisa na katika yeye utimilifu wote umesitirika. (***Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote. Wakolosai 1:18***), (***Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. Waefeso 5:23***). Kwa maana kitabu kitakatifu Biblia yote inamuelezea Yesu tangu Mwanzo mpaka Ufunuo. ***"Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe. Luka 24:27***" angalia pia "***Kwa maana manabii wote na torati walitabiri mpaka wakati wa Yohana. Mathayo 11:13***".

Madhehebu yetu ya leo ni kama majukwaa tu ambayo yanatangaza habari za Yesu na kuwaalika watu katika wokovu mkuu wa Yesu lakini msingi wa kanisa ni Yesu mwenyewe na ndiye mwenye kanisa. Hakuna kanisa au dini leo ya kuwapeleka watu mbinguni au kuwapa uhakikisho wa wao kuingia mbinguni isipokuwa ni kwa Yesu Kristo pekee. ***"Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi. Yohana 14:6"***

Yesu kishatoa msingi na muongozo wa jinsi mtu yeyote awe, yaani ni ule wokovu ambao mtu huupata baada ya kumwamini Yesu kama Bwana na mwokozi wa maisha na baada ya hapo mtu huyo ataitwa amekombolewa (mteule, mwamini, mtakatifu, kanisa, mkristo); na (2) atatakiwa kuacha dhambi zote na kuanza maisha mpya ndani ya Yesu (***Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa***

***kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya. 2Wakorintho 5:17***) na kuishi maisha matakatifu na kutenda mema (Ebr 12:14); (3) kuwa mtu wa maombi mengi ("***Akawaambia mfano, ya kwamba imewapasa kumwomba Mungu sikuzote, wala wasikate tamaa. Luka 18:1")***; (4) kusoma Neno la Mungu na kuliishi

(Zab 119:105; 2Tim 3:16-17), (5) kujiepusha na mambo ya dunia yaliyo kinyume na Mungu (1Yoh 2:1517), (6) kujumuika pamoja na watakatifu wengine kwa ibada na kujengana kiroho (Ebr 10:25; Mt 18:1920), (7) kuwaeleza wengine habari za ukombozi yaani Yesu Kristo (Mt 28:19). Mtu huyu atakuwa ni mtakatifu na Yesu anamhakikishia ulinzi dhidi ya Shetani na mapepo yake, ulinzi dhidi ya mabaya, uponyaji wa afya na mengine mengi. Pia anamhakikishia uzima wa milele kama mtu huyu atadumu katika kuvumilia katika Imani na kuyashika hayo. (***wale ambao kwa saburi katika kutenda mema wanatafuta utukufu na heshima na kutokuharibika, watapewa uzima wa milele. Warumi 2:7***), Yn 5:24; 10:28;

17:15

Leo hii kila dhehebu na misimamo yake lakini hayo yanajaribu kuwaelekeza watu katika njia ya Yesu Kristo, sasa utofauti wa itikadi za kidhehebu au kidini isiwe sababu ya kuwakosesha watu kuingia katika ufalme wa Mungu yaani kumwamini Yesu Kristo. Na pia kila mtu anapaswa kumtazama Yesu kibinafsi na sio dini au dhehebu. Mtu asijivunie dini, dhehebu wala kanisa lake bali amtukuze Mungu kwasababu amempata Yesu moyoni mwake na kuishi maisha matakatifu.

Si kanisa, dhehebu wala dini itakayo waokoa wanadamu, bali kama mtu binafsi ataamua kumwamini na kumpa Yesu Kristo maisha yake ataokoka na kuwa kanisa halisi la Mungu na huyo ndiye Yesu anaye mtazama na kumwangalia kama mteule wake na mrithi wa ahadi za Mungu.

***"Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu. Kwa maana andiko lanena, Kila amwaminiye hatatahayarika.Warumi 10:9-11"***

***"Amin, amin, nawaambia, Yeye aaminiye yuna uzima wa milele. Yohanan 6:47"***

***"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu
Bwana wetu. Warumi 6:23"***

*"katika tumaini la uzima wa milele, ambao Mungu asiyeweza kusema uongo aliuahidi tangu milele. Tito 1:2" "ili tukihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu. Tito 3:7"*

*"ili tukihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu. 1Yohana 2:25" "Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. 1Yohana 5:11"*

# KITABU CHA YOELI

Kitabu cha Yoeli ni moja ya kitabu cha manabii wadogo, kinachopatikana katika kitabu cha agano la kale. Nabii Yoeli alihudumu katika upande wa Yuda.

**MWANDISHI**

Mwandishi wa kitabu hiki ni Yoeli mwenyewe **(Yoeli 1:1),** mwana wa Pethuel jina Yoeli ni muunganiko wa majina mawili yaani "yahwe na eli" yenye maana yahwe ni Mungu.

Yoeli anafahamika Zaidi kama nabii wa pentekoste kwa sababu yeye alitabili siku ya pentekoste kwa uwazi **(Yoeli 2:28-32)** alitabili watu watapokea roho mtakatifu kwa kila aaminiye na Yesu alikazia kwamba ni lazima aje uyo roho mtakatifu **(Yohana 14:16-20)** na utimilivu wa kile alichokitabili kilitimia siku ya pentekoste **(Matendo 2:14-22**), na mtume Petro pia alinukuu kile kilichotabiliwa na nabii yoeli katika ile siku ya pentekoste katika kuwaelewesha watu kuwa huo ulikuwa ni nguvu ya Mungu ndani yao.

**MUDA WA KUANDIKWA**

538-796 K.K

Japo tarehe na muda sahihi na mwaka haujulikani kwa sababu kitabu hakijataja hata jina la mfalme yeyote, hivyo muda haujulikani.

Zipo sababu kuu mbili zinazotufanya tuamini kuwa kitabu hiki cha Yoeli kiliandikwa muda huu 538-796 K.K:-

i. **UTHIBITISHO KULINGANA NA MATUKIO YA KITABU.**
   Matukio yaliyoripotiwa katika kitabu yanatupa uthibitisho kuwa ni mwaka 538-796 k.k tukilinganisha **(Yoeli 3:4-19)** kulingana na mahusiano yake ya Tire, Sidon,Philistia, Misri na Edomu kama maadui. hawa walikuwa maadui wa kwanza kabisa wa ufalme wa kusini (Yuda) kabla ya uhamishoni Babeli na baada ya uhamisho wao adui zao walikuwa ni Asiria, Wababeli na Pesia.

ii. **UTHIBITISHO KULINGANA NA HISTORIA YA YUDA.**

Baadhi ya wachambuzi wa historia wanaamini kitabu hiki kiliandikwa kipindi cha mfalme Yosia aliyetawala akiwa na umri wa miaka 8 uko Yuda **(2wafalme 22:1-2)** na alifanya matengenezo makubwa pia kwa kuwa kitabu ni cha matengenezo na mfalme hakutajwa kwa sababu ya umri wake mdogo hivyo tunaamini kiliandikwa mwaka 538 - 796 kutokana na ujumbe wa kitabu ni wa matengenezo na mfalme Yosia alifanya matengenezo makubwa ya pasaka hadi Mungu alisema hii ni pasaka kubwa ambayo haijawai kutokea tangu enzi za waamuzi **(2 wafalme 23:21-24)**. hivyo kitabu kinaaminika kiliandikwa katika mwaka huo. *(kwa uthibitisho Zaidi wa matengenezo rejea 2 wafalme sura ya 22 na 23).*

**NIA NA MAKUSUDI.**

a) **KUTANGAZA SIKU YA BWANA YA HUKUMU DHIDI YA UOVU WA YUDA.**

Yoeli anatumia ukame na nzige zitakazoshambulia Yuda na kutumia jeshi kama adhabu kwa Yuda baada ya kuacha kumuabudu Mungu wa kweli **(Yoeli 1:14-16, Yoeli 1:8-9)** na kuvunja maadili na utu wa mwanadamu yaani dhambi za kiibada na dhambi dhidi ya utu wa mwanadamu mfano ulevi, uzinzi, dhuruma n.k.

**NB:** Kitabu cha Yoeli wakati wowote mwanadamu anapoacha ibada ya kweli na **kuvunja maadili ya utu kwa mwanadamu Mungu huleta adhabu** kwa sababu ya makosa ya mwanadamu, Yoeli anatangaza siku ya Bwana kwa sababu ya kuvunja tunu ya Mungu kwa wanadamu. Tunu hizo ni kama ifuatavyo:-

1. Kumuabudu Mungu wa kweli
2. Kuishi kwa upendo
3. Uwajibikaji
4. Utu wema(huruma,kufadhiliana,kuvumiliana na kuheshimia)
5. Umoja

Mwanadamu anapoacha mambo haya mara nyingi hujikuta katika mazingira mabaya na ndio sababu ya mateso ya Yuda.

b) **WITO WA TOBA YA KWELI NA MATENGENEZO**

Kitabu cha Yoeli hakiishii kutaja mabaya tu bali kinaonyesha njia ya kuepuka mabaya hayo na njia sahihi ya kuepuka adhabu ya Mungu ni toba ya kweli na sio taratibu za kidini au dhehebu bali ni badiliko la ndani la kuacha uovu **(Yoeli 1:13-20, Yoeli 2:1-17) na kwa nyakati tulizo nazo leo toba ya kweli ni kumwamini Yesu Kristo na kazi ya msalaba iondoayo dhambi na kuamua kufuata tunu za Mungu** (Tuishi maisha ya upendo na imani)

c) **KUTANGAZA NEEMA NA UPENDO WA MUNGU KWA WATU WAKE**

Kitabu cha Yoeli kinatangaza neema na upendo wa Mungu kwa watu wote hasa wenye dhambi, nia ya Mungu ni kuwarejea watu wake kwa upendo na kuwasamehe, kuwarudishia vitu walivyonyang'anywa katika uzalimu wao **(Yoeli 2:18-26)** hakika Mungu wa upendo na msamaha na huruma kwa wote wanaotaka kumrejea

**NB:** Tunaposoma kitabu cha yoeli tusitazame hukumu ijayo kutokana na maovu yetu **bali tuutazame wema, neema na upendo wa Mungu kwa wenye dhambi**.

Yoeli kama manabii wa agano la kale wote walikuwa wakitabili habari za Yesu Kristo, yoeli aliyetabiri mmwagiko wa Roho mtakatifu **(Yoeli 2:28-32)** linganisha na **(Yohana 16:7-15) (Matendo 1:8) (Yoeli 2:28-30)** Zaidi Yesu ametabiliwa kuwa muhukumu wa kimataifa **(Yoeli 3:2-12).** pia Yesu kama nguzo na kimbilio la utukufu wa Yuda **(Yoeli 3:16)**

***Wito wa Anil Blaster kwa wote watakao soma: watu wamwini Yesu Kristo kama mwokozi wa maisha yao na alikufa kwa ajili ya dhambi zetu ili tuwe huru. upendo huo aliotuonyesha Kristo yatupasa tuuoonyeshe kwa watu wote tunaoishi nao.***

***Prepared by Anil Michael***

***0783 067 297/ 0676 771 585***